

**FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA
KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE
KUKATALIWA**

الفوائد المقصودة في بيان الأحاديث الشاذة المردودة

Kimeandikwa na:

Sharifu Abdullah bin Muhammad bin
as-Siddiq al-Ghamari al-Hasani

Kimetarjumiwa na:

Amiri Mussa Kea

ترجمة

الفوائد المقصودة في بيان الأحاديث الشاذة المردودة

تأليف

الشيخ عبد الله بن محمد بن الصديق الغماري الحسني

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

©**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 – 17 – 046 – 3

Kimeandikwa na:
Sharifu Abdullah bin Muhammad bin
as-Siddiq al-Ghamari al-Hasani

Kimetarjumiwa na:
Amiri Mussa kea

Kimehaririwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

Kimesomwa Profu na:
Al-Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitiwa na:
Mujahid Rashid

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Desemba, 2016
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.alitrah.info

YALIYOMO

Dibaji	1
Neno la Mchapishaji	2
Utangulizi.....	3
Hadithi zisizokuwa za kawaida:	16
Hadithi ya Kwanza:	21
Hadithi ya kijakazi: Yuko wapi Mwenyezi Mungu?.....	21
Hadithi ya Pili:	27
Hadithi inayomkataza Mtume kumuomba msamaha mama yake	27
Hadithi ya Tatu:	28
Hadithi inayosema: Hakika baba yangu na baba yako ni wa motoni.....	28
Hadithi ya Nne:	34
Hadithi ya watu wa namna nne ambao watatoa udhuru Siku ya Kiyama; Kiziwi, kikongwe, mpumbavu na mtu aliyekufa zama za ujinga	
Hadithi ya Tano:.....	35
Hadithi ya kwamba bwana wetu Jibrail aliingiza udongo kinywani mwa Firaun	
Hadithi ya Sita:	36
Kila ardhi ina Adam kama Adam wenu	
Hadithi ya Saba:.....	37
Hadithi ya Unyonyeshaji, aliingia mbuzi nikamla	
Hadithi ya Nane: Matanga ya mwanamke: Vaa vipande vitatu vya nguo kisha fanya upendavyo	38

Hadithi ya Tisa:	39
Kula daku baada ya Alfajiri na kabla ya kuchomoza jua.....	39
Hadithi ya Kumi:	41
Mwenyezi Mungu ameumba mchanga siku ya Jumamosi	41
Hadithi ya Kumi na Moja:	41
Maombi matatu ya Abu Sufiyan kwa Mtume	41
Hadithi ya Kumi na Mbili:	43
Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi kwa kuyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa misikiti.....	43
Hadithi ya Kumi na Tatu:	48
Hadithi ya Abbas.....	48
Hadithi ya Kumi na Nne:	51
Kiti ni mahala pa nyayo mbili.....	51
Hadithi ya Kumi na Tano:	52
Mwenyezi Mungu ataweka unyayo wake motoni, utasema: Basi basi.....	52
Hadithi ya Kumi na Sita:	55
Hakuna mtu yeyote mwenye wivu zaidi kuliko Mwenyezi Mungu (s.w.t)	55
Hadithi ya Kumi na Saba:	56
Alikuwa bwana wetu Adam akifanya tasbihi za Malaika pindi aliposhuka.....	56
Hadithi ya Kumi na Nane:	57
Pindi Mwenyezi Mungu alipomaliza kazi ya umbaji alilala chali.....	57

Hadithi ya Kumi na Tisa:	61
Waumini wa kijini hawaingii peponi	61
Hadithi ya Ishirini:	62
Hadithi ya Kiyahudi na vidole	62
Hadithi ya Ishirini na Moja:	64
Hadithi ya ukaaji juu ya kiti na vidole vinne	64
Hadithi ya Ishirini na Mbili:	66
Hadithi ya sauti ya kipandona kwamba Arshi ni kama vile tungi.....	66
Hadithi ya Ishirini na Tatu:	68
Malaika wameumbwa kutokana na nuru ya dhiraa mbili na kifua	68
Hadithi ya Ishirini na Nne:	68
Hakika Mtume (s.a.w.w) alimuona Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika uwanja wa kijani	68
Hadithi ya Ishirini na Tano:	71
Hadithi ya ukaaji nasauti ya kipando	71
Hadithi ya Ishirini na Sita:	73
Hadithi ya Dajjal na kwamba yeye ni chongo na Mola Wenu sio chongo	73
Hadithi ya Ishirini na Saba:	74
Hadithi ya Swala ya hofu ni rakaa moja	74
Hadithi ya Ishirini na Nane:	75
Hadithi ya Talaka tatu za pamoja ni moja.....	75
Hadithi ya Ishirini na Tisa:	77

Kauli ya Mtume (s.a.w.w)kwa mlemavu wa macho ikiwa unasikia wito ni wajibu zaidi	77
Hadithi ya Thelathini:	78
Hadithi kuhusiana na tayammamu mpaka mabegani na kwapani.....	78
Hadithi ya Thelathini na Moja:	79
Hadithi ya kumuona Mola Manani na ndani yake: Hakika mmoja wenu atahudhuria kwa Mola wake Mlezi	79
Hadithi ya Thelathini na Mbili:.....	80
Mkirimuni shangazi yenu mtende.....	80
Hadithi ya Thelathini na Tatu:	81
Mwanamke alitoka kwa ajili ya Swala basi akakutana na mwanaume	81
Hadithi ya Thelathini na Nne:	84
Mwanamke mmoja alimwambia Nibi Aisha: Nimemuza kijakazi kwa mia nane	84
Hadithi ya Thelathini na Tano:.....	85
Huu ndiyo wudhuu ulivyo basi yule anayezidisha au kupunguza kwa hakika amefanya uovu na amedhulumu.....	85
Hadithi ya Thelathini na Sita:	87
Mbingu ilinyesha barafu basi Abu Twalha akala hiyo naye akiwa amefunga.....	87
Hadithi ya Thelathini na Saba:.....	88
Muunganisheni na aliyetutangulia mwema Uthman bin Madhuun	88

Hadithi ya Thelathini na Nane:	88
Tulikuwa tukiwafanyia Talbiya wanawake.....	88
Hadithi ya Thelathini na Tisa:	89
Anayemuosha maiti basi aoge	89
Hadithi ya Arubaini:.....	90
Kufuturu nyumbani kwake yule anayetaka kusafiri kabila ya kuanza safari	90
Hadithi ya Arubaini na Moja:	93
Kuhusiana na uchinjaji: Kama utamchinja (mnyama) pajani itatosheleza	93
Hadithi ya Arubaini na Mbili:	93
Hadithi ya bwana wetu Jibrail kuwa alikuja na kioo cheupe.....	93
Hadithi ya Arubaini na Tatu::	96
Hadithi ya unyonyeshaji mara tano.....	96

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

SMS: +255 778 300 140

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina, *al-Fawaidu 'l-Maqsudatu fi Bayani 'l-Ahadith ash-Shadhata 'l-Mardudah* kilichoandikwa na Sharifu Abdullah bin Muhammad bin as-Siddiq al-Ghamari al-Hasani.

Mwandishi wa kitabu hiki amefanya utafiti wa kisomi kwa ajili ya kubaini hadithi zisizo sahihi ambazo kwazo amehusishwa nazo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Mitume waliomtangulia, Maimamu Watoharifu, Jibrail, wakeze Mtume na wachamungu wengine kwa masilahi na malengo ya watu binafsi.

Sisi tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana husasan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Amiri Mussa kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kwa Kiswahili; pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

MCHAPISHAJI
AL-ITRAH FOUNDATION

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu
Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu, rehema na amani ziwe juu ya Bwana wetu Mtume Muhammad 3na Aali zake wema watoharifu, na radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Masahaba wake wachamungu, na yule mwenye kuwafuata hao kwa wema hadi siku ya mwisho.

Ama baada: Kitabu hiki **Faida Zenye Kukusudiwa Katika Kubainisha Hadithi Zisizokuwa za Kawaida**, cha bwana wetu na Sheikh wetu Imam mwanahadithi Sayyid Abdullah bin Muhammad bin Swadiiq Ghamariy Hasaniy, ambaye alizaliwa huko Thaghru Twanjat, moja kati ya miji ya nchi ya Moroko, mnamo mwaka 1328 AH, na aliyefariki sehemu katika mji huo mwezi 20 Shaban 1413 AH, sawa na tarehe 11/2/1993 AD, ndani yake kuna vidokezo vina-voasisi kanuni ambazo kwazo hujulikana hadithi zisizokubalika, ili itimie kauli yake (s.w.t):

وَمَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ
الْحَقِّ شَيْئًا

**“Nao hawana ujuzi wowote wa hayo isipokuwa wanafuata dhana tu,
na hakika dhana haifai kitu mbele ya haki.” (an-Najm; 53:28)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا
بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ

“Enyi ambao mmeamini! Akiwajia fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyotenda.” (al-Hujurat; 49:6).

Na ni kufanyia kazi maelezo yaliyokuja katika hadithi sahihi ya Mtume ﷺ: “Mtakapoisikia hadithi kutoka kwangu ambayo nyoyo zenu zinajua, na inalainisha hisia zenu na bishara zenu, na mnaona kwamba inafaa kutoka kwenu, basi mimi ni mbora zaidi kwayo kuliko ninyi, na mtakapoisikia hadithi kutoka kwangu, ambayo zinakataa nyoyo zenu na zinachukia hisia zenu na bishara zenu, na mnaona kwamba hiyo haifai kutoka kwenu, basi mimi nipo nayo mbali zaidi kuliko ninyi.”¹

Na akasema Khatwiib Baghdadi katika kitabu chake kiitwacho *Al-Faqihu wal-Mutafaqqahu*, uk. 132: “Mlango wa mambo yanayopelekea habari ya mtu mmoja kukataliwa: ... na akipokea mtu mkweli na mwaminiwa habari yenye sanad ya kuunganika hukataliwa kwa sababu ya mambo yafuatayo:

La kwanza: Iwapo inakwenda kinyume na yale ambayo yanawajibishwa na akili, hivyo hujulikana ubatili wake kwa sababu sharia inaleta yale yanayokubaliwa na akili, wala haileti yale yaliyo kinyume na akili.

¹ Ameipokea *Ahmad bin Hanbali*, Juz. 3, uk. 497 na Juz. 5, uk. 425 na Ibn Haban katika *Sahih* yake Juz. 1, uk. 264 na Twahawi katika kitabu *Mishkilil-Athaar*, Juz. 15, uk. 344, na Ibn Saad katika kitabu *Twabaqaatul-Kubra*, Juz. 1, uk. 387 na *Al-Bazar*, Juz. 1, uk. 105, *Kashful-Astaar* na akaisahihisha hiyo mpingaji wa zama zetu Albani katika *Sahih* yake, Juz. 2, uk. 369 nambari 732 na Sheikh Shuaib na Ahmad Shakir, na akasema Hafidh Haythami katika kitabu *Majmau Zawa'id*, Juz. 1, uk. 150: Ameipokea Ahmad na Al-Bazar na watu wake ni watu wa Sahihi.

La pili: Iwapo inatofautiana na andiko la Kitabu na Sunnah iliyo mutawatiri, basi hapo inajulikana kwamba haina asili au ni yeye kufutwa.

La tatu: Iwapo inatofautiana na ijmai, basi hapo inathibiti kuwa ni yenye kufutwa au haina asili, kwani haijuzu iwe ni sahihi ambayo haijafutwa, kisha umma ukongamane juu ya kinyume chake.

La nne: Iwapo ni mtu mmoja tu ndiye aliyepokea hadithi ambayo ni wajibu viumbe wote wajue, basi inajulisha hali hiyo kwamba hadithi hiyo haina asili, kwani haijuzu iwe na asili kisha awe ni yeye peke yake baina ya viumbe wote ndiye mwenye kuijua hadithi hiyo...”

Hakika kanuni hizi zimefanyiwa kazi na wanazuoni na Masahaba watukufu, na juu ya hilo kuna mifano mingi ndani ya Sahihi Mbili na katika vitabu vingine miongoni mwa vitabu mama vya hadithi. Na alikuwa Imam Malik رحمته الله akirudisha na kuzikataa hadithi zinapoto-fautiana na amali ya watu wa Madina, kama vile kuswali katikati ya khutba na nyinginezo kama lilivyo hilo maalum na mashuhuri kwa watu wa elimu.

Na alikuwa Ahmad bin Hanbali akiamrisha kuitupilia mbali hadithi na kuipuuza wakati inapopingana na kitu miongoni mwa yale ya kukata shauri au yaliyosihi zaidi, na lau habari ya mtu mmoja ingekuwa inafaidisha elimu na yakini basi isingetupiliwa mbali, na haya ndiyo madhehebu yake ambayo alikuwa nayo kipindi cha maradhi yake ya mwisho ambayo alifia: Kwa hakika *Bukhari* amepokea katika kitabu *Fat'hul-Bari*, Juz. 6, uk. 612 na *Muslim* 2917 na Ahmad bin Hanbali katika *Musnad* yake, Juz. 2, uk. 301 hadithi isemayo: “Atauangamiza umma wangu huu, mtu hai kutokana na Qurayshi, wakasema: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, lipi unatuamrisha sisi? Akasema: Ni vizuri watu wakajitenga nao.” Abdul-

lah bin Imam Ahmad amesema huko katika kitabu *Musnad* baada ya hadithi hii moja kwa moja: [Amesema baba yangu katika maradhi yake aliyofia: ‘Itupilieni mbali hadithi hii kwani inakwenda kinyume na hadithi zilizopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ yaani kauli yake: ‘Sikieni, mtii na subirini.’]

Na kuhusu Masahaba رضي الله عنهم kuna mifano chungu nzima katika Sahihi Mbili na vitabu vinginevyo, ambayo inaonesha kwamba Masahaba walizirudisha na kuzikataa hadithi zilizothibiti katika Sahihi Mbili, na hawakuzikubali kwa kuwa zinapingana na zile za yakini walizonazo. Basi la kwanza lililozuka katika Uislamu kutokana na elimu ya ukosoaji wa hadithi ni ukosoaji wa matini kabla ya ukosoaji wa sanad, kwani haikuwa katika sanad ila mtu mmoja, naye ni sahaba mpokezi aliyepokea toka kwa Mtume, na miongoni mwa mifano yake ni:

1. Ukanushaji wa Bibi Aisha رضي الله عنها madai ya kwamba hakika maiti huadhibiwa kwa kuliliwa na watu wake wa karibu: Bibi Aisha رضي الله عنها alimpinga bwana wetu Umar na mwanawe Abdullah رضي الله عنه katika hadithi isemayo: “Anaadhibiwa maiti kwa kuliliwa na watu wake wa karibu.” Hakika amepokea Bukhari katika kitabu *Fat’hu*, Juz. 3, uk. 151 – 152, na *Muslim*, Juz. 2, uk. 638 – 642, kwamba hakika bwana wetu Umar na mwanawe bwana wetu Abdullah wamepokea kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema: “Hakika maiti anaadhibiwa kwa kuliliwa na watu wake wa karibu.”

Basi Bibi Aisha رضي الله عنها akaikataa hiyo na akasema kama ilivyo katika *Sahihi Muslim* 932, kutoka kwa Umrat hakika yeye alimsikia Bibi Aisha iliposemwa mbele yake kwamba hakika Abdullah bin Umar anasema: ‘Hakika maiti anaadhibiwa kwa kuliliwa na mtu aliye hai.’ Alisema: ‘Mwenyezi Mungu amsamehe baba yangu Abdul-Rahman.

Ama hakika yeye hakuadhibiwa, lakini alisahau au alikosea. Hakika Mtume ﷺ alipita kwa mwanamke wa Kiyahudi aliyekuwa akililiwa na watu wake akasema: Hakika wao wanamlilia yeye, kwa hakika yeye anaadhibiwa kaburini mwake.”

Na katika hadithi ya Bukhari 1288: Kutoka kwa Ibn Abbas رضى الله عنه amesema: “Nilimtajia hilo Aisha رضى الله عنها akasema: ‘Mwenyezi Mungu amrehemu Umar, naapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mtume ﷺ hakusema hakika Mwenyezi Mungu anamwadhibu muumini kwa kuliliwa na watu wake wa karibu! Lakini Mtume ﷺ amesema: ‘Hakika Mwenyezi Mungu anamzidishia kafiri adhabu kwa kuliliwa na watu wake wa karibu.’ Na akasema Aisha: Inawatosha nyinyi Qur’ani, inasema: “Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine.....” (6:164).

Amesema Imam Hafidh Nawawi katika *Sharhu Sahih Muslim*, Juz. 6, uk. 228: “Na hadithi hizi ni kutokana na hadithi za Umar bin Khatwab na mwanawe Abdullah رضى الله عنه na amezikanusha Aisha, na akawahusisha wao wawili na usahaulifu na ukoseaji. Na akakanusha hilo kutoka kwa Mtume ﷺ na kwamba hakulisema hilo, bali akalitolea hoja kwa kauli yake (s.w.t): **‘Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine.....’ (6:164)**. Akasema (Aisha): ‘Hakika Mtume ﷺ alisema kuhusiana na mwanamke wa Kiyahudi ambaye alikuwa akiadhibiwa na wao wakimlilia, yaani anaadhibiwa kwa ukafiri wake wakati wa kuliliwa na watu wake wa karibu, na si kwa sababu ya kilio chao.”

Nasema: Na imekuja katika hadithi chungu nzima kwamba hakika Mtukufu Mtume ﷺ alimlilia maiti, na pia alinyamaza kuhusiana na kumlilia maiti. Hivyo basi mwenye kutafakuri na kuingatia hadithi hii: “Maiti anaadhibiwa kwa kuliliwa na watu wake wa karibu,” iliyomo katika Sahihi Mbili, nayo ni miongoni mwa habari za mtu mmoja, aidha ameikataa Bibi Aisha kwa andiko la kukata shau-

ri la Qur’ani Tukufu: “Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine....” (6:164), atajua kwamba hadithi ya mtu mmoja hata kama wawili (Bukhari na Muslimu) wataipokea kutoka kwa Mtume ﷺ bado haifaidishi ila dhana. Na ile ambayo haileti faida ila dhana, yaani ambayo huenda ndani yake kuna makosa, vipi ijengewe juu yake itikadi mbalimbali?! Na je, inafaa Mwislamu kuitakidi kuhusiana na dhati ya Mwenyezi Mungu, kwa vitu ambavyo huenda ikadhiri baadaye kuwa vilikuwa na makosa?! Na kwa nini inaitwa itikadi ikiwa haijajengeka juu ya vithibiti ambavyo haiwezekani kutokea juu yake mambo yatakayoitengua?!!

1. Mfano mwingine: Ukanushaji wa Bibi Aisha na Ibn Abbas kuhusiana na ile hadithi ambayo imepokewa kwamba Swala inakatwa na mbwa, punda na mwanamke. Amepokea Muslim katika *Sahih Muslim* 510 na 511, kutoka kwa Abu Huraira na Abu Dharr رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ amesema: “Anakata Swala mwanamke, punda na mbwa, na kinazuia hilo kitu mfano wa mkia wa kipando.”

Amekosoa hilo Bibi Aisha رضي الله عنها na wala hakuangalia sanad!! Hakika Bukhari amepokea 511 na Muslim 512, kutoka kwa Masruuq kutoka kwa Bibi Aisha رضي الله عنها kwamba lilitajwa kwake jambo ambalo linakata Swala, kwamba ni mbwa, punda na mwanamke! Akasema (Aisha): “Hakika mmetufanya sisi mambwa, hakika nilimuona Mtume ﷺ akiswali hali mimi nipo kati yake na Kibla nikiwa nimejilaza juu ya kitanda, ninapokuwa na haja nachukia kumuelekea yeye hivyo ninapita kiubavu....”

Vile vile amekosoa hilo Ibn Abbas رضي الله عنه na wala hakuangalia sanad yake. Hakika amepokea Ibn Haban katika kitabu chake Juz. 6, uk. 143, Swahban amesema: “Tulikuwa kwa Ibn Abbas, basi tukataja vile ambavyo vinakata swala, wakasema: Punda na mwanamke.

Akasema Ibn Abbas^L: ‘Hakika nilikuja mimi pamoja na kijana kutoka katika ukoo wa Bani Abdul-Mutwalib, akiwa juu ya punda, na Mtume ﷺ akiwaswalisha watu katika ardhi ya jangwa. Tukamwachacha punda mbele yao na kisha tukaja mpaka tulipoingia kati yao, wala (Mtume) hakujali hilo.’”

Na hakika amepokea Bukhari 76, 493, na Muslim 504 kutoka kwa Abdullah bin Abbas ^{رضي الله عنه} kuwa amesema: “Nilikuja nikiwa nimepanda juu ya punda wa Atani – na mimi siku hiyo nimepatwa na kujiotea – na Mtume ﷺ akiwa anaswali Mina pasi na kuwepo ukuta, basi nikapita mbele ya mistari na nikamtuma Atani Tartau, basi nikaingia katika mstari hakunikemea mimi kuhusu hilo.”

Kadhalika Bibi Aisha ^{رضي الله عنها} alimpinga Abu Huraira ^{رضي الله عنه} kuhusiana na hadithi ya mkosi, isemayo kwamba mkosi upo katika mambo matatu; kwa mwanamke, nyumba na farasi: Amepokea *Abu Daud Tway-alisi* uk. 215 kutoka kwa Mahkuul kwamba Aisha aliambiwa, hakika Abu Huraira anasema kuwa Mtume ﷺ amesema: “Mkosi upo katika mambo matatu; kwenye nyumba, mwanamke na farasi” Aisha akasema: Abu Huraira hakuhifadhi kwani yeye aliingia na kumkuta Mtume ﷺ akisema: “Mwenyezi Mungu awaue Mayahudi wanaosema hakika mkosi upo katika mambo matatu; kwenye nyumba, mwanamke na farasi.” alisikia mwisho wa hadithi na wala hakisikia mwanzo wake.

[Hadithi ya mkosi ameipokea Ibn Umar ^{رضي الله عنه} katika *Bukhari* 5753 na *Muslim* 2225 kwa lafudhi: “Si kukosa bahati wala si mkosi, hakika mkosi upo katika mambo matatu; kwa mwanamke, farasi na nyumba.”]

Ninasema: Makuhul hakisikia kutoka kwa Bibi Aisha ^{رضي الله عنها} kama ilivyokuja katika kitabu *Fat'hul-Bari*, Juz. 6, uk. 61 ila ni kwamba hakika athari hii au hadithi hii ina ufuatiliwaji, Hafidh amesema: Amepokea Ahmad, Ibn Khuzaima na Hakim kutoka ka-

tika njia ya Qatadah kutoka kwa Abu Hasaan: “Hakika watu wawili wanaotokana na Ukoo wa Aamir waliingia kwa Aisha wakasema: Hakika Abu Huraira amesema: Hakika Mtume ﷺ amesema: ‘Mkosi upo kwenye farasi, mwanamke na nyumba’, Aisha akaghadhibika ghadhabu kubwa akasema: ‘Hakusema hivyo, bali alisema: Hakika watu wa zama za ujinga walikuwa wakiona kwamba mkosi unapatikana katika mambo hayo.’”

Nasema: Na asili ni kwamba hakuna imani ya kupata mkosi katika Uislamu, hakika imani ya kupata mkosi ni amali mbaya isiyo-faa ambayo inamkokota mhusika hadi motoni, na tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka kwalo, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

قَالُوا إِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ لَئِن لَّمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُم مِّنَّا عَذَابٌ
أَلِيمٌ قَالُوا طَائِرُكُمْ مَعَكُمْ ؕ أَلَيْسَ ذُكِّرْتُمْ ؕ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ

“Wakasema hakika sisi tunapata mkosi kwa ajili yenu, kama hamta-koma basi hakika tutawapiga mawe na itawafika adhabu chungu kutoka kwenu. Wakasema: mkosi wenu mnao wenyewe. Je, ni kwa kuwa mnakumbushwa? Bali nyinyi ni watu mnaopituka mipaka.”
(36:18-19), na imekuja katika hadithi kwamba hakika Mtume ﷺ amesema: “Imani ya kupata mikosi ni shirki.”

Hafidh Mandhuri katika kitabu *Targhiib*, Juz. 4, uk. 64 amesema: “Ameipokea Abu Daud na Tirmidhiy akasema: “Ni hadithi hasan sahihi,” na kwa hivyo Bibi Aisha رَضِيَ اللهُ عَنْهَا kaikataa na kuirudisha, na ikadhihiri kwetu sisi kurudishwa kwake. Hakika mpokezi wa habari ya mtu mmoja hata akiwa katika tabaka la juu la kuaminiwa kama vile Sahaba Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ hakika habari yake haileti yakini na uhakika, na kwa hivyo umefaa urudishwaji wake kwa kupingwa na Aya ya Qur’ani na habari mutawatiri.

Na hakika amepokea *Bukhari* 3199 na *Muslim* 159 kutoka katika njia ya Ibrahim Taymiy kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه amesema: Mtume عليه السلام alisema kumwambia Abu Dharr رضي الله عنه pindi jua lilipozama: “Je, unajua linakwenda wapi?” Nikasema: Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanajua zaidi. Akasema: “Hakika linakwenda hadi linafika na kusujudu chini ya Arshi, linaomba idhini na linapewa idhini, na linakaribia kusujudu tena lakini hali-kubaliwi, linaomba idhini lakini halipewi, linaambiwa rudi utokako, na ndipo linachomoza kutoka Magharibi na hiyo ndio kauli yake (s.w.t):

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

“Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye nguvu, Mwenye kujua.” (36:38)

Na yote haya kwa mtazamo wangu yamechukuliwa kutokana na kauli ya Mtume عليه السلام, na kanuni zilizotegemewa katika kuasisi hilo zimechukuliwa kutoka katika kisa cha Dhulyadayni: Hakika ime-thibiti katika *Sahih Bukhari* Juz. 1, uk. 566 na *Muslim* Juz. 1, uk. 403 nambari 573, kwamba hakika Dhulyadayni alisema kumwambia Mtume عليه السلام pindi aliposwali Swala ya Adhuhuri au Alasiri raka mbili: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu je, umesahau au umepunguza Swala?” Akamwambia: “Sijasahau na sijapunguza.” Kisha akawaambia watu: “Je, nanyi ni kama asemavyo Dhulyadayni?” wakasema: Ndio. Basi akatangulia akaswali hakuacha kitu kisha akatoa salam.....

Nasema: Pindi aliposema Dhulyadayni kumwambia Mtume عليه السلام: Je, umesahau au umepunguza Swala? Kauli hiyo ilimpa dhana Mtume عليه السلام na si yakini, kwa kutegemea kwamba huenda Dhulyadayni amechanganya na kukosea, licha ya kwamba mpokezi alikuwa

mwadilifu, mdhibiti, mkweli naye ni Sahaba. Mtume ﷺ akawauliza watu na kati yao akiwa Abu Bakr na Umar رضى الله عنه na waliposadikisha habari ya Dhulyadayni na wao ni idadi ya tawaturi ndipo Mtume ﷺ akawa na uhakika na habari hiyo ikawa imejenga yakini.

2. Umar bin Khatwab رضى الله عنه aliikataa hadithi ya Fatima binti Qays, pale alipokuja kwa bwana wetu Umar akieleza kwamba mumewe alikuwa amemwacha zama za Mtume ﷺ na ikathibitika talaka yake, na wala Mtume ﷺ hakumuwekea matumizi wala malazi, bali alimwambia yeye: “Kaa eda katika nyumba ya Ibn Ummi Maktum kwani yeye ni mlemavu wa macho.” Umar hakukubali hilo kutoka kwake, akasema: “Hatuachi Kitabu cha Mola Wetu Mlezi na Sunnah ya Nabii wetu kwa kauli ya mwanamke. Hatujui huenda yeye amehifadhi au amesahau.” Mwenyezi Mungu anasema: **“Msiwatoe katika nyumba zao...” (65:1).**

Nasema: Na imethibiti katika *Sahih Muslim*, Juz. 2, uk. 1116 vile vile ukataaji wa Bibi Aisha رضى الله عنها juu ya hilo, kama alivyokataa bwana wetu Umar رضى الله عنه. Basi angalia hapa vipi bwana wetu Umar hakuikubali habari ya Fatima bint Qays pamoja na kuwa kwake (Fatima) ni Sahaba mwenye kuaminiwa, kwakuwa habari yake inapingana na Aya, na kwayo inabainika kwamba hakika habari ya mtu mmoja huzingatiwa ni mkosa na hukataliwa ikiwa itapingana na lile ambalo limethibiti na lenye yakini, na akiwa bwana wetu Umar رضى الله عنه ameikataa habari ya mtu mmoja katika suala la kifikihi basi vipi likiwa ni suala la kiitikadi ambalo linahitaji andiko lenye kukata shauri ambalo haifai kuingiwa na kosa na mkanganyiko?!!

Amesema Hafidh katika wasifu wa bwana wetu Umar bin Khatwab رضى الله عنه katika kitabu *Tadhkiratul-Huffadh*, Juz. 1, uk. 6 na hili ndilo andiko lake:-

[Na yeye ndiye aliyewawekea wanahadithi utaratibu wa kuhakiki nukuu. Na wakati mwingine alikuwa anajizuia kuifanyia kazi habari ya mtu mmoja na anapokuwa na shaka. Amepokea Jariiri kutoka kwa Abu Nadhrat kutoka kwa Abu Said, kwamba hakika Abu Musa alimtolea salamu Umar bin Kwatwab nyuma ya mlango mara tatu lakini Umar hakumpa idhini. Abu Musa akarudi, Umar akamtumia mtu akisema: Kwa nini umerudi?! Akasema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema: ‘Anaposalimia mmoja wenu mara tatu asipojibiwa basi arudi.’ Umar رضى الله عنه akasema: ‘Je, unaweza kuniletea ushahidi juu ya hilo au nitakuadhibu wewe.’ Abu Musa akatujia hali amebadilika rangi yake na sisi hali tukiwa tumekaa, tukasema: Una nini? Akatupa habari na akasema: ‘Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliyesikia?’ Tukasema: Ndio, sote tumesikia. Basi wakamtuma mtu miongoni mwao pamoja naye mpaka kwa Umar, akampa habari.² Umar alipenda kuhakiki habari ya Abu Musa kwa kauli ya Sahaba mwingine. Katika hili ipo dalili kwamba habari ikipokewa na wakweli wawili inakuwa na nguvu zaidi na uzito zaidi kuliko ile iliyopokewa na mtu mmoja, na kwa ajili hiyo imesisitizwa kukithirisha njia nyingi za hadithi, ili hadithi ivuke kutoka daraja la dhana hadi daraja la elimu. Ikiwa mtu mmoja inawezekana kwake kusahau na kuchanganya, hilo halikaribii kuwezekana kwa wakweli wawili ambao hakuna aliyetofautiana nao.] Yamekwisha maneno ya Hafidh Dhahabi.

Na vile vile Hafidh Dhahabi ni miongoni mwa wanaosema habari ya mtu mmoja inafaidisha dhana, na hakika kila idadi ya wapokezi wa habari husika inapokuwa kubwa ndipo inapopanda kwenda kwenye daraja la yakini zaidi na kukaribia huko.

3. Na pia ukanushaji wa Bibi Aisha juu ya Abu Huraira katika hadithi nyingine: Amepokea Abu Daud Twayalisi katika *Musnad* wake uk. 199 kwa sanad sahihi kwa sharti la Muslim kutoka kwa

² Amejipokea *Bukhari* katika kitabu Fat’hu, Juz. 11, Uk. 27, *Muslim* na wengineo.

Alkamat, amesema: Tulikuwa kwa Aisha رضي الله عنها akaingia kwake Abu Huraira, akasema: “Ewe Abu Huraira wewe ni yule ambaye unaeleza kuwa mwanamke aliadhibiwa kutokana na paka wake aliyemfunga na hakumpa chakula na hakumnyweshwa maji?” Abu Huraira akasema: “Niliisikia hiyo kutoka kwa Mtume ﷺ.” Bibi Aisha akasema: “Je, unajua alikuwa ni mwanamke wa aina gani?!” Akasema: “Hapana.” Akasema: “Hakika mwanamke pamoja na aliyoyafanya alikuwa ni kafiri; hakika muumini ni mtukufu zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuweza kumwadhibu yeye kutokana na paka. Unapohadithia kutoka kwa Mtume ﷺ basi angalia vipi unahadithia.” Na katika ukanushaji huu kuna ubainifu wa wazi kwamba habari ya mtu mmoja inaweza kuwa na makosa, sasa vipi ujengwe juu yake msingi wa dini?!

4. Habari ya mtu mmoja inafaidisha dhana wala haifaidishi elimu na yakini kwa mujibu wa bwana wetu Abu Bakr Swiddiq رضي الله عنه:

Hafidh Dhahabi amesema katika kitabu *Tadhkiratul-Huffadh*, Juz. 1, uk. 2: Na alikuwa – Abu Bakr – wa kwanza kati ya waliochukua tahadhari kuhusiana na habari ya mtu mmoja. Amepokea Ibn Shahab kutoka kwa Qabiswat bin Dhuwaib kwamba hakika ajuza alikuja kwa Abu Bakr akiomba urithi, akasema: “Sipati katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu haki yako.” Kisha hapo akawauliza watu, akasimama Mughira akasema: “Nilihudhuria kwa Mtume ﷺ nika muona akimpatia moja ya sita.” Akamwambia: “Je, yupo pamoja na wewe yeyote?!” Akashuhudia Muhammad bin Muslimat mfano wa hilo, basi Abu Bakr رضي الله عنه akatekeleza hilo.³

³ Ameipokea hiyo Ahmad bin Hanbali katika *Musnad*, Juz. 4, uk. 225 na Ibn Jaaruud katika kitabu *al-Muttaqi* 959 na Abdul-Razzaq katika kitabu *Muswanaf*, Juz. 10, uk. 274 na Bayhaqi katika kitabu chake *Sunan*, Juz. 6, uk. 234 na Hakim katika Juz. 4, uk. 338, na akaisahihisha na kukiri Dhahabi juu ya uwepo wake, na Ibn Haban katika *Sahih* yake, na Malik katika kitabu *Muwatwai*, Juz. 2, uk. 513 na *Sunan Abu Daud*, Juz. 3, uk. 121 na *Tirmidhi*, Juz. 4, uk. 419, nayo ni sahihi.

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

Na hii ni mifano ya wazi kabisa inayofaidisha kwamba habari ya mtu mmoja haifaidishi elimu na yakini. Hivyo tunaweza kui-kataa na kuipinga hata kama sanad yake ni sahihi, pindi tunapokuta kuwa fikira yake inakwenda kinyume na misingi na fikira ambazo zimepatikana katika Qur’ani Tukufu au hadithi lukuki zilizothibiti, Na sisi hatutaki kurefusha zaidi katika utangulizi huu kutokana na ishara na vidokezo hivi, bali inatupasa kuangalia yale aliyoyaeleza Sheikh wetu Imam Allamah mwana hadithi Sharifu Sayyid Abdullah bin Swadiq katika kitabu hiki kilichojaa faida kemkemu, na mambo mengi ya kipekee, na tunamuomba Mwenyezi Mungu (s.w.t) taufiki, uwezeshwaji na mwongozo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Mwanzo wa kitabu “Faida zenye kukusudiwa” na utangulizi
wa ndugu yetu mwandishi**

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA HADITHI ZISIZOKUWA ZA KAWAIDA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.**

Sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu aliyetukuka, Msifiwa kwa sifa tukufu, na Msifiwa kwa sifa za ukamilifu, pia amepukana kuwa na umbo, sura na kufananishwa na mifano mbali mbali. Mwenyezi Mungu amepukana na kuwa katika sehemu fulani, au anapitwa na wakati, au anabadilika kwa mabadiliko ya tabianchi, na kubadilika hali moja hadi nyingine. Na rehema na amani zimfikie bwana wetu Muhammad na ndugu zake watukufu, pia radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya Masahaba wake na kizazi kilichokuja baada ya Masahaba.

Ama baada: Hakika kuitendea kazi hadithi ya Mtume ﷺ ni wajibu, na kumtii Mtume ﷺ ni jambo la lazima, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), anasema:

مَنْ يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ﷻ

**“Mwenye kumtii mtume ndio amemtii Mwenyezi Mungu...”
(an-Nisaa; 4:80), na kauli yake (s.w.t) anasema:**

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ

**“Sema: Ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuatani, Mwenyezi Mungu atawapenda na atawaghufiria madhambi yenu...”
(3:31).**

Na zipo hadithi lukuki zilizopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ zenye maana hii. Aidha ipo ijmai ya umma juu ya kuwajibika kumfuata yeye ﷺ kwa yale yaliyothibiti kutoka kwake pasi na kuweka mipaka wala sharti. Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا ۗ

“Na anachowapa Mtume kichukueni, na anachowakataza jiepusheni nacho.....” (al-Hashr; 59:7), pia (s.w.t) anasema:

ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

“Na kisha wasione dhiki katika nyoyo zao kwa uliyoyahukumu na wanyenyekee kabisa kabisa.” (an-Nisaa; 4:65).

Isipokuwa ni kwamba kuna kundi miongoni mwa walahidi, wamejifunga katika kuitendea kazi Qur’ani tu, na wakakanusha kuitendea kazi sunnah,⁴ na wakatoa sababu zisizo na mashiko, kwa mu-

⁴ Na hakuenda katika kuiacha Sunnah na kutoitendea kazi, yaani kundi miongoni mwa makundi ya Waislamu yenye kuheshimiwa kama vile Muutazila na Imamiyya na Zaydiyya na Ibaadhiyya na wengineo bali wote wameafikiana juu ya kuitendea kazi Sunna takatifu ya Mtume ﷺ, na vitabu vyao vya Fiqhi na vya Itikadi na vinginevyo ni ushahidi mzuri juu ya hilo, kama vile walivyoafikiana watu hawa pamoja na Ahlu Sunna wasio na fikira ya kwamba Mwenyezi Mungu ana kiwiliwili, kuwa haifai kujengea itikadi juu ya hadithi ya mpokezi mmoja, na bwana wetu mwandishi Ghumaari, Mwenyezi Mungu amnyanyue daraja lake kwa yote hayo! Na kitabu chake hiki ni ushahidi mzuri juu ya hilo.

jibu wa kauli yao: Hakika hadithi kuna madhaifu mengi na hadithi chungu tele zilizobuniwa, na zikaingizwa zile zenye fikra za Kiyahudi, na nyingine zinazofanana na hizo miongoni mwa hoja zinazojulikana ubatili wake kwa dharura. Hakika wanazuoni wa hadithi wamebainisha hadithi dhaifu na za uwongo katika vitabu makhsusi. Wakazitambua hadithi zenye fikra za kiyahudi, na wakawakosoa wapokezi wa hadithi ukosoaji wa wazi kwa kuweka kanuni, vidhibiti na vigezo ambavyo kutokana navyo hujulikana yule ambaye hukubaliwa hadithi yake na yule ambaye haikubaliwi hadithi yake. Na wakazungumza juu ya sababu za hadithi za dhahiri na zisizo za dhahiri, pamoja na ilhamu ya Mwenyezi Mungu aliyowapa, iliyowawezesha kuijua hadithi yenye kubuniwa na kuzushwa, ikiwa itakuwa sanad yake katika dhahiri ni sahihi. Akasema Rabi'u bin Khathim: "Hakika hadithi ina mwanga kama vile mwanga wa mchana unaoujua, na uongo una giza kama vile giza la usiku unalolichukia."⁵

Na amepokea Ahmad kutoka katika njia ya Rabi'at kutoka kwa Abdul-Malik bin Said bin Sweid kutoka kwa Abi Asid au Abi Hamid: Hakika Mtume ﷺ amesema: "Mtakapoisikia hadithi kutoka kwangu ambayo nyoyo zenu zinaijua na inalainisha hisia zenu na bishara zenu, na mnaona kwamba inafaa kutoka kwenu, basi mimi ni mbora zaidi kwayo kuliko ninyi. Na mtakapoisikia hadithi kutoka kwangu, ambayo zinaikataa nyoyo zenu, na zinachukia hisia zenu na bishara zenu, na mnaona kwamba hiyo haifai kutoka kwenu, basi mimi nipo mbali nayo zaidi kuliko nyinyi."⁶

Na hakika wametofautiana waislamu kama vile inavyojulikana juu ya baadhi ya hadithi baina ya kukubalika na kutokubalika, na hili halimaanishi kwamba wao wameacha Sunna au hakika wao hawakuzichukua hizo!!

⁵ Ameipokea Ibn Saad katika *Twabaqatul-Kubra*, Juz. 6, uk. 186 na Khatwiib katika *Kifaayat*, uk. 431.

⁶ Ameipokea Ibn Saad katika *Twabaqatul-Kubra*, Juz. 1 uk. 387 na Ahmad katika *Musnad* Juz. 3 uk. 497 na Juz. 5 uk. 425 na ibn Haban katika sahihi yake Juz. 1 uk. 264 na Al-Bazar katika kitabu *Kashful-Astaar* Juz. 1 uk. 105 na wengineo, na watu wake ni watu wa Bukhari na Muslim ila Abdul-Malik bin Saad kwani yeye ni miongoni mwa watu wa

Hafidh ibn Rajab amesema: Na sanad yake hakika imesemwa kwa sharti la Muslim, lakini hiyo ni yenye matatizo, kwani hiyo ameipokea Bakir bin Ashji kutoka kwa Abdul-Malik bin Said kutoka kwa Abbas bin Sahil kutoka kwa Ubay bin Kaab, amesema: “Yatakapowafikia kutoka kwa Nabii ﷺ yale yanayojulikana na kulinisha ngozi, basi hakika amesema Nabii ﷺ kheri, na wala hasemi ila kheri. Bukhari amesema: Na hili inashabihiana zaidi: Na amepokea Yahya bin Adam kutoka kwa Ibn Abu Dhiib kutoka kwa Saad Maqbari kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume ﷺ, amesema: ‘Mtakapohadithiwa hadithi kutoka kwangu ambayo mnaijua hiyo wala hamuichukii basi isadikisheni, kwani hakika mimi nasema yale yanayojulikana na yasiyochukiza. Na mtakaposimuliwa hadithi kutoka kwangu ambayo mnaichukia wala hamuijui basi msiisadikishe hiyo. Hakika mimi sisemi yanayochukiza wala yasiyojulikana.’”

Hafidh Ibn Rajab⁷ amesema: “Na hadithi hii ni yenye kasoro pia. Hakika wametofautiana katika sanad yake juu ya Ibn Abu Dhiib, na wameipokea mahafidhi kutoka kwake, kutoka kwa Said hali ya kuwa ni hadithi *mursali*. Na hadithi *mursali* ni sahihi zaidi kwa maimamu wa mahafidhi, miongoni mwao Ibn Muin, Bukhari, Abu Hatam Raazi na Ibn Khuzaima, na amesema: “Sijamuona yeyote miongoni mwa wanazuoni wa hadithi anayethibitisha uungaji wake. Na hakika mfano wa hadithi hizi hata tukikadiria kuwa ni sahihi, bado zitaishia kuonesha maarifa ya maimamu wa hadithi,

Muslim naye ni mkweli. Na akasema Hafidh Haythami katika *Majmaul-Zawaid*, Juz. 1, uk. 150: Amepokea Ahmad na Al-Bazar na watu wake ni watu wa sahihi, na hadithi ameisahihisha mpingaji wa zama katika *Sahih* yake Juz. 2 uk. 369 nambari 732, na Ahmad Shakir katika utoaji wake wa maelezo juu ya juzuu ambayo ameisambaza kutoka katika sahihi ya ibn Haban, kama vile ilivyokuja hilo katika utoaji wa maelezo ya Shuaib Arnaaut juu ya *Sahih* ya Ibn Haban Juz. 1, uk. 264, kimechapishwa na taasisi ya Risaalat, na *Sayr Aalaam Nubalaai* Juz. 7, uk. 238 na ameisahihisha pia Shuaib Arnaaut katika utoaji wake wa maelezo juu ya kitabu *Mushkilil-Athaar* Juz. 15 uk. 344.

⁷ Katika kitabu *Jaamiul-Uluum wal-Hukm* uk. 256 kimepigwa chapa na Daarul-Maarifa toleo la kwanza mwaka 508 AD. Beirut – Lebanon.

wakosoaji nguli ambao wamekithirisha kuchambua maneno ya Mtume ﷺ na maneno ya mwingine, kutazama hali za wapokezi wa hadithi, na wanukuzi wa habari mbalimbali, na kutaka kujua ukweli wao na uongo wao, na kutaka kuwadhhibiti na kuwahifadhi. Hakika watu hawa wana ukosoaji mahsusi katika hadithi wenye kubobea katika kuyajua hayo, kama vile mtazamaji mahiri anavyotambua sarafu nzuri na mbaya, zinazofaa na zisizofaa. Na ni kama mtaalamu wa vito anavyojua vito halisi na visivyokuwa halisi. Na kila mmoja miongoni mwa watu hawa huwezi kutolea maelezo sababu za maarifa yake, wala kuzitolea dalili. Na alama ya hilo ni kwamba huwekwa hadithi ya mtu mmoja mbele ya wanaojua elimu hii, na hatimaye huafikiana katika jibu pasi na kupingana. Na hakika wamewahi kutahiniwa baadhi miongoni mwao zaidi ya mara moja katika zama za Abi Zur'at na Abu Hatam, na jibu likakutwa ni hivyo, muulizaji akasema: Ninashuhudia hakika elimu hii ni ya ilhamu.”

Haya ni maneno ya Hafidh ibn Rajab. Angalia yaliyobakia katika ufafanuzi wa hadithi ya ishirini na saba kutoka katika kitabu *Jamiul-Uluum wal-Hukm*, ili ujue kiwango cha ijthadi ya wanahadithi katika kuzitakasa hadithi kutokana na uongo na uzushi wa mambo, pamoja na umakini wa utafiti wao katika ukosoaji wa wapokezi wa hadithi.⁸ Na hakika wametoa ushuhuda Mustashrikii-na kuhusu kanuni za ukosoaji ambazo wameziasisi wanahadithi kuwa hakuna mfano wake katika umma wa wasiokuwa Waislamu.⁹

⁸ Maneno haya ambayo ameyanukuu Sayyid, ‘Mwenyezi Mungu anyanyue daraja lake’ kutoka kwa ibn Rajab Hanbali kwa mtazamo wangu ni maneno ya insha yaliyopitiliza! Kwani ni mara ngapi Jamhuri ya mahafidhi wa kale na wale wa baada yao wamezingatia hadithi kuwa ni sahihi ilihali ni hadithi isiyo ya kawaida au batili yenye kurudishwa na kukataliwa, aidha katika sahihi mbili kuna mfano kuhusiana na hilo! Na kwa hivyo imehitajika watu mfano wa Daaruu Qutni na wengineo kupitia upya na kubainisha yale ambayo yapo ndani yake kutokana na mapungufu na kasoro!!

⁹ Maneno haya siafikiani nayo, elimu ya kujua kasoro na mapungufu ya wapokezi wa hadithi ina misimamo inayotokana na chuki za kimadhehebu na hususan katika njia ya watu

Na makusudio ni kwamba hakika kuitendea kazi hadithi sahihi iliyosalimika kutokana na kasoro na ugonjwa ni wajibu, lakini wengi miongoni mwa watu wa elimu wanadhani kwamba ikiwa hadithi ni sahihi basi ni wajibu kuitendea kazi moja kwa moja (bila kikwazo wala kipingamizi), na hili sio sahihi, bali ni sharti kwamba hadithi hiyo isiwe ni yenye kwenda kinyume na hadithi mutawatiri au kanuni zilizokubalika.

Kundi hili lifuatalo ni miongoni mwa hadithi zenye kwenda kinyume na hadithi mutawatiri au kanuni zilizokubalika. Pia tutatoa ubainifu wa muonekano wa kuwa kwake kinyume na hadithi mutawatiri au kanuni zilizokubalika. Na sijakusudia kuziorodhesha zote, na hakika nimetaja mifano tu ili iwe kielelezo tosha cha kutuongoza katika mlango huu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye mwezes haji.

HADITHI YA KWANZA

Kutoka kwa Muawiya bin Hakam Salami amesema: Nilikuwa na mifugo eneo la baina ya Ahadi na Jawaniyyat, na alikuwepo hapo kijakazi wangu, nikachunguza siku moja nikagundua mbwa mwitu amekwenda na mbuzi mmoja, basi ikanisikitisha na hivyo nikamuweka (kijakazi) kizuizini, nikaenda kwa Mtume ﷺ nikamtajia hilo. Akanijia na kuweka umuhimu mkubwa juu yangu, nikasema: Ewe Mtume! Je, nimwache huru? Akasema: “Mwache huru.” Basi nikamwita yeye, akamuuliza: Yuko wapi Mwenyezi Mungu? Akajibu: Mbinguni. Mtume akamuuliza: “Mimi ni nani?” Akajibu: Wewe ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akase-

wa ithibati, kutoka kwa wanahadithi ambao wameathirika na siasa ya Bani Umayya na Bani Abbasi kutokana na pande mbili za chuki binafsi na ushabihishaji! Na kitabu Al-Utbul-Jamiil ala Ahlil-Jarhi wa Ta’adiili cha Sayyid Muhammad bin Aqiil Baalawiy (r.a) na yale tuliyoyatolea maelezo juu yakeni mifano mingi kuhusiana na hilo!!

ma: “Mwache huru, hakika yeye ni muumini.”¹⁰ Ameipokea hiyo Muslim, Abu Daud, Nasai na wengineo.

Albani katika kitabu *Mukhtaswarul-Uluwi* amesema: [Katika habari hii kuna masuala mawili: Mojawapo ni uhalali wa Mwislamu kusema: ‘Yuko wapi Mwenyezi Mungu?’¹¹ Na la pili: Kauli ya muulizwaji: Yuko mbinguni. Hivyo basi yule mwenye kuyakanusha masuala haya mawili, kwa hakika amemkanusha Mtume Muhammad Mustafa ﷺ].¹² Imekwisha.

Na utoaji wa hukumu sio sahihi, kwa sababu hadithi hii si ya kawaida, hivyo haifai kuitendea kazi. Na kuna mambo kadhaa yanayoonesha kuwa si ya kawaida: Inatofautiana na tawaturi iliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ, kwani yeye alikuwa anapojiwa na mtu anay-

¹⁰ Hadithi hii ameipokea Malik 1511 na Muslim 537 na Nasaai 1218 na Abu Daud 930! Na ameipokea kwa lafudhi: “Ni nani mola wako mlezi?” kutokana na hadithi ya Shariid bin Sweid Thaqaifi: Nasaai 3653 na Ahmad Juz. 4 uk. 222 na ibn Haban katika sahihi yake Juz. 1 uk. 418 na wengineo! Na ameipokea kwa lafudhi: “Je, unashuhudia hapana mungu ila Mwenyezi Mungu” Abdul-Razzaq katika kitabu Muswanaf Juz. 9 uk. 175 na Malik katika kitabu Muwatwai 1512 na Daar Qutni 2358 na Ahmad Juz. 3 uk. 451 na Ibn Abi Shaiba Juz. 6 uk. 162. Na hadithi hizi zinapelekea mkorogo wa hadithi ila hakika sisi tumeipa uzito hadithi “Je, unashuhudia” kwani hiyo inaafikiana na hali nyingine za Mtume ﷺ na hadithi zilizokithiri zinazopatikana kutoka kwake ﷺ au ambazo inaweze-kana zimepokewa kutoka kwake, basi sisi tumekata shauri kwa kutohibiti hadithi “Yuko wapi Mwenyezi Mungu” na kumuepusha Mtume ﷺ kuwa ameyasema hayo. Na mimi ninayo Risala mahsusi kuhusu hadithi hii, nimebainisha ndani yake kutohibiti hadithi yenye lafudhi “Yuko wapi Mwenyezi Mungu” na hakika yeye ni mwenye kuepukana na kuwa mbinguni au juu ya Arshi, nimeita: *Tanqihul-Maf’humu al-Aaliyah Bimathabata Wamalamyathbutu Min Hadithil-Jariyyah*, nayo imechapishwa!!

¹¹ Bali hili sio sharia kwani halijathibiti kulingana na tathniya ya hadithi! Na hakika hiyo inajulisha juu ya sehemu na Mwenyezi Mungu ametukuka kuwa na sehemu makhususi, yeye ni muumbaji wa sehemu, na mbingu ni sehemu, nayo ni baadhi ya viumbe wake, na Mwenyezi Mungu ametakasika na kuepukana na kuwa mahali fulani au kuwa na mwili amekaa au ametulia juu ya Arshi, ametukuka Mwenyezi Mungu na hilo utukukaji mkubwa mno kabisa!

¹² Sisi tunakanusha masuala haya mawili na tunayazingatia ni miongoni mwa upotofu wa wazi katika itikadi, na hakika Mtume ﷺ hakuuliza kuhusu Mwenyezi Mungu kwa lafudhi ya “Yuko wapi?” wala hakusema kijakazi mbinguni!

etaka kuwa Mwislamu, alikuwa akimuomba atoe shahada mbili! Na akikubali kutoa shahada mbili anahukumu Uislamu wake.

Na katika kitabu *Muwatwai* kutoka kwa Abdullah bin Utbat bin Mas'ud imepokewa kwamba: Hakika mtu miongoni mwa Answar alikuja kwa Mtume ﷺ pamoja na kijakazi mweusi, basi akasema: “Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu ninaye mtumwa muumini, basi iwapo nawe unamuona ni muumini mwache huru.” Mtume ﷺ akasema kumuuliza yeye: “Je, unashuhudia hapana mungu anayepaswa kuabudiwa ila Allah” akasema: Ndio. Akamuuliza: “Je, unashuhudia hakika Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu?” Akajibu: Ndio. Akamuuliza: “Je, unakiri kuwa kuna ufufuo baada ya kufa?” Akajibu: Ndio, hapo Mtume ﷺ akasema: “Mwache huru.”¹³

Na hii ndio hali inayojulikana kutoka kwa Mtume ﷺ kwa dharura.

Ndiyo amepokea Hafidh Abu Ismail Harawi katika kitabu *Arbaina Fii Dalaail Tawhiid*, kutoka katika njia ya Sa'id bin Marziyan kutoka kwa Akramat, kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: Alikuwa mtu mmoja kwa Mtume ﷺ akiwa na kijakazi mweusi akasema: Mimi ninaye mtumwa je, inafaa huyu kuondoka kwangu? Mtume akamuuliza: “Yuko wapi Mwenyezi Mungu?” basi (kijakazi) akashiria mkono wake mbinguni, akamuuliza: “Mimi ni nani?” Akajibu (kijakazi): Wewe ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akasema ﷺ: “Mwache huru, hakika huyu ni muumini.” Na hii pia ni hadithi isiyo ya kawaida na ni dhaifu, ndani yake yumo Sa'id bin Marziyan, naye ni mwenye kuachwa, hadithi zake hazichukuliwi, ni mchakachuaji.¹⁴

Na zimekuja hadithi mbili zenye kutofautiana na hadithi ya Muawiya, ambazo zinatilia mkazo kuwa ni hadithi isiyo ya kawaida.

¹³ Ameipokea Malik katika kitabu chake *Muwatwai*, 1512 na wengineo, na hakika limetanguulia hilo hapo kabla! Nayo ni hadithi sahihi.

¹⁴ Angalia wasifu wake katika kitabu *Tahdhiibul-Kamaal*, Juz. 11 uk. 52.

Amepokea Bayhaqi katika *Sunan* yake ¹⁵ kutokana na njia ya Aun bin Abdillah bin Utbat: Amenihadithia baba yangu kutoka kwa babu yangu, amesema: Alikuwa mwanamke mmoja kwa Mtume ﷺ pamoja na kijakazi mweusi, akasema: Ewe Mtume! Hakika mimi nina mtumwa muumini je, inafaa kumwacha huyu huru? Akamuuliza: “Ipi dini yako?” Akajibu: Uislamu. Akamuuliza: “Mimi ni nani?” Akajibu: Wewe ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akamuuliza: Je, unaswali swala tano na unaliunganisha ulilokuja nalo mbele ya Mwenyezi Mungu? Akajibu: Ndio, Basi Bwana Mtume ﷺ akampiga mgongoni kwake, akasema: “Mwache huru.”

Pia imepokewa kutoka katika njia ya Hamad bin Salama kutoka kwa Muhammad bin Amru, kutoka kwa Abi Salama, kutoka kwa Sharid bin Thaqafi, amesema: Nilisema: “Ewe Mtume hakika mama yangu aliniusia nimwache huru mtumwa huyu, na mimi nina kijakazi Mnubi.” Mtume ﷺ akasema: “Mwite huyo.” Akamuuliza: “Ni nani Mola Wako?” Akajibu: “Mwenyezi Mungu.” Akamuuliza: “Mimi ni nani?” Akajibu: “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.” Akasema: “Mwache huru, hakika huyo ni muumini.”

Na imekuja hadithi ya tatu. Ahmad katika *Musnad* yake Juz. 3, uk. 451 amesema: “Alitueleza sisi Abdul-Razzaq: Alitusimulia sisi Muammar, kutoka kwa Zuhari, kutoka kwa Abdullah bin Abdillah, kutoka kwa mtu mmoja miongoni mwa Manswari: Hakika yeye alikuja pamoja na kijakazi mweusi akasema: ‘Ewe Mtume! Hakika mimi nina mtumwa muumini, iwapo nawe utamuona huyu ni muumini nitamwacha huru.’ Mtume ﷺ akasema kumwambia yeye: ‘Je, unashuhudia kwamba hakika hakuna mungu muabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu Mmoja?’ Akasema: ‘Ndio.’ Akamuuliza: ‘Je, unashuhudia kwamba hakika mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi

¹⁵ *Sunanul-Kubra*, Juz. 7 uk. 388 cha Bayhaqiy na sheikh wake Hakim katika kitabu chake *Mustadrak*, Juz. 3 uk. 289, nayo ni hadithi nzuri na sahihi.

Mungu?’ Akajibu: Ndio. Akamuuliza: ‘Je, unaamini ufufuo baada ya kufa?’ Akajibu: ‘Ndio.’ Akasema: ‘Mwache huru.’¹⁶ Na hadithi hii ni yenye kuunganishwa na *mursali* ya *Muwatwai*.

Bazar amesema: Ametuhadithia Muhammad bin Uthman: Ametusimulia sisi Abdullah: Ametuelezea sisi Ibn Abi Layla, kutoka kwa Al-Munhaal ibn Amru, kutoka kwa Sa’id bin Jubair kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: “Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume ﷺ akasema: Hakika mimi nina mtumwa, kijakazi mweusi. Mtume ﷺ akasema: ‘Hebu niletee hapa.’ Akamwambia: ‘Je, unashuhudia kwamba hakika hakuna mungu anayepaswa kuabudiwa ila Allah na mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu?’ Akajibu: Ndio, akasema: ‘Mwache huru.’”¹⁷

Hakika Mtume ﷺ amebainisha nguzo za imani, katika hadithi ya swali alilomuuliza Jibrail, aliposema: “Imani ni kumwamini Mwenyezi Mungu, Malaika Wake, vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho na kuamini makadara¹⁸ kheri yake na shari yake.” Na haikutajwa ndani yake itikadi ya kwamba Mwenyezi Mungu yuko mbinguni. Hakika itikadi iliyotajwa haithibitishi tawhid wala haikanushi shirki, basi iweje Mtume ﷺ amsifu mwenye nayo kuwa ni muumini? Walikuwa washirikina wakiitakidi kwamba hakika Mwenyezi Mungu yuko mbinguni, na wakimshirikisha pamoja naye miongu mingine ardhini. Na alipokuja Haswiin bin Utba au Ibn Abiid mzazi wa Imran kwa Mtume ﷺ, Mtume alimuuliza yeye: “Mara

¹⁶ Ameipokea hiyo Ibn Jarud katika kitabu chake Al-Muntaqii 234 na akasema Hafidh Al-Haythami katika kitabu chake Majmaul-Zawaid Juz. 1 uk. 23: Ameipokea Ahmad na hakika watu wake ni watu sahihi.

¹⁷ Ameipokea Ibn Abi Shaiba Juz. 6 uk. 162 na Twabarani katika kitabu chake Awsat Juz. 5 uk. 350, na Ibn Abi Layla ndani yake kuna udhaifu.

¹⁸ Imani ya makadara imepatikana katika hadithi ya bwana wetu Jibrail عليه السلام katika kitabu Sahihi Muslim (8) kutoka katika hadithi ya Umar bin Khatwab, na ama Bukhari hakika ameipokea katika Sahihi yake (50) na (4777) kutoka hadithi ya Abu Huraira hakuna humo utajo wa makadara.

ngapi unaabudu mungu?” Akajibu: “Mara sita ardhini, na mara moja mbinguni.”¹⁹ Na akasema Firaun kumwambia Haman:

فَجَعَلْ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَطَّلِعُ إِلَى إِلِهِ مُوسَىٰ

“....Unijengee mnara nipate kumchungulia Mungu wa Musa....”
(al-Qasas; 28:38), kwa itikadi yake kwamba Mwenyezi Mungu yuko mbinguni, pamoja na hivyo akasema kuwaambia watu wake:

فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ

“Akasema: Mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu.” (an-Nazia’t; 79:24),
na akawaambia wao:

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرِي

“Na akasema Firauni: Enyi waheshimiwa! Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi....” (28:38). Na linalojulikana ni kwamba Mwenyezi Mungu kuwa mbinguni si kwa maana ya uhakika wake, hiyo ni kwa mujibu wa ijmai ya wanazuoni, bali hilo limeawiliwa kwa maana ya hali ya juu ya kimaana.

Baaji amesema kuhusu kauli ya kijakazi: “Yuko mbinguni,” huenda yeye anataka kumsifu Yeye kwa sifa ya juu zaidi, na kwa hilo husifiwa yule ambaye shani yake iko juu kabisa, husemwa: Sehemu ya fulani ni mbinguni, yaani hali yake ni ya juu na imenyanyuka shani yake. Na ametaja Sabku katika kitabu *Twabaqaatul-Shafiyyat*, Juz. 1, uk. 265, beti zilizonasibishwa kwa Abdullah bin Rawahat:²⁰

¹⁹ Ameipokea Tirmidhiy (3483) na akasema: Ni nzuri na ngeni, hadithi haijathibiti. Na hakika nimeieleza hiyo katika utoaji maelezo juu ya kitabu ‘Uluwu’ andiko 29 cha Dhahabi.

²⁰ Hazithibiti beti hizi kutoka kwa Abdullah bin Rawaha (r.a)! Na sanad yake imekatika kama vile alivyokiri hilo Dhahabi katika kitabu *Al-Uluwu* katika andiko nambari 64, angalia huko katika utoaji wa maelezo yetu juu ya hilo.

“Nimeshuhudia hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ya adhabu ni haki – na hakika moto ni mafikio ya makafiri.

Na hakika Arshi ni yenye kuelea juu ya maji, na juu ya Arshi yuko Mola Mlezi wa ulimwengu wetu.

Na baada yake akasema: “Uzuri uliyoje wa kauli ya Imam Raafii katika kitabu chake *Aamali*, na hakika ametaja beti hizi: Ujuu huu ni ujuu wa adhimu na wenye kujitosheleza, na katika mukabala wa sifa ya wasifaji kwa sifa za wenye kushindwa na kuisha.” Imekwisha. Na nguzo za imani, haziingiliwi na taawili.

HADITHI YA PILI

Vile vile amepokea Muslim kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: “Nilimuomba idhini Mola Wangu Mlezi nimuombe mama yangu, na hakunipa idhini, na nikamuomba idhini ya kuzuru kaburi lake basi akanipa idhini.”²¹ Na hadithi hii pia si ya kawaida, kwa kukhtilafiana kwake na Aya za Qur’ani Tukufu, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا

“Wala sisi hatuadhibu mpaka tupeleke Mtume.....”
(Bani Israil; 17:15). Vile vile Mola Manani (s.w.t) anasema:

ذَٰلِكَ أَن لَّمْ يَكُن رَّبُّكَ مُهْلِكَ الْفَرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلَهَا غَافِلُونَ

“Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola Wako hakuwa ni mwenye kuingamiza miji kwa dhulma na hali wenyewe wameghafilika.”
(al-Anam; 6:131), yaani hawakujiwa na muonyaji, na kuhusiana na Waarabu anasema (s.w.t):

²¹ Amepokea *Muslim* (976) wala haijathibiti! Katika sanad yake yupo Yazid bin Kaysaan, akasema Yahya Qatwan: Yeye sio kati ya wale wenye kutegemewa, yeye ni mtu mwema wa kati.”

وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ

“Wala hatukuwatumia muonyaji kabla yako.” (34:44). Hali kadhalika amesema:

لَتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَاهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ

“Ili uwaonye watu wasiofikiwa na muonyaji kabla yako, huenda wakaongoka.” (as-Sajdah; 32:3), na mama wa Mtume ﷺ aliishi katika kipindi fulani cha zama za ujinga, hawakujiwa na muonyaji, na hakujua hilo. Basi kwa mujibu wa Aya hizi zimekanusha wazi wazi adhabu juu yake, na hadithi iliyotajwa inayozuia kumombea msamaha ni hadithi isiyo ya kawaida haitendewi kazi. Na habari ya mtu mmoja haitangulizwi juu ya Qur’ani Tukufu, na hili lipo wazi kabisa wala halina kificho.

Na mfano wake ni ile aliyopokea Ahmad katika *Musnad* kwa sanad yake dhaifu kutoka kwa Abu Razin Aqiili, akasema: “Nikamuuliza: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, yuko wapi mama yangu? Akasema: “Mama yako yuko motoni.” Nikamuuliza: Basi wapi wanakwenda miongoni mwa watu wako wa karibu? Akasema: “Je, huridhii mama yako kuwa pamoja na mama yangu?”²² Basi hadithi hii pamoja na udhaifu wake pia si ya kawaida.

HADITHI YA TATU

Vilevile amepokea Muslim kutoka katika njia ya Hamad bin Salama kutoka kwa Thabit kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Hakika mtu mmoja alisema: “Ewe Mtume, baba yangu atakuwa wapi?”

²² Ameipokea *Ahmad* Juz. 4 uk. 11 na Twabarani katika *al-Kabiir* Juz. 19, uk. 208, na katika sanad yake yupo Wakii bin Udus au (Hudus) asiyejulikana hali kama alivyosema Ibn Qatwan Al-Faasi na hakumkubali ukweli wake ila Ibn Haban, naye ni mhusika wa hadithi potofu yenye kuchukiza katika kitabu cha *Tirmidhi* 3109, na akaiona ni nzuri.

Akasema ﷺ: “Motoni.” Yule mwanaume alipoacha kumuombea yeye dua, Mtume akasema: “Hakika baba yangu na baba yako watakuwa motoni.”²³

Nasema: Hadithi hii kwa lafudhi hii si ya kawaida, ni yenye kukataliwa kwa mujibu wa yale ambayo ubainifu wake umeshatangulia huko nyuma. Abdul-Adhiim Abadi katika kitabu *Awnul-Maabud*²⁴ ameizungumzia hadithi hii, amenukuu huko maneno ya Nawawi kuhusiana na yule anayekufa katika kipindi ambacho walikuwa Waarabu wakiabudu masanamu kwamba yeye atakuwa miongoni mwa watu wa motoni. Na kufanya hivyo si kumwadhibu mtu kabla ya kufikiwa na ulinganio, kwani hakika watu hawa uliwafikia ulinganio wa Nabii Ibrahim عليه السلام na Mitume wengineo, kisha mwandishi akasema:

[Na kila hadithi iliyopokewa kuhusiana na kuwa hai wazazi wa Bwana Mtume ﷺ na imani yao na kuokoka kwao, hadithi ambazo zimepokewa katika maudhui zaidi ya moja, ni uwongo na uzushi, na baadhi yake ni dhaifu mno, hazisihi kwa hali yoyote ile kwa mujibu wa maafikiano ya maimamu wa hadithi. Na kwamba ni dhaifu na za uwongo, wamesema hayo Daar Qutni, Jauzuqani, Ibn Asakir, Ibn Nasir, Ibn Jawzi, Suhaili, Qurtubi, Muhibu Tabari na Fat’hudin Ibn Sayyid Naas, Ibrahim Halabi na wengineo. Na hakika amezungumza kwa kirefu kuhusiana na kutookoka kwa wazazi wawili, Allamah Ibrahim Halabi katika Risala yenye kujitegemea, na Allamah Ali Qaari katika kitabu *Sharhul-Fiqhil-Akbar* na katika Risala yenye kujitegemea, na hadithi hii sahihi²⁵ ni ushahidi juu ya mwelekeo huu.

²³ Ameipokea Muslim 203 na Abu Daud 4718, nayo inatokana na hadithi ya Hamad bin Salama naye ni dhaifu mwenye fikira ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili, kila alilolipokea yeye miongoni mwa yale ambayo ndani yake yanaeleza kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili au kutilia mkazo madhehebu ya wale wenye chuki na Sayyidina Ali kwani hiyo ni kati ya hadithi ambazo zilizoanguka zenye kukataliwa.

²⁴ Angalia kitabu Uyuunul-Ma’abuud Juz. 12 uk. 324.

²⁵ Bali hadithi ni batili yenye kukataliwa yenye kuikhtilafiana na Qur’ani tukufu!

Na Sheikh Jalalud-Diin Suyutwi ametofautiana na mahifadhi na wanazuoni wahakiki na akathibitisha kwao hao wawili imani na kuokoka. Hivyo akatunga Risala kadhaa kuhusiana na hilo. Naye ni mtu wa kawaida mno, maneno yake hayazingatiwi katika mlango huu, maadamu hawakuafikiana naye maimamu wakosoaji, na Sandiy amesema: “Yule anayeamini uokovu wa wazazi wawili wa Mtume ﷺ analibeba hilo kwa hoja ya ami, hakika jina ‘baba,’ li-natumika hata kwa ami, na kwa kuwa Abu Twalib kwa hakika al-imlea Bwana Mtume ﷺ anastahiki kupewa jina la ‘baba’ kutokana na mtazamo huo.” Na vile vile maneno haya ni dhaifu na batili, na hakika mwandishi wa kitabu *Tafsiru Ruhul-Bayan* ameijaza tafsiri yake hadithi hizi zilizobuniwa na za uongo, kama ilivyo desturi yake katika mahali pa tafsiri yake kuleta hadithi za uwongo. Hivyo basi tafsiri yake ikawa ni hazina ya hadithi za uwongo, na wamesema baadhi ya wanazuoni: Kusimama mlangoni ni salama zaidi na ndio maneno mazuri]. Yameisha maneno ya mwandishi wa kitabu *Aunul-Maabud*.

Majibu:

1. Kauli ya Nawawi kwamba hakika watu wa zama za ujinga miongoni mwa Waarabu uliwafikia ulinganio wa Nabii Ibrahim عليه السلام na Mitume wengine, yanakinzana na maana ya kipindi hicho, kwani makusudio ya zama za ujinga kwa istilahi ya Uislamu ni zama ambazo utume haukuwafikia watu wake wala hawakujua dini miongoni mwa dini za Allah. Sasa vipi watu wa zama hizo wawe wamefikiwa na ulinganio wa Nabii Ibrahim عليه السلام, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuhusiana na Waarabu anasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ

“Wala hatukuwatumia muonyaji kabla yako.” (34:44), vile vile anasema:

لِنُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَاهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِنْ قَبْلِكَ

“Ili uwaonye watu wasiofikiwa na muonyaji kabla yako.” (28:46).

2. Hadithi za kuwa hai wazazi wawili wa Mtume ﷺ na imani yao ni hadithi zenye kubuniwa, haifai kuzitegemea. Na hakika katika hilo tunategemea juu ya maneno ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Na hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا

“Wala sisi hatuadhibu mpaka tupeleke Mtume.....” (Bani Israil; 17:15), na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

ذَلِكَ أَنْ لَمْ يَكُنْ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْفَرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلُهَا غَافِلُونَ

- “Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola Wako hakuwa ni mwenye kuingamiza miji kwa dhulma na hali wenyewe wameghafilika.” (al-Anam; 6:131). Na anasema kuhusiana na haki ya Waarabu – nao ni watu wa Makka na vitongoji vyake:**

وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ

“Wala hatukuwatumia muonyaji kabla yako.” (34:44), basi Aya hizi na nyinginezo miongoni mwa zile zilizopo katika maana yake nayo ndizo tunazozitegemea katika uokovu wa watu wa zama zaujahilia, na miongoni mwao ni wazazi wawili wa Mtume ﷺ.

3. Ali Qaari na Ibrahim Halabi kutegemea hadithi hii katika kauli zao za kwamba hakika wazazi wawili wa Mtume ﷺ ni watu

wa motoni ni kurahisisha mambo, na ni kughafilika kukubwa dhidi ya yale ambayo yamekubalika katika elimu ya Misingi ya Sharia,²⁶ na hakusema yeyote miongoni mwa wanazuoni kwamba habari ya mtu mmoja inatangulizwa juu ya Qur'ani, na Halabi na Qaari na wapambe wao hao, wamekwenda kinyume na maimamu na wanazuoni, kwa kuitegemea habari ya mtu mmoja na wakaiacha Qur'ani tukufu.

4. Hafidh Suyutwi ni mtu mpuuzaji wa haki, lakini yeye katika mlango huu ameshikamana na haki yenye kuungwa mkono na dalili lukuki. Na yatosha Qur'ani kuwa ni dalili tosha kwa kauli yake. Ama mwandishi wa Tafsiri iitwayo *Ruhul-Bayan* sio miongoni mwa watu wa hadithi! Kwa hivyo anataja hadithi zilizobuniwa ndani ya tafsiri yake. Ni kama vile Zamakhshari, Baydhawi, Abu Sau'd na wengineo.
5. Amebainisha rafiki yetu Allamah Sheikh Zahid Kawthari kwamba hakika Ali Qaari katika kauli yake ya kutookoka wazazi wawili wa Mtume ﷺ aliitegemea juu ya ibara iliyopatikana katika *Fiqhul-Akbar* cha Abu Hanifa inayoonesha hivyo, kwa kweli amekosea, kwa sababu katika nakala nyingine za kitabu *Fiqhul-Akbar* alichokitegemea kuna tamko bayana na la wazi la Abu Hanifa akithibitisha uokovu wa wazazi wawili.

Na ufupisho ni kwamba hadithi husika si ya kawaida, ni yenye kukataliwa kama ilivyotangulia. Lakini imepatikana kutokana na njia nyingine ikiwa haina tamko lisilo la kawaida. Amepokea Bazar, Twabari na Bayhaqi kutoka katika njia ya Ibrahim bin Saad, kutoka kwa Zahri kutoka kwa Amiri bin Saad bin Abi Waqas, kutoka kwa

²⁶ Lau angelikuwa mwandishi wa kitabu cha Aunul-Ma'abud amesoma elimu ya Misingi ya Sharia au kuifahamu asingeliitegemea hadithi ya mtu mmoja yenye kupingana na Qur'ani tukufu na yale ambayo yamethibitika ndani ya kitabu cha Mwe-nyezi Mungu (s.w.t)!!

baba yake, kwamba hakika bedui mmoja alimuuliza Mtume ﷺ: “Yuko wapi baba yangu?” Akasema: “Motoni.” Akamuuliza: “Yuko wapi baba yako?” Akasema: “Kila upitapo kwenye kaburi la kafiri mbashirie moto.”²⁷ Sanad yake ni kwa sharti la masheikh wawili, nayo ni sahihi zaidi kutokana na hadithi za Muslim, na ndani yake hakuna ibara kwamba wazazi wawili wa bwana Mtume ﷺ wako motoni, na hadithi ndiyo yenye kutegemewa.

6. Kuchukua maneno ya aliyechagua kusimama katika mlango huu ni kosa, kwani kusimama hakika kunapatikana pale dalili zinapolingana na kutoshana nguvu. Na hapa dalili hazijalingana wala kutoshana nguvu, kwani Qur’ani ni yenye kukata shauri juu ya kuokoka kwa watu wa zama za ujinga, na miongoni mwao ni wazazi wawili wa Mtume ﷺ.

Tanbihi: Usimamaji wa Hafidh Sakhawi katika suala la kuokoka kwa wazazi wawili wa Mtume ﷺ na kuchagua kunyamaza na kutokubainisha kama wako katika uokovu au la, kwao, kwa kutegemea juu ya hadithi hizi mbili zisizo za kawaida, ni jambo la kushangaza kutoka kwake, kwani kusimama kunapatikana pale dalili zinapotoshana nguvu, na hapa haipatikani hali ya kutoshana nguvu baina ya dalili, kwani Qur’ani tukufu inakata shauri juu ya kuokoka kwao. Na habari ya mtu mmoja haiwi na nguvu ya kupingana na Qur’ani tukufu. Na jambo la kushangaza zaidi kuhusu hilo ni msimamo wa Ali Qaari, kwani aliandika Risala elfu moja akipitisha na kuhukumu kuwa wazazi wa Mtume ﷺ wako motoni, na akaacha Qur’ani tukufu yenye kukata shauri kuwa hawako motoni, akategemea hadithi mbili zisizokuwa za kawaida, na ninadhani hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) atamwadhivu juu ya hilo.

²⁷ Ameipokea Muammar bin Rashid katika *Al-Jaamiu*, Juz. 10 uk. 454, Ibn Majah 1573, Bazar Juz. 3 uk. 299, *al-Kabiir* Juz. 1, uk. 145 cha Twabarani, Baydhawi katika *Al-Mukhtara* Juz. 3, uk. 204 na wengineo.

HADITHI YA NNE

Amepokea Imam Ahmad bin Hanbali katika kitabu chake *Musnad* na Bayhaqi katika kitabu chake *Itikad* kutoka kwa As'wad bin Sariu na Abu Huraira: Hakika Mtume ﷺ amesema: “Watu wanne watatoa hoja Siku ya Kiyama; kiziwi asiyesikia chochote, mpumbavu, kikongwe, na mtu aliyekufa katika zama za ujinga. Ama kiziwi atasema: Ewe Mola Wangu Mlezi, hakika ulikuja Uislamu na mimi sikuwa nasikia chochote. Na ama mpumbavu, atasema: Hakika ulikuja Uislamu wakati watoto wakinitupia mimi kinyesi cha mnyama. Na ama kikongwe, atasema: Ewe Mola Wangu hakika Uislamu ulikuja wakati mimi sielewi chochote. Na ama yule aliyekufa katika zama za ujinga, atasema: ‘Ewe Mola Wangu, hakunijia mimi mjumbe Wako.’ hapo atachukua miadi yao ili wamtii yeye. Basi utatumwa kwao ujumbe: Hakika waingizeni motoni, basi atakayeuingia utakuwa wa baridi na salama kwake, na asiyeuvingia atakokotwa hadi motoni.”²⁸

Na hadithi hii hata kama Bayhaqi ameizingatia kuwa ni sahihi katika kitabu *Itikad*, na kwa njia chungu tele, na hata kama ameisalimisha Hafidh pale aliposema: “Dhana juu ya wazazi wote wa Mtume ﷺ ni kwamba watatii mbele ya mtihani, ili litulie jicho lake ﷺ kwao’²⁹ bado ni hadithi isiyo ya kawaida, ni yenye kupondwa katika usahihi wake.

Ibn Abdul-Barri katika kitabu *Tamhid*³⁰ amesema kuhusu hadithi hii na zile zilizokuja katika maana yake: “Hadithi hizi sio miongoni

²⁸ Ameipokea Ahmad bin Hanbali Juz. 4, uk. 24, Ibn Haban katika *Sahih* yake Juz. 16 uk. 356 na Bayhaqiy katika *Itikad* uk. 169 na hadithi si ya kawaida kimatini, na sio sahihi, na katika sanad yake yupo Maadh bin Hisham na ndani yake kuna maneno yanayohitajika kuchunguzwa.

²⁹ Na hadithi ameipokea kutoka kwake Hafidh Suyutwi katika Barua yake “Masaalikul-Hunafaa fii Waalidayil-Mustwafa.

³⁰ *Tamhiid* Juz. 18 uk. 130.

mwa hadithi za maimamu, na hakika hadithi hizi ni za masheikh. Amesema Aqil bin Abu Twalib: Na linalojulisha juu ya udhaifu wake ni kwamba hakika Akhera sio nyumba ya ukalifisho, kwani linalotakiwa ni imani kwa mambo ya ghaibu, na akhera ni nyumba ya kushuhudia kwa macho, na kwa hivyo haimfai mtu toba anayotubia wakati wa kutolewa roho, wala wakati wa kuchomoza jua kutoka Magharibi, kwani hiyo ni saa ya kushuhudia uhalisia kwa macho. Na ikiwa haitomnufaisha yeye duniani, izeje imnufaishe huko Akhera?” Imekwisha.

HADITHI YA TANO

Ampokea Ahmad na Tirmidhi na wengineo kutoka kwa Ibn Abbas K kuhusiana na kauli ya Mwenyezi Mungu isemeyo:

حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ آمَنْتُ

“.....mpaka kulipomfikia kufa maji, akasema: Naamini.....” (10:90), amesema: Mtume ﷺ alisema: “Jibril aliniambia: Natamani ungeliniona mimi wakati nilipochukua udongo wa bahari na kum-sokomeza nao kinywani nikihofia asije kupata rehema.”³¹

Tirmidhi ameiona kuwa ni sahihi, lakini ni hadithi isiyo ya kawaida, kwani Jibril عليه السلام ni yule ambaye aliteremka kwa mama wa Musa na kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t):

أَنْ أَذْفَبِيهِ فِي التَّابُوتِ فَأَذْفَبِيهِ فِي الْيَمِّ فَلْيَلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ يَأْخُذُهُ عَدُوٌّ
لِي وَعَدُوٌّ لَهُ ج

³¹ Ameipokea Ahmad bin Hanbali Juz. 1, uk. 309 na Tirmidhi 3107 na akasema hiyo ni nzuri na hilo ni kosa sana!! Kwani katika sanad yake wapo watu wawili miongoni mwa wadhaifu mashuhuri nao ni Ali bin Zayd bin Juduan na Yusuf bin Mahran, na ameitaja hiyo Dhahabi katika *Al-Mizaan* katika wasifu Yusuf bin Mihran kwa kuashiria kuwa hiyo ni kati ya yale yake yenye kuchukiza!

“Kwamba mtie katika kisansuku, kisha kitupe mtoni, na mto utamfikisha ufukweni. Atamchukua adui Yangu na adui yake....” (Twha; 20:39). Na hii ni habari kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba Firauni ni adui wa Mwenyezi Mungu na wa Mtume Wake Musa ﷺ, na habari ya Mwenyezi Mungu haiachwi. Iweje Jibril ﷺ aseme: Nilikuwa nasokomeza udongo mdomoni mwa Firauni kwa kuhofia ili asifikiwe na rehema?

Kwa sababu akipata rehema hatokuwa adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na muda huo habari ya Mwenyezi Mungu itakuwa imekwenda kinyume, na hili ni muhali, na hadithi si ya kawaida, ni yenye kukataliwa.

HADITHI YA SITA

Amepokea Bayhaqi katika kitabu chake *Asmau wa Sifaat* kutoka katika njia ya Atwai bin Saaib kutoka kwa Abu Dhuha, kutoka kwa Ibn Abbas, amesema kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ

“Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba na katika ardhi mfano wa hizo.” (at-Talaq; 65:12), akasema: “Ardhi saba, katika kila ardhi yupo Nabii kama vile Nabii wenu, na Adam mfano wa Adam, na Nuhu mfano wa Nuhu, na Ibrahim mfano wa Ibrahim, na Isa mfano wa Isa.”³² Bayhaqi amesema: “Sanadi hii kutoka kwa Ibn Abbas ni sahihi, nayo si ya kawaida kama ilivyo-tangulia. Sijui ufuatiliaji wowote juu ya Abu Dhuha, na Mwenyezi

³² Ameipokea Hakim Katika *al-Mustadrak* Juz. 2, uk. 493, na Bayhaqi katika kitabu *Al-Asmau wa Sifaat*, uk. 390 mwisho wa mlango wa (kuanza uumbaji). Na hakika amenukuu Suyuutwi maneno ya Bayhaqi katika *Tadriibul-Raawi* Juz. 1, uk. 233 na akasema: “Na bado ninaendelea kushangaa kutokana na Hakim kuizingatia kuwa ni sahihi, hadi nikamuona Bayhaqi amesema: Sanad yake ni sahihi lakini si ya kawaida.

Mungu ni Mjuzi zaidi. Imekwisha.

Nayo ni kama alivyosema, hakika haiingii akilini kupatikane Adam wawili, Nuhu wawili na Ibrahim wawili n.k. Wala hakuna dalili inayojulisha hilo kutoka katika akili wala andiko. Na baadhi yao wameiletea maana nyingine hadithi hii, kwamba inapatikana katika kila ardhi mfano wa Adam, Ibrahim n.k.

HADITHI YA SABA

Ampokea Imam Ahmad bin Hanbali katika kitabu chake *Musnad*, Juz. 6, uk. 269 kutoka kwa Aisha رضي الله عنها, amesema: Hakika imeteremshwa Aya ya rehema na kuwanyonyesha watu wazima mara kumi. Ilikuwa katika karatasi chini ya kitanda nyumbani kwangu, na pindi alipougua Mtume صلى الله عليه وسلم tulishughulishwa na jambo lake, na akaingia mbuzi kwetu akaitafuna.³³

Athari hii si ya kawaida, ni yenye kukataliwa, na ni isiyojulikana kabisa, kwa sababu ufutaji wa usomaji ni muhali, kama nilivyobainisha hilo katika juzuu ya *Dhaukul-Tilaawat fii Bayaan imtinaai Naskhul-Tilaawat*.

Kisha ni miongoni mwa lisilokubalika ambalo haliingii akilini, la mbuzi kuingia ndani ya nyumba na kula karatasi yenye maandiko ya Qur'ani. Wala hajui hilo yeyote, na hili ni batili lenye kukataliwa kwa kukata shauri. Na lau tutaruhusu uwezekano wa mbuzi kula karatasi yenye maandiko ya Qur'ani yaliyofutwa, kama asemavyo mwenye rai ya kwamba ufutaji wa maandiko unawezekana, basi

³³ Na sanad yake ni sahihi, na asili yake ipo katika kitabu *Sahih Muslim* 1452 kwa lafudhi ya: "Ilikuwa kati ya yale yaliyoteremshwa miongoni mwa Qur'ani tukufu ni Aya 'Unyonyeshaji mara kumi wenye kujulikana unaharamisha' kisha ikafutwa kwa mambo matano yenye kujulikana, hadi anafariki Mtume صلى الله عليه وسلم. Aya hizo zilikuwa katika zile tunazozisoma kutokana na Qur'ani tukufu." Na anataja kuwa mbuzi ndiye aliyezetafuna. Na ameipokea Ibn Majah 1944 na Abu Ya'ali Juz. 8, uk. 64. na Daarul Qutni Juz. 4, uk. 179 na Twabarani katika kitabu *Al-Muujamul-Al-Awsat* Juz. 8, uk. 12.

itawezekana pia kula karatasi yenye maandiko ya Qur’ani ambayo hayakufutwa, na hapo ukweli wa Qur’ani utaondoka, kwani itakuwa inawezekana kuna maandiko yaliliwa, ilihali Mwenyezi Mungu swt. anasema:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ

“Hakika sisi tumeuteremsha Ukumbusho huu, na hakika sisi ndio tuulindao.”³⁴ (al-Hijr; 15:9).

HADITHI YA NANE

Amepokea Ahmad bin Hanbali na Ibn Haban na Twahawi kutoka kwa Asmaa bint Umais, amesema: “Aliingia kwangu Mtume ﷺ siku alipouwawa Ja’far, akasema: “Mvalishe vipande vitatu kisha fanya upendayo.”³⁵

Asmau alikuwa mke wa Ja’far bin Abu Twalib عليه السلام na mumewe alikuwa amekufa shahidi katika vita vya Muuta. Akasema Mtume ﷺ: “Vaa kaniki kwa uzito wa kitabu.” Nayo ni nguo huivaa mwanamke wakati wa eda.

³⁴ Hakika amezungumza juu ya hadithi hii Ibn Qutaiba katika kitabu *Taarwilu Mukhtalafil-Hadiith* uk. 310 kimepigwa chapa na Daarul-Jabal, Lebanon 1972 AD.

³⁵ Amapokea Ahmad bin Hanbali Juz. 6, uk. 369 na 438; na Ibn Haban Juz. 7, uk. 418 na Bayhaqi, Juz. 7, uk. 438, na Twahawi katika kitabu *Sharhu Maanil-Athaar* Juz. 3, uk. 74 na 78, na Is-haaq bin Raahawayh katika *Musnad* Juz. 1, uk. 39, na Twabarani katika *al-Kabir* Juz. 24, uk. 139, na wengineo. Akasema Hafidh Haythami katika *Majmaul-Zawa'id* Juz. 3, uk. 17: “Na watu wa Ahmad ni watu wakweli.” Na akaizingatia ni sahihi Hafidh ibn Hajar katika *Fat'hu-Baari* Juz. 9, uk. 487. Lakini hadithi hii ameleza ibn Abi Hatam katika *Ilalul-Hadithi* Juz. 1, uk. 438, na si ya kawaida kwa kuwa inapingwa na hadithi ya Ummu Atwiya iliyopo kwa *Bukhari* 313, na ya Ummu Habiba iliyopo kwa *Bukhari* 1280 pia, na ya Bibi Zaynab iliyopo kwa *Bukhari* 5335: “Si halali kwa mwanamke mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho kujifunika nguo nyeusi kwa ajili ya maiti kwa kila usiku kwa siku tatu isipokuwa amkalie eda mume miezi minne na siku kumi.” Nayo pia ipo katika *Sahihi Muslim* 1486 na 1487 na 1490 na kwingineko.

Imam Ahmad amesema: “Hadithi hii ni kati ya hadithi zisizo za kawaida, ni yenye kutupiliwa mbali.” Na amenukuu Hafidh katika kitabu *Fat’hul-Bari*³⁶ kutoka kwa sheikh wake Hafidh Iraqiy, amesema katika kitabu *Sharhul-Tirmidhiy*: “Dhahiri ya hadithi hii ni kwamba si wajibu mfiwa kukaa eda baada ya siku ya tatu, kwa sababu Asmau bint Umays alikuwa mke wa Ja’far bin Abu Twalib kwa maafikiano, naye ni mzazi wa watoto wake Abdullah, Muhammad na Aun na wengineo, bali dhahiri ni katazo la kukaa eda, na kwamba haifai.

Nasema: Kwa sababu imekuja katika hadithi ya Ahmad na Ibn Hanban kwamba hakika Mtume ﷺ aliingia kwa Asmau katika siku ya tatu baada ya kuuawa Ja’far akasema: ‘Usikae eda baada ya siku yako hii.’³⁷ Na amejibu Hafidh Iraqiy³⁸ kwamba hakika hadithi hii si ya kawaida, inakwenda kinyume na hadithi sahihi, na hakika wamejumuika juu ya kinyume chake, akasema: ‘Na inategemewa kusemwa kuwa: Hakika Ja’far aliuawa kishahidi na mashahidi wapo hai mbele ya Mola Wao.’ Akasema: ‘Na dhana hii ni dhaifu, kwani halikupokewa hilo katika haki ya mwingine asiyekuwa Ja’far miongoni mwa mashahidi, na miongoni mwa wale ambao imekatwa shauri kuwa wao ni mashahidi, kama ilivyokatwa shauri kwa Ja’far, watu mfano wa Hamza bin Abdul-Mutwalib baba yake mdogo, na kama vile Abdullah bin Amru bin Haram, mzazi wa Jabir.’” Hafidh akasema: “Na inategemewa nyuma ya hilo majibu kadhaa aliyoyataja kisha akaiona ni hadithi dhaifu.”

HADITHI YA TISA

Ameipokea Said bin Mansur kutoka kwa Abu Ahwas kutoka kwa Aswim kutoka Zarri kutoka kwa Hudhayfa, amesema: “Tulikula

³⁶ *Fat’hul-Baari*, Juz. 9, uk. 487.

³⁷ Ameipokea Ahmad bin Hanbali Juz. 9, uk. 469 na sanad yake ni kwa nguvu ya kwanza.

³⁸ Ameinukuu kutoka kwake Hafidh Ibn Hajar katika kitabu chake *Fat’hul-Baari* Juz. 9, uk. 487.

daku mchana pamoja na Mtume ﷺ, naapa kwa Mwenyezi Mungu, lakini jua lilikuwa halijachomoza.”³⁹

Na ameipokea Twahawi kutoka kwa Zarri bin Habash, amesema: “Nilikesha kisha nikaenda msikitini, basi nikapita kwenye nyumba ya Hudhayfa, nikaingia kwake, basi akaamrisha akamuliwe mnyama aliyezaa, basi nikakamua, nikachemsha kwa sufuria, kisha akasema: ‘Kula’, nikasema: Hakika mimi ninataka kufunga, akasema: ‘Na mimi ninataka kufunga.’ Tukala kisha tukanywa tukaja msikitini. Basi ikasimamishwa Swala, akasema: ‘Hivyo ndivyo alivyofanya kwangu mimi Mtume ﷺ.’ Nikasema: Baada ya asubuhi? Akasema: ‘Baada ya asubuhi wakati jua bado halijachomoza.’”⁴⁰

Hadithi hii inatofautiana na hadithi sahihi zilizosema kinaga ubaga kwamba kula kunaishia kwa adhana ya Alfajir, wala hakundelei baada yake. Bali inatofautiana na Qur’ani tukufu. Jawzaqani amesema: “Hadithi hii imewachosha wanazuoni maarifa yake, na hakika wamezifanyia kazi baadhi ya wanazuoni, na amali kwayo ni dhafu, kwa sababu hadithi sahihi zinatofautiana nayo. Na Twahawi ameichukulia hadithi hii kwa maana ya kwamba ilikuwa ni kabla ya kuteremka kauli yake swt:

وَكُلُّوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ۗ

³⁹ Ameipokea Ahmad bin Hanbali Juz. 5 uk. 396 na Twahawi katika kitabu chake *Sharhu Maanil-Athaar*; Juz. 2, uk. 52 na Nasaai 2153 na Ibn Maaja 1695 na Hazimi katika kitabu *Naasikh wa Mansukh* 145 na 146 na akasema Hazimi: “Wamejikusanya watu wa elimu juu ya kuacha amali ya hadithi hii.”

⁴⁰ Ameipokea Twahawi katika *Sharhu Ma’anil-Athaar*, Juz. 2, uk. 52. Amesema Hafidh ibn Hajar katika *Fat-hul-Baari* Juz. 4, uk. 137: [Ameipokea kwa sanad yake sahihi kutoka kwa Salim bin Abiid Ashjai na anao usuhuba, na kwamba hakika Abu Bakr alimwambia: Hadithi hii inatofautiana na hadithi sahihi ya wazi wazi, hakika ulaji inashia kwa adhana ya Alfajiri, na wala hauendelei baada yake, bali inatofautiana na Qur’ani tukufu.

‘Na kuleni na kunyweni mpaka uwabainikie weupe wa al-fajiri katika weusi wa usiku’ (al-Baqarah; 2:187), na hili ni kosa, kwa sababu Hudhayfa aliifanyia kazi baada ya kifo cha Mtume 3, kama alivyoeleza Zarri, na yeye ni Tabiina.

HADITHI YA KUMI

Amepokea Muslim na Nasai na wengineo kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه, amesema: “Mtume ﷺ amesema: Mwenyezi Mungu ali-umba udongo siku ya Jumamosi, na akaumba majabali siku ya Jumapili, na akaumba miti siku ya Jumatatu, na akaumba ya-chukizayo siku ya Jumanne, na akaumba nuru siku ya Jumatano, na akaeneza humo wanyama siku ya Alhamisi, na akamuumba Adam baada ya alasiri siku ya Ijumaa. Ni kiumbe cha mwisho alichokiumba saa za mwisho za siku ya Ijumaa, baina ya alasiri hadi kuingia usiku.”

Hadithi hii si ya kawaida, kwani inafaidisha uumbaji wa ardhi na vilivyomo kwa siku saba, pamoja na kuwa Qur’ani inafaidisha hakika uumbaji wa mbingu na ardhi kwa pamoja ulikuwa kwa muda wa siku saba. Na hakika *Bukhari* ameikuta na ila hadithi hii katika kitabu chake *Tarikh*,⁴¹ amesema: “Wameipokea baadhi yao kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Kaab Akhbar, nayo ndiyo kauli sahihi.”⁴²

⁴¹ *Al-Tariikhul-Kabiir* Juz. 1, uk. 413 – 414.

⁴² Amesema Ibn Kathiir katika *Tafsiri* yake Juz. 1, uk. 99 chapa ya Shuab: “Hadithi hii ni miongoni mwa zile ngeni za *Sahih Muslim* na hakika amezungumza juu yake Ibn Madinii na Bukhari na zaidi ya mmoja miongoni mwa mahafidhi na wakaijaalia miongoni mwa maneno ya Kaab Akhbar, na hakika Abu Huraira aliisikia kutokana na maneno ya Kaab Akhbar na akakosea juu ya baadhi ya wapokezi wa hadithi akaifanya ni marfuu.” Hakika amekiri hili Ibn Taymiyya katika *Majmuatul-Fataawa* Juz. 17, uk. 236 na akasema: “Na lakini hili lina nadharia nyingi, amepokea Muslim hadithi nyingi na hakika zimejulikana kuwa hizo ni makosa.”

HADITHI YA KUMI NA MOJA

Amepokea Muslim kutoka katika njia ya Akrama bin Ammar amesema: “Ametuhadithia Abu Zamil, kutoka kwa Abbas, amesema: “Waislamu walikuwa hawamwangelii Abu Sufiyan wala hawakai naye, akamwambia Mtume ﷺ: “Nipe mambo matatu.” Mtume akasema: “Sawa”, Abu Sufiyan akasema: “Ninaye mbora wa Waarabu kwa uzuri wake ulioje, Ummu Habiba bint Abi Sufiyan, je, nikuoze huyo?” Akasema: “Ndio.” Abu Sufiyan akasema: “Na Mu’awiyah umfanye mwandishi wako.” Akasema: “Sawa.” Abu Sufiyan akasema: “Na unipe uamiri ili nipambane na makafiri kama vile nilivyokuwa nikipambana na Waislamu.” Akasema: “Sawa.”⁴³

Hadithi hii si ya kawaida, ni yenye kukataliwa. Ibn Hazim amesema: “Hakika hiyo ni yenye kubuniwa,”⁴⁴ na akamtuhumu Akrama bin Ammar, kwani inatofautiana na yale yaliyothibiti katika vitabu vya historia. Mtume ﷺ alimuoia Ummu Habiba wakati akiwa uhabeshi (Ethiopia) alipohamia huko na Waislamu wa mwanzo, na mahari yake ilimfikia kupitia kwa Najjash ambaye alimpa Dinari 400. Na pindi alipokuja baba yake Abu Sufiyan Madina ili kufanya upya ahadi kati yake na Mtume ﷺ, na akaingia kwake, alipotaka kukaa juu ya busati la Mtume ﷺ binti yake Ummu Habiba aliondoa na kuvuta busati, akasema: “Hakika hilo ni busati la Mtume ﷺ, na wewe ni mshirikina.” Abu Sufiyan akasema: “Ewe! Binti yangu, hakika imekupata baada yangu shari.” Na hili limeafikiwa na watu wa historia.

Ama kuhusu kauli ya Abu Sufiyan: “Na unipe uamiri” na Mtume kusema: “Sawa,” hakika Qurtuniy amesema: “Katu haijawahi

⁴³ Ameipokea *Muslim* 2501.

⁴⁴ Amenukuu hiyo Nawawi katika *Sharhu Muslim* Juz. 16, uk. 63, na akakiri hilo Ibn Taymiyya pia katika *Majmuatul-Fataawa* Juz. 17 uk. 236!! Na Dhahabi katika *Sayr Aalam Nubalaa* Juz. 7 uk. 137 na Ibn Jawzi!!

kusikika kwamba Mtume alimpa uamiri yeye, hadi alipokufa, na vipi Mtume ﷺ asitekeleze ahadi? Hili ni kati ya yale ambayo haya-fai juu yake. Na Abu Sufiyan alisilimu mwaka wa ukombozi wa Makka bila kupenda, na walikuwa Masahaba hawakai naye, wala hawamwangelii yeye kwa kitendo chake alichomtendea Mtume ﷺ na Waislamu wakati wa ushirikina wake, kwani wakati wa ushirikina hakufanya yeyote kama alivyofanya yeye. Na Mu’awiyah hakuwahi kuwa mwandishi wa Wahyi, bali hakika alikuwa akiandika barua. Na haikusihii kutoka kwake ila uandishi wa barua mbili. Basi wale ambao wanasema: Hakika yeye alikuwa akiandika Wahyi ni wenye kukosea.”

HADITHI YA KUMI NA MBILI

Kutoka kwa Abu Huraira na Ibn Abbas na Aisha, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: “Mwenyezi Mungu awalaani Mayahudi ambao wali-yafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni misikiti.”⁴⁵ Hadithi hii imethibiti katika Sahihi Mbili na vitabu vinginevyo kutoka katika njia mbalimbali, na hakika wameitendea kazi wengi miongoni mwa wanazuoni wa kale na wa sasa, na hawakugundua yale yaliyopo miongoni mwa sababu na ila ambazo hupelekea hadithi kuachwa na kutotendewa kazi. Hakika Qur’ani tukufu inapingana na hadithi hii kwa mitazamo mitatu:

1. Mwenyezi Mungu ameeleza habari za Mayahudi kwamba wao wamesema:

إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni fukara na sisi ni matajiri.” (3:181),
na wakasema tena:**

⁴⁵ Ameipokea hiyo Bukhari katika maudhui mbalimbali, kati ya hayo ni: 1330 na Muslim 529, nayo ni yenye kukataliwa kama vile alivyosema mwandishi.

يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ

“.....Mkono wa Mwenyezi Mungu umefungwa.....” (al-Maidah; 5:64), vilevile wakasema: “Hakika Mwenyezi Mungu alipoumba mbingu na ardhi alipumzika Jumamosi.” Na wakamnasibishia majuto yeye, na yasiyokuwa hayo miongoni mwa yale yanayopingana na shani ya Mwenyezi Mungu, wala hayafai katika haki yake, basi vipi wanafanya makaburi ya Mitume Wake kuwa ni misikiti? Hili haliingii akilini.

2. Hakika Mayahudi wanawaudhi Mitume. Amesema (s.w.t):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ آذَوْا مُوسَىٰ فَبَرَّأَهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا
وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِيهًا

“Enyi ambao mlioamini msiwe kama wale ambao walimuudhi Musa, lakini Mwenyezi Mungu alimtakasa na waliyoyasema; naye alikuwa ni mwenye heshima mbele ya Mwenyezi Mungu.” (al-Ahzaab; 33:69).
Na akasema (s.w.t):

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَا قَوْمِ لِمَ تُوَدُّونَنِي وَقَدْ تَعْلَمُونَ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ
إِلَيْكُمْ

“Na Musa alipowaambia watu wake; Enyi watu wangu! Kwa nini mnaniudhi nanyi mnajua kuwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu niliyetumwa kwenu?” (as-Saf; 61:5). Walifanya hivyo japokuwa Musa ﷺ alikuwa kwao ni Nabii wao adhimu mno, na mwenye kuleta sharia zao. Walimuudhi Nabii Daud ﷺ, wakamdhania kuwa amezini na mwanamke wa Uriya na kwamba alibeba ujauzito wake. Na wakamnasibisha yeye

na unywaji wa pombe. Na wakaukataa utume wa Suleimani عليه السلام na wakasema: “Alikuwa mfalme mwenye hekima, na ufalme wake aliujenga kwa msingi wa uchawi.” Na wakamsingizia Maryam عليها السلام kwa tuhuma nzito, kama ilivyokuja katika Qur’ani tukufu, na kama walivyo mtuhumu Nabii Isa عليه السلام kuhusiana na nasaba yake. Basi inafikiana vipi kuudhi kwao Mitume pamoja na ufanyaji wao makaburi yao kuwa ni misikiti? Na hili haliingii akilini!

3. Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameeleza habari ya Maya-hudi kuwauwa Mitume, akasema (s.w.t):

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّينَ بِغَيْرِ الْحَقِّ ذَٰلِكَ
بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ

“Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa ishara za Mwenyezi Mungu na wakiwaua Manabii pasipo haki. Na hayo ni kwa sababu ya kuasi kwao na kupituka mipaka.” (2:61), na pia akasema:

أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُكُمْ اسْتَكْبَرْتُمْ فَفَرِيقًا كَذَّبْتُمْ
وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ

“Kila alipowafikia Mtume kwa yale yasiyopenda nafsi zenu, mlitakabari, kundi moja mkalikadhibisha na kundi jingine mkaliua!” (2:87). Zimefaidisha Aya hizi hali za Mayahudi kwa Mitume wao, zikieleza mambo mawili: Ukadhibishaji na mauaji, na akasema (s.w.t):

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّينَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ
يَأْمُرُونَ بِالْقِسْطِ مِنَ النَّاسِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

“Hakika wale ambao wanazikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na wakawaua manabii pasipo haki na wakawaua wanaoamrisha mambo ya haki, wabashirie adhabu iumizayo.” (Aali-Imran; 3:21).

Zimefaidisha Aya hizi kwamba Mayahudi walikuwa wanawaua watu wema ambao walikuwa wakipita njia ya Mitume, na akasema (s.w.t):

وَضْرِبَتْ عَلَيْهِمُ الدَّلَّةَ وَالْمَسْكَنَةَ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ ۗ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّينَ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوْا
وَكَانُوا يَعْتَدُونَ

“Na ikapigwa juu yao (chapa ya) udhalili na umaskini; na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa ishara za Mwenyezi Mungu na wakiwaua Manabii pasipo haki. Na hayo ni kwa sababu ya kuasi kwao na kupituka mipaka.” (al-Baqarah; 2:61).

Na akasema Mwenyezi Mungu:

قُلْ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ قَبْلِي بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالذِّكْرِ ۗ قُلْتُمْ فَلِمَ قَتَلْتُمُوهُمْ إِنْ
كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Sema: Hakika waliwajia Mitume kabla yangu kwa hoja zilizo wazi-wazi na kwa hayo mliyosema basi mbona mliwaua kama mu wakweli?” (Aali-Imran; 3:183). Na akasema Mwenyezi Mungu:

فَبِمَا نَقْضِهِمْ مِيثَاقَهُمْ وَكُفْرِهِمْ بِآيَاتِ اللَّهِ وَقَتْلِهِمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ
وَقَوْلِهِمْ قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۗ بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا

وَبِكْفَرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ بُهْتَانًا عَظِيمًا وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ
عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ

“Basi (tuliwalaani) kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, na kuzikufuru kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuua kwao Manabii pasi na haki, na kusema kwao nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru yao. Basi hawataamini ila wachache tu. Na kwa kufuru yao na kumsingizia kwao Maryam uwongo mkubwa. Na kwa kusema kwao: Sisi tumemua Masihi Isa, mwana wa Maryam, Mtume wa Mwenyezi Mungu.....” (4:155-157).

Na angalizo hapa ni kwamba, hakika Mwenyezi Mungu ameeleza katika Aya hizi kwamba Mayahudi wanaua Mitume, kwa kutumia kitendo cha wakati uliopo kwa kuashiria kuwa uuaji wa Mitume umekuwa ni desturi yao ikitokea kila alipokuwa akija Mtume, na waliendelea juu ya hili mpaka alipotumwa Mtume Muhammad ﷺ. Basi wakajaribu kumuua mara mbili; mara ya kwanza pindi walipompelekea bega la mbuzi lenye sumu. Na hadithi hii ipo katika *Sahih* Mbili.⁴⁶ Na mara ya pili ni wakati alipokwenda katika ukoo wa Bani Nadhir akiwaomba msaada wao katika fidia ya wauaji wawili, ambao baina ya watu wao na ukoo wa Bani Nadhir kuna makubaliano na mkataba. Mayahudi wakasema kumwambia Mtume ﷺ: “Ndio, ewe Abul-Qasim tunakusaidia juu ya yale uliyoyapenda, katika yale uliyotuomba msaada sisi. Kaa tukupatie chakula na utarajea baadaye kwa ajili ya haja yako.” Basi akakaa akiegemea kibambaza cha nyumba zao.

Basi wakaende chemba baadhi yao na wakasema: “Hakika hamtompata mtu huyu tena katika hali kama hii, basi ni nani atakayepanda juu ya nyumba na kurusha jiwe kubwa kutoka sakafuni ili tumzimze na mtu huyu.” Basi wakamchagua kwa jukumu hilo Amru

⁴⁶ Ameipokea *Bukhari* 2617 na *Muslim* 2190.

bin Jahashi bin Kaab akiwa mmoja wao, akasema: “Mimi nitalifanya hilo.” Akapanda juu ya dari ili amwanguhie Mtume ﷺ jiwe, na Mtume ﷺ akiwa na baadhi ya Masahaba wake, miongoni mwao Abu Bakr, Umar na Ali ﷺ. Basi ikamjia habari kutoka mbinguni ya yale waliyoyakusudia wale watu. Mtume ﷺ akasimama na kuanza kurudi Madina.⁴⁷

Kwa hivyo historia ya Mayahudi imetapakaa damu kwa kuwa Mitume na watu wema, na yule ambaye aliokoka na mauaji yao hakusalimika na kumkadhibisha kwao na kumuudhi kwao, basi inakuwaje wafanye makaburi ya Mitume wao kuwa misikiti? Hili haliingii akilini.

Na hili ni kati ya maswala ambayo hajayagundua yeyote kabla yangu miongoni mwa wanazuoni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kustahiki kujisifu na Mwenye fadhila.

HADITHI YA KUMI NA TATU

Amepokea Abu Daud na Tirmidhiy na Ibn Majah kutoka katika njia ya Sammak kutoka kwa Abdullah bin Amira, kutoka kwa Ahnaf bin Qays, kutoka kwa Abbas bin Abdul-Mutwalib ﷺ, amesema: “Nilikuwa Bat’hai katika kundi miongoni mwao alikuwa ni Mtume ﷺ, basi likapita wingu kwao, akaliangalia, akasema: ‘Mnaitaje hiki?’ Wakasema: ‘*Sahabat* (Wingu).’ Akasema: ‘Na *Muznu* (Wingu)?’ Wakasema: ‘Ndio na *Muznu*’, akasema: “Na *Anan* (Wingu)?’ Wakasema: ‘Ndio na *Anaan*.’ Mtume akasema: ‘Je, mnajua umbali uliopo baina ya mbingu na ardhi?’ Wakasema: ‘Hatujui.’ Akasema: ‘Umbali uliyopo baina ya hivyo viwili ima ni miaka sabini na moja au sabini na mbili au sabini na tatu, kisha

⁴⁷ *Siiratul-Nabawiyya*, Juz. 4 uk. 144 cha Ibn Hisham na *Tariikh Twabari*, Juz. 2, uk. 84 na *Tariikh Ibn Kathiir* Juz. 4, uk. 332.

mbingu ya juu yake ni vivyo hivyo, mpaka mbingu saba. Kisha juu ya mbingu ya saba kuna bahari, umbali uliopo kati ya chini yake na juu yake ni sawa na umbali uliopo baina ya mbingu moja na mbingu nyingine. Kisha juu yake kuna vilele vinane (malaika walio kama vilele), umbali uliopo baina ya kucha zao na magoti yao ni sawa na umbali uliopo kati ya mbingu moja na mbingu nyingine. Kisha juu migongo yao kuna Arshi, na umbali uliopo kati ya chini yake na juu yake ni sawa na umbali uliopo kati ya mbingu moja na mbingu nyingine, kisha Mwenyezi Mungu yuko juu ya hapo.”⁴⁸

Tirmidhiy amesema ni hadithi nzuri. Lakini si kweli, kwa sababu Abdullah bin Umaira hakusikia kutoka kwa Ahnaf, kama alivyosema Bukhari. Kisha hakika Sammak wametofautiana juu yake, kama alivyosema hilo yeye mwenyewe Tirmidhi katika *Tahdhibul-Tahdhib*, na hadithi baada ya haya si ya kawaida, Ibn Arabi amesema: “Hakika hiyo ni kati ya zile za Kiyahudi, na ushahidi kuwa ni hadithi isiyo ya kawaida ni kutokana na mambo yafuatayo:

⁴⁸ Ni hadithi iliyobuniwa na batili. Ameipokea Ahmad bin Hanbali katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 106 na Abu Ya’ali 6713 na Hakim Juz. 2, uk. 501 na katika sanad yake yupo Yahya bin Raazi Jabali. Ahmad bin Hanbali amesema kumhusu yeye: “Ni muongo mbunifu wa hadithi.” Na akasema Falas, Nasaai na Daarū Qutni: “Ni mwenye kuachwa.” Na Sammak alikuwa akimsomea naye akisikiliza. Na Abdullah bin Umaira ambaye inamzunguka hadithi hii ametajwa na Aqili na Ibn Uday kuwa ni miongoni mwa wadhaifu, na Dhahabi akasema: “Hajulikani.” Na ametajwa na Ibn Haban katika kitabu *Thuqaat Ala Aadathi fi Tawthiiq Majaahil*, na hadithi kwa sanad hii ni dhaifu. Na amebakia Ahnafu, naye ni mwenye kuangushwa kutoka katika sanad yenye kukatika, kwa sababu haijulikani ni wapi Ibn Umaira alisikia kutoka kwa Ahnaf kama alivyosema Bukhari. Angalia kitabu *Tahdhibul-Kamaal* Juz. 15, uk. 386. Na ameitoa Abu Daud 4723 na Tirmidhiy 3320 na Ibn Majah 193, na Bayhaqi katika kitabu *Al-As-maau wa Sifaat* uk. 399; na Ibn Jawzi katika kitabu *Ilalu-Munaahiyat* Juz. 1, uk. 24 – 25. Na Ajuuri katika kitabu chake *Al-Shariia* uk. 292 na Ibn Khuzaima katika kitabu chake *Tawhiid* uk. 102; na Waliid bin Abdullah bin Abi Thaur Marhabi amezungumziwa na Ibn Muin kuwa: “Sio chochote”, na akasema Ibn Namiir: “Ni muongo.” Na akasema Aqili: “Anahadithia hadithi kutoka kwa Sammak zichukizazo wala hafuatwi.”

1. Hakika hiyo inatofautiana na hadithi chungu tele ambazo zinafaidisha kuwa kati ya mbingu na ardhi ni miaka mia tano. Vivyo hivyo kati ya mbingu moja na mbingu nyingine, na hakika imekusanywa hiyo na hadithi nyingine na kuhitimi-sha kwamba masafa yanatofautiana kutokana na utofauti wa kasi ya mwendo na udhaifu wake. Mwendo wa mnyama ni wa haraka zaidi kuliko mwendo wa mtu wa kutembea kwa miguu. Ndio ukusanyaji huu bado ni dhaifu, kwa sababu tofauti ya mwendo huwa ukadiriaji wa masafa yaliyopo baina ya mji mmoja na mwingine, miongoni mwa maeneo yanayofikwa na watu na wanyama. Ama maeneo yaliyopo kati ya mbingu na ardhi, wala hawezi kuyakadiria binadamu asilani, bali hilo ni mahsusi kwa malaika, na kati ya malaika hakuna mwenye nguvu na dhaifu, bali malaika wanatembea kutoka ardhini mpaka mbinguni kwa punde tu, na hakika amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t):

يُدَبِّرُ الْأَمْرَ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ
مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ

“Hulipanga jambo kutoka mbinguni hadi ardhini, kisha linapanda kwake katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu....”
(as-Sajdah; 32:5).

2. Hakika yeye amejaalia wabeba Arshi kuwa hawana mbawa. Na hili linatofautiana na yale yaliyokuja katika Qur’ani na Sunnah kuhusu wasifu wa Malaika, kwamba wao ni wenye mbawa. Kisha *Tiis* (neni la kiarabu lililotumika kuwasifu Malaika hao) ni sifa mbaya kwa Waarabu, hakika Mtume (s.a.w.w) alilitumia kwa mtu ambaye anaoa mke ili awe halali kwa mumewe, na hiyo ni sifa mbaya. Kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu

amewalaumu washirikina ambao waliwafanya malaika ni wanawake, na mwanamke ni bora kuliko *Tiis*.

HADITHI YA KUMI NA NNE

Amepokea Ibn Khuzaima na Ibn Jariir katika *Tafsiir* kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: “Hakika *Kursiyyi* ni kanyagio la nyayo mbili, na Arshi hawezi yeyote kukadiria ukubwa wake.”⁴⁹ Na amepokea Ibn Jarir mfano wake kutoka kwa Abu Musa na wengineo.⁵⁰

Ameipokea Hafidh Abu Ismail Harawi katika kitabu chake *Ar-baiina* na ameandika kwa anwani: “Mlango unaohusu kuweka Mwenyezi Mungu unyayo Wake juu ya *Kursiyyi*.” Hadithi hii si ya kawaida, haifai kuitakidi hivyo, na la kushangaza kutoka kwa Harawi ni kule kuifanya hadithi hii kuwa ni kati ya dalili za Tawhid.

⁴⁹ Ameipokea Twabarani katika *Al-Kabiir* Juz. 12 uk. 39, na Hakim Juz. 2, uk. 282 na Abdullah bin Ahmad katika kitabu chake *Al-Sunna* Juz. 1, uk. 301 na 586 na Khatiib katika *Tariikh Baghdad* Juz. 9, uk. 251 na Ibn Jawzi katika kitabu *Ilalu-Mutanahiya* Juz. 1, uk. 22 na Ibn Jariir pale alipoitaja katika *Tafsiir* yake Juz. 3, uk. 10 hakuipa nguvu kwa kuiegemeza kwa Ibn Abbas, bali amepokea kuwa ni kutokana na kauli ya Muslim Batwiin. Nayo ni dhaifu, haithibiti kutoka kwa Ibn Abbas kama nilivyolibainisha hilo katika barua mahsusii iliyochapishwa pamoja na kitabu *Qawlul-Asaad*, jina lake ni *Ilaam Thaqaalain Bi Khurafat Kursiyyu maudhiu Qadamain*, na lilothibiti kutoka kwa Ibn Abbas katika tafsiiri ya *Kursiyyu* katika aya hii ni imeenea elimu yake. Ameipokea kutoka kwake Ibn Jariir katika *Tafsiir* yake Juz. 3, uk. 9, na akasema huko Juz. 3, uk. 11: [Na ama ambalo linajulisha juu ya kusihi kwake ni dhahiri ya Qur’ani tukufu. Kauli ya Ibn Abbas ambayo amepokea Ja’far bin Mughira kutoka kwa Said bin Jubair kutoka kwake ni kwamba hakika yeye alisema: Ni elimu yake...]. Na akasema Al-Majd Qayruuz Abaad katika kitabu chake *Al-Kamusi Al-Muhiit*: [Na *Kursiyyu* kwa kuweka dhamma (u) na kasra (i): Ni kitanda na elimu]. Na inaunga mkono hili, pia hakika Bukhari ametaja katika *Sahih* yake kutoka kwa Said bin Jubair amesema: Hakika *Kursiyyu* ni elimu yake. Angalia kitabu *Fat-hul-Baari* Juz. 8, uk. 199 kabla ya hadithi nambari 4535 moja kwa moja.

⁵⁰ Ameipokea Ibn Jariir katika kitabu chake cha *Tafsir* Juz. 3, uk. 9-10 na Bayhaqi katika kitabu *Al-Asmaau wa Sifaat* uk. 404 kutoka kwa njia ya Amaara bin Umair, kutoka kwa Abu Musa, na sanad hii ni yenye kukatika! Kwa sababu ya Amaara bin Umair amepokea kutoka kwa Ibrahim bin Abi Musa na wala hakumwacha Abu Musa.

Yaani dalili ya Tawhidi inapatikana katika habari inayomfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe Wake. Na umekuja ufananishaji huu wa kinaga ubaga katika maneno ya Dhahak ambayo ameyapokea Ibn Jarir katika *Tafsiir* yake, aliposema: “Amenihadithia Muthanna: Ametuhadithia Is’haq: Ametuhadithia Abu Zahir, kutoka kwa Juwair-bar, kutoka kwa Dhahak kuhusu kauli yake (s.w.t): **“Elimu Yake imeenea mbingu na ardhi.” (2:255)**, akasema: “Ni kiti chake ambacho kimewekwa chini ya Arshi, ambacho wafalme huweka nyayo zao juu yake.”⁵¹ Na ufananishaji huu ni wa wazi bayana, lakini sanad ya kufika kwa Dhahak haisihi, kwayo yupo Jubair naye ni uozo.

Wala siachi kumshangaa yule ambaye anategemea katika Tawhid ya Mwenyezi Mungu na sifa Zake juu ya habari ya mtu mmoja ambayo haina faida yoyote katika mlango huu, hususan ikiwa ni kauli ya Sahaba, kama athari hii isiyo ya kawaida. Na hapo baadaye kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafafanua maana hii.

HADITHI YA KUMI NA TANO

Imethibiti katika *Sahih* Mbili kutoka kwa Anas bin Malik kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: “Ataingizwa motoni, utasema: Je, kuna ziada? Hadi aweke unyao wake utasema: Basi basi basi.”⁵²

Na vilevile ndani ya hizo *Sahih* Mbili kuna riwaya kutoka kwa Abu Huraira, amesema: “Na ama moto wala haujai mpaka aweke

⁵¹ *Tafsiir ibn Jarir*, Juz. 3, uk. 10.

⁵² Hii ni jumla ya zile hadithi za Kiyahudi zenye kuingizwa katika sahihi mbili bila kusita! Na hadithi hii ni kutoka katika hadithi za Anas bin Malik na Abu Huraira na Abu Said Khudri, na wote wao ni miongoni mwa wale waliopokea kutoka kwa Kaab Akhbar, na ametanabahisha Bukhari katika sahihi yake 4849 juu ya hadithi hii kuwa ni kati ya zile ambazo zimepokewa zikikomea kwa Swahaba! Na hili linajulisha kuwa ni kauli ya Abu Huraira na sio kauli ya Mtume ﷺ kwa uhakiki! Bukhari amesema huko: [Kutoka kwa Abu Huraira ameinyanyua na mara nyingi zilikuwa zikikomea kwa Abu Sufiyan...]. na hadithi hii ya Anas amepokea Bukhari 4849, 4850, 7449 na Muslim 2848 na wengineo.

mguu wake, basi utasema: Basi basi basi, hapo utajaa na utapanda baadhi yake juu ya baadhi.”⁵³ Ameipokea hadithi hii kwa riwaya mbili Abu Ismail Harawi katika kitabu *Arbaiina*, riwaya ya kwanza ameandika kwa anwani “Mlango wa kuthibitisha unyayo wa Mwenyezi Mungu aliyetukuka.” Na riwaya ya mwisho ameandika kwa anwani “Mlango wa dalili inayothibitisha kwamba hakika unyayo ni mguu.”⁵⁴ Na hii ni kutokana na upotovu wa mtu huyu, katika uthibitishaji wa sifa za Mwenyezi Mungu aliyetukuka anashikamana na habari ya mtu mmoja yenye tafsiri nyingi ili kuiletea taawili.

Tunasema katika kumrudi yeye kwamba:

Mosi: Hadithi hii imekuja na ziada kinyume na ilivyo katika Qur’ani. Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema:

يَوْمَ نَقُولُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَأَتْ وَتَقُولُ هَلْ مِنْ مَزِيدٍ

“Siku tutapoiambia Jahannamu: Je, umejaa? Nayo iseme je, kuna ziada.” (Qaf; 50:30).

Na hadithi hii hata kama ni sahihi bado haina nguvu kuliko Qur’ani, wala haifai kukata shauri kwa kuyakubali yale ya ziada na kuifanya ni sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Pili: Ametaja Ibn Jawzi⁵⁵ kwamba hakika hadithi ambayo imekuja kwa lafudhi mguu ni upotoshaji kutoka kwa baadhi ya wapokezi, kwa dhana yao kwamba makusudio ya unyayo ni kiungo, hivyo

⁵³ Hadithi za Kiyahudi hazisihi kama ilivyokwisha kutangulia! Ameipokea Bukhari 4849, 4850, 7449 na Muslim 2846.

⁵⁴ Huko kuna hadithi katika *Sahihi Bukhari* 4850: “Wala hajui mpaka aweke mguu wake basi utasema Basi basi” basi zingatieni uzushi na upotoshaji huu. Na hadithi za Kiyahudi vipi zikawa hadithi za Mtume katika sahihi mbili zilizo maasum kwa baadhi ya vipofu kutokana na ufuataji na ung’ang’anizi!

⁵⁵ Katika kitabu *Daf’u Shubha Tashbih* kwa uhakiki wa mja dhaifu fukara hadi kwa Mwenyezi Mungu uk. 170.

wakaipokea kwa maana na wakakosea. Imekwisha. Na kwa kuwa dhana ya kwamba hadithi imepokewa kwa maana ipo kuhusiana na hadithi, basi haifai kuinasibisha na Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Tatu: Hakika hadithi hii ni yenye kuawiliwa kwa mitazamo mingi. Imeelezwa katika kitabu *Fat’hul-Bari* na vitabu vinginevyo.

Nne: Amesema Abu Wafai Ibn Aqil:⁵⁶ “Mwenyezi Mungu ametukuka na amepukana na kuwa hawezi kufanya jambo lake motoni mpaka aombe msaada kupitia kitu kingine kutokana na dhati yake au sifa yake, kwani Yeye ndiye aliyeuambia moto: “Kuwa baridi na salama.” 21:69, basi yule anayeumrisha moto uliowashwa na mwingine, ubadili tabia yake, nayo ni kuunguza, na hatimaye unabadilika vipi ahitaji msaada katika moto aliouwasha mwenyewe?” Imekwisha.

Inakuwaje pamoja na mushkeli huu Harawi anakata shauri kwa kuthibitisha unyayo na mguu kuwa ni sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t)? Na sifa za Mwenyezi Mungu hazithibiti ila kwa dalili ya kukata shauri kama vile Qur’ani au Sunnah sahihi yenye kuyakinisha, wala hakuna nafasi ya kutegemea taawili katika hilo.

Muhtasari ni kwamba hakika ni hadithi sahihi⁵⁷ kwamba moto utasema je, kuna ziada? Mpaka Mola mlezi aweke unyayo wake ndani yake, lakini haifai kukata shauri kwamba hakika unyayo ni sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), kwani neno hilo linaweza kufanyiwa taawili. Wala sifa hainasibishwi na Mwenyezi Mungu ila ile iliyothibiti kwa yakini. Basi yule mwenye kuthibitisha unyayo kwa Mwenyezi Mungu kisha anadhani anamtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na viungo, huyo ni mwenye kujipinga mwenyewe. Kwa hakika yeye amethibitisha kiungo kisha analikanusha hilo.

⁵⁶ Ameinukuu hiyo kutoka kwake Allama ibn Jawzi katika kitabu *Daf’u Shubhu Tashbih Biakuffi Tanziih* uk. 174 kwa lafudhi iliyo karibu na hili.

⁵⁷ Na ama kwa Abdul-Qadir mtumishi wa Sayyed Abdullah ibn Swadiiq basi hadithi hiyo sio sahihi kwa yale ambayo niliyotangulia kuyaeleza.

HADITHI YA KUMI NA SITA

Imethibiti katika Sahihi Mbili kutoka kwa Mughira amesema: “Alisema Saad bin Ubada: ‘Lau ningelimuona mwanamme pamoja na mwanamke wangu ningeliwapiga kwa upanga na nisingelikuwa mwenye kuwasamehe.’ basi habari hiyo ikamfikia Mtume ﷺ....” hadithi. Bukhari ameandika hiyo chini ya anwani: [Kauli ya Mtume ﷺ: Hakuna mtu mwenye wivu zaidi kuliko Mwenyezi Mungu].⁵⁸ Harawi katika kitabu chake *Arbaina* ameandika hiyo chini ya anwani: “Mlango wa kubainisha kwamba Mwenyezi Mungu (a.j) ni mtu.” Imekwisha.

Ibn Batwal katika kitabu *Sharhul-Bukhari* amesema⁵⁹: “Umma umekusanyika juu ya kwamba Mwenyezi Mungu hasifiwi kwa sifa ya mtu...” Imekwisha.

Amesema Ismaili⁶⁰: Kauli yake: ‘Hakuna mtu mwenye wivu zaidi kuliko Mwenyezi Mungu’ si kuthibitisha kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni mtu, bali hilo ni kama ilivyokuja: ‘Hakuumba Mwenyezi Mungu kitu adhimu zaidi kuliko Aya Kursiyy.’ kwani hiyo haiko katika kuthibitisha kuwa hakika Aya Kursiyy imeumbwa,⁶¹ bali makusudio ni kwamba hicho ni adhimu zaidi kuliko viumbe, na hiyo ni kama vile anavyosema mwenye kumsifu mwanamke mkamilifu mwenye umbo zuri kwa kusema: ‘Kati ya watu hakuna mwanaume anayeshabihiana naye’, huwa anataka kumfadhilisha yeye juu ya wamaume na sio kwamba yeye ni mwanaume. Imekwisha.

⁵⁸ Angalia katika kitabu *Fat-hul-Baari*, Juz. 13, uk. 399 katika kitabu Tawhiid, na hakika ameitoa hiyo kwa mlango huu pamoja na kuwa hakuipokea kwake, nayo ni kutokana na vitendo vya wapokezi wenye kuunga mkono wale ambao wanawaita hao Juhmiyya!!

⁵⁹ *Fat'hul-Baari*, Juz. 13, uk. 400.

⁶⁰ *Fat'hul-Baari*, Juz. 13, uk. 401.

⁶¹ Bali hicho kimeumbwa kimezuka kwa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Sura Anbiyai: 2.

Na Ibn Batwal amesema:⁶² “Yametofautiana matamshi ya hadithi hii, na wala haikuja tofauti katika hadithi ya Ibn Mas’ud رحمته iliyokuja kwa neno: “Hakuna yeyote’ basi ikadhihiri kwamba neno ‘mtu’ limekuja sehemu ya neno ‘yeyote’ basi kama kwamba ni miongoni mwa vitendo vya mpokezi.” Kisha akasema: “Zaidi ya hapo ni kwamba hiyo ni miongoni mwa mlango wa utengaji kutokana na isiyokuwa jinsi yake, kama vile kauli ya (s.w.t):

مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتَّبَاعَ الظَّنِّ

‘Hawana ujuzi ila kufuata dhana tu’ (an-Nisa’a; 4:157), na dhana si katika aina za elimu.

Hafidh Ibn Hajar amesema⁶³: Na hili ndilo linalotegemewa, na hakika amelithibitisha Ibn Furak, na kutoka kwake amechukua Ibn Batwal baada ya yaliyotangulia, hivyo ukadiriaji ni kwamba watu wenyewe kusifika kwa wivu hawaufikii wivu wake, na hata kama haiwezekani kuwepo wivu kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), na hata kama si mtu kwa maana yake. Imekwisha. Angalia maneno yaliyobakia juu ya hadithi hii katika kitabu *Fat’hul-Bari*, Juz. 13, uk. 342.

Hitimisho ni kwamba Harawi katika kuthibitisha sifa za Mwenyezi Mungu (s.w.t) anategemea maneno yasiyomaanisha hilo atakalo, pamoja na dhana kubwa kwamba neno hilo ni kutokana na kitendo cha mpokezi, na hii si miongoni mwa dalili za Tawhiid.

HADITHI YA KUMI NA SABA

Ampokea Harawi katika kitabu *Arbaiina* kutoka kwa Ibn Abbas رحمته kwamba hakika Mtume ﷺ amesema: “Hakika Adam A alikuwa

⁶² Katika kitabu *Fat’hul-Baari*, Juz. 13, uk. 401.

⁶³ Katika kitabu *Fat’hul-Baari*, Juz. 13, uk. 342.

akisabihi tasbihi za Malaika, na akiswali Swala zao, wakati alipokuja ardhini, kutokana na urefu wake na ukaribu wake na mbingu. Basi Mwenyezi Mungu akaweka mkono wake juu yake akapungua kwenda ardhini kiasi cha dhira sabini.”⁶⁴ Harawi ameandika chini ya anwani: “Mlango wa kuthibitisha mikono miwili ya Mwenyezi Mungu (s.w.t),” na hadithi hii ni ya kuchukiza, na maana yake ni muhali. Na kwa nini Nabii Isa asiwe na urefu wa Adam mpaka asikie tasbihi za malaika mbinguni? Na hakika kati ya mbingu na ardhi kuna miaka mia tano. Na nini kilipunguza dhira sabini kutoka kwenye urefu wake? Basi hadithi hii ni yenye kuchukiza na ya kubuniwa! Na la kushangaza ni Harawi kuitaja hiyo katika dalili za Tawhiid.

HADITHI YA KUMI NA NANE

Amepokea Bayhaqi katika kitabu *al-Asmau Waswifat* kutoka katika njia ya Muhammad bin Falih, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Said bin Harith, kutoka kwa Abid bin Hanin, amesema: “Nilikuwa nimekaa msikitini, pindi alipokuja Qatada bin Nu'man رحمته, akaketi na kuanza kusimulia Hadithi, basi watu wakamzunguka, kisha akasema: ‘Twende zetu kwa Abu Said Khudri رحمته, hakika mimi nimepata habari kwamba anaumwa.’ Basi tukaenda mpaka tulipoingia kwa Abu Said Khudri رحمته, tukamkuta yeye amelala chali ameweka mguu wake wa kulia juu ya mguu wa kushoto. Tukamsalimu na tuka. Mara Qatadah akanyanyua mkono wake mpaka kwenye mguu wa Abu Said Khudri, akaushusha kwa nguvu. Abu Said akasema: ‘Subhaanallah ewe mtoto wa mama, umenisababishia maumivu.’

⁶⁴ Hadithi imewekwa na sheikh wa mwandishi, na sheikh wa sheikh wake wote wawili hawajulikani! Na aliye juu yao hao wawili ni Uthman bin Said Daarmi, naye ni mashuhuri mwenye imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ana mwili. Hadithi yake ni yenye kukataliwa! Na hakika amekiri mhakiki wa kitabu *Arbaiina* mwanafikihi mwenye imani ya kwamba Mwenyezi Mungu ana mwili, kwamba hadithi inafanana zaidi na iliyobuniwa! Basi Mwenyezi Mungu anawatosha waumini mapigano!!

Qatadah akasema: ‘Hilo ndilo nililolitaka, kwani hakika Mtume ﷺ alisema: Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) alipomaliza kuumba viumbe wake alilala chali, kisha akaweka mmoja wa miguu yake juu ya mwingine, kisha akasema: Haipasi yeyote miongoni mwa viumbe wangu afanye hivi.’⁶⁵ Abu Said akasema: Hakuna tatizo, sifanyi hivi tena.’”

Bayhaqi⁶⁶ amesema: [Hadithi hii ni yenye kuchukiza na wala si-kuiandika ila kutokana na mwelekeo huu. Na Falih bin Suleiman pamoja na kuwa anatokana na sharti la Bukhari na Muslim, lakini hawakuitaja hadithi yake hii katika *Sahih* zao, naye kwa baadhi ya mahafidhi si mtu hoja.... Na ikiwa ni mtu ambaye mahafidhi wametofautiana juu ya uaminifu wake, basi haithibiti riwaya yake katika mfano wa jambo hili adhimu. Na riwaya hii ina kasoro nyingine, nayo ni: Hakika Qatadah bin Nu'man alikufa zama za ukhalifa wa Umar bin Khatwab رضي الله عنه, na Umar ndiye aliyemswalia yeye, na Abid bin Hunain alikufa akiwa na miaka 105, hivyo hadithi yake kutoka

⁶⁵ Hadithi ni yenye kubuniwa. Amepokea Twabarani katika *al-Kabiiir*, Juz. 19, uk. 13 na Khalalu katika Sunnan yake na vinginevyo. Na hakika amebainisha sababu yake (kasoro yake) Bayhaqi katika kitabu *al-Asmaau wa Sifaat*, uk. 355.

Na miongoni mwa yale ambayo yanaunga mkono kuwa hadithi hii ni ya Kiyahudi ni yale aliyopokea Ibn Abi Swaiba katika *Muswanaf* Juz. 5, uk. 228 akasema: [Ametuhadithia Waqii kutoka kwa Abu Hilal kutoka kwa ibn Siriin kutoka kwa ibn Abbas رضي الله عنه: Hakika yeye amechukia kujilaza chini huku akiwa ameweka mguu wake mmoja juu ya mwingine. Basi Kaab akasema kumwambia yeye; uteremshe, kwani haifai kwa kiumbe kufanya hivyo]. Na kwangu mimi ni karaha (ni jambo lichukizalo). Aamenukuu ibn Abbas رضي الله عنه kutoka kwa Kaab Akhbar na kwamba Kaab Akhbar alisema kuwa aina hii ya ukaaji haipaswi kwa kiumbe. Na amepokea Abu Awaana Juz. 5, uk. 269 akasema: [Ametuhadithia Salami akasema: Ametuelezea Abdul-Razzaq, kutoka kwa Mummar kutoka kwa Zahari kwa sanad yake: Nilimuona Mtume ﷺ amelala chali msikitini akiinua mguu mmoja juu ya mwingine, akasema Zahari: Amenipa habari mimi Said bin Musayyib akasema: Na ama Umar na Uthmani walifanya hivyo wala haina idadi, akasema Zahari: Kisha wakaja watu na jambo kubwa mno].

⁶⁶ Katika kitabu *Al-Asmaau wa Sifaat* uk. 355. Na akasema Albani maneno yenye kupingana katika utoaji wa maelezo juu ya kitabu *Sunnan* cha ibn Abi Aswim Juz. 1, uk. 349: [Sanad yake ni dhaiifu na matini yake ni yenye kuchukiza kama kwamba hiyo inatokana na uwekaji wa Mayahudi, kwa hakika maafa hayo yatamkumba Said bin Harith].

kwa Qatadah ni yenye kukatika sanadi. Na kauli ya mpokezi ‘Basi tukaenda mpaka tulipoingia kwa Abu Said Khudri رضي الله عنه’, hairejei kwa Abid bin Hunain, na hakika inarejea kwa yule aliyeivusha kwake, na sisi hatumjui, wala hatukubali hadithi zilizo *mursali* (zilizovushwa) zinapozungumzia mambo ya hukumu, basi itakuwaje katika jambo hili adhimu?

Na yaliyonukuliwa katika habari hii hakika yanafanywa na wasio na shughuli wala kazi, yule aliyepatwa na uchovu na kupatwa na uvivu miongoni mwa wenye kustarehe kwa kulala chali, na wawekaji wa mguu mmoja juu ya mwingine. Na hakika Mwenyezi Mungu amewakadhibisha Mayahudi wakati walipomsifu Yeye kwa kustarehe na kupumzika baada ya kuumba mbingu na ardhi, akasema:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِنْ
لُغُوبٍ فَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ

“Na hakika tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake katika siku sita; na wala haukutugusa uchovu. Basi vumilia kwa hayo wayasemayo.....” (Qaf; 50:38-39), Bayhaqiy anasema: Na ama katazo la uwekaji wa mguu mmoja juu ya mwingine, kwa hakika limepokewa na Abu Zubair kutoka kwa Jabir kutoka kwa Mtume رضي الله عنه pasi na kisa hiki, na watu wa elimu wakatafsiri katazo hilo kwa maana ya kuhofia kudhihirisha utupu, nao ni paja, iwapo atanyanyua mguu wake mmoja juu ya mwingine akiwa amelala chali ilihali shuka ni dogo. Na kufanya hivyo (kunyanyua mguu mmoja juu ya mwingine akiwa amelala chali) ni jambo lenye kuruhusiwa kwa wote ikiwa hakuna hofu hiyo. Mwisho wa maneno ya Bayhaqiy.

Na hadithi hii pamoja na kuwa kwake ni yenye kuchukiza chukizo kubwa mno, pia ni ya kubuniwa. Kwa hakika wameichukua hiyo Mahanbali wenye imani kuwa Mola Manani ana umbo na mwili, kama vile Mhanbali Abu Bakr Swamit katika kitabu chake *As-Swifat*, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

Na Abu Bakr bin Abi Aswim katika kitabu chake *As-Sunnah*, Juz. 1, uk. 248 amesema: [Amesema Abu Is'haq Ibrahim Huza-mi: Na nimesoma kutoka katika kitabu chake kisha akakichana na akasema kuniambia mimi baada ya kuniomba samahani: 'Hakika mimi nimeapa kuwa sintakiona hicho ila nitakichana.' Basi ukakatika upande wa kitabu wenye maelezo kutoka kwa Muhammad bin Falih kutoka kwa Said bin Harith kutoka kwa Abdullah bin Manin, kwamba alisema: 'Nilikuwa nimekaa msikitini, pindi alipokuja Qatadah bin Nuuman رحمته. Akaketi na kuanza kusimulia Hadithi, basi watu wakamzunguka, kisha akasema: Twende ewe Ibn Manin kwa Abu Said Khudri رحمته, hakika mimi nimepewa habari kwamba yeye anaumwa.] Na akataja hadithi husika kama ilivyotangulia katika hadithi ya Bayhaqiy, isipokuwa sanadi imetofautiana katika maeneo mawili: Hapa anapokea Muhammad bin Falih kutoka kwa Said bin Harith. Kwa Bayhaqi amepokea Muhammad bin Falih kutoka kwa baba yake, na hii ndio yenye uzito.

Eneo lingine lenye tofauti ni kwamba: Hapa yupo Abdullah bin Manin, kwa Bayhaqi kutoka kwa Abid bin Hanin. Na Abdullah bin Manin kwa Nuni (N) yenye kutengeneza udogo kwa lugha ya Wamisri, wamepokea kutoka kwake Abu Daud na Ibn Majah. Na Yakub bin Sufiyan akamzingatia kuwa ni mkweli, na kauli yenye nguvu zaidi ni ile ya Bayhaqiy, kwa sababu Abid bin Hanin kwa Haa (H) yenye kutengeneza udogo, ni mwenyeji wa Madina, na Falih bin Sulaiman na mwanawe ni watu wa Madina, na Abid anapokea kutoka kwa Qatadah bin Nu'man, na Abdullah bin Maniin anapokea kutoka

kwa Amru bin Aswi. Na hadithi kwa hali zote mbili ni ya kubuniwa. Na kwa ajili hiyo aliapa Huzami Sheikh wa Ibn Abi Aswim kwamba hakika hataiona kwenye kitabu ila atakichana.

HADITHI YA KUMI NA TISA

Dhahabi amepokea katika kitabu *Tadhkarat Khwawaswi* kutoka katika njia ya Hafidh Abu Fadhli Naswar bin Muhammad ibn Ahmad Atwar Swaafi, amesema: Ametupa habari Ahmad bin Husein bin Muhammad Azhar huko Misri: Ametuhadithia Yusuf bin Yazid Qatwisi: Ametusimulia Walid bin Musa: Ametuhadithia Munabbih bin Uthman, kutoka kwa Ur'wat bin Ruwaim, kutoka kwa Hasan, kutoka kwa Anas bin Malik, kutoka kwa Nabii ﷺ, amesema: "Hakika waumini wa kijinni wana thawabu na wana adhabu." Basi tuka-muuliza yeye kuhusu thawabu zao na muumini wao, akasema: "Juu ya *Aarafu* na hawatakuwa wao peponi na umma wa Muhammad ﷺ." Tukasema: *Aarafu* ni nini? Akasema: "Ukuta wa peponi, unapita hapo mito, na hapo huota miti na matunda." Dhahabi akasema: Hadithi hii ni yenye kuchukiza mno.

Na ni wapokezi wa Bayhaqiy katika kitabu *Baa'ih*, na wa Ibn Asakir katika kitabu *Tarikh*, kutoka katika njia ya Ur'wat bin Ruwaim, kutoka kwa Hasan, kutoka kwa Anas bin Malik. Nayo ni hadithi yenye kuchukiza kama alivyosema Dhahabi, wala haiko mbali kuwa ni yenye kubuniwa na kupachikwa, kwa kutojulikana sanad yake na kuchukiza maana yake. Hadithi hiyo inaonesha kwamba waumini wa kijini sio miongoni mwa umma wa Muhammad ﷺ. Na hili ni tofauti na andiko na Ijmai. Ama kuhusu andiko, hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameeleza kwamba alimtuma Mjumbe Wake kwa walimwengu wote, na katika Surat ar-Rahman akawahutubia majini na watu. Na wote walikalifishwa kwa usawa, na katika Surat Jinni wakasema:

إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا
أَحَدًا

**“Hakika sisi tumeisikia Qur’ani ya ajabu! Inaongoza kwe-
nye uongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha
yeyote na Mola Wetu.” (al-Jinn; 72:1-2), na katika Sura Ahqaaf
kuna kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t):**

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفْرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا
أَنصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ

**“Na tulipokuletea kundi la majini kusikiliza Qur’ani. Basi
walipoihudhuria walisema: nyamazeni! Na ilipomalizwa, wali-
rudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.” (Ahqaaf; 46:29). Na
Ijmaai imethibiti kutoka kwa Waislamu wote kwamba Mtume 3
alitungwa kwa majini na watu, Ijmai hiyo imeelezwa na Ibn Hazm,
Ibn Abdul-Barri, Ibn Taymiyya, Suyutwi na wengineo na Mwenyezi
Mungu ni Mjuzi zaidi.**

HADITHI YA ISHIRINI

Imethibiti katika Sahihi kutoka kwa Abdullah bin Masuud رضي الله عنه,
amesema: Alikuwa mtu mmoja kwa Mtume ﷺ miongoni mwa watu
wa kitabu, akasema: “Ewe Abul-Qasim! Hakika Mwenyezi Mungu
huzishika mbingu juu ya kidole, na ardhi, miti na udongo juu ya
kidole, na viumbe juu ya kidole, kisha husema: ‘Mimi ni Mfalme,
mimi ni Mfalme.’” Basi nikamuona Mtume ﷺ akicheka mpaka
yakaonekana magego yake, kisha akasoma:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

“Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya kadiri yake.....” (al-An’am; 6:91).

Na amepokea Ahmad kutoka katika njia ya Hasan kwamba: Hakika Aisha alisema: Ombi ambalo Mtume ﷺ alikuwa akikithirisha kuliomba ni: “Ewe mbadilishaji wa nyoyo uthibitisha moyo wangu juu ya dini yako.” Aisha akasema: Ewe Mtume ninakuona ukikithirisha kuomba ombi hili, Mtume akasema: “Hakuna binadamu yeyote ila moyo wake upo baina ya vidole vyake viwili miongoni mwa vidole vya Rahman (s.w.t), na akipenda amsimamisha humsimamisha yeye na akipenda amuondoe humuondoa.” Amepokea Harawi hadithi ya Aisha katika kitabu *Arbaiina* na ameiandika kwa anwani: Mlango wa uthibitishaji wa vidole vya Mwenyezi Mungu (s.w.t)!! Na akasema Ibn Batwal:⁶⁷ “Utajo wa vidole hautafsiriwi kwa maana ya viungo bali hutafsiriwa kwa maana ya sifa miongoni mwa sifa za dhati. Na hili linanasibishwa na Ashairah.” Na amemuwafiki katika hilo Ibn Tin.

Khatwabi amesema: “Havijatajwa vidole katika Qur’ani wala katika Hadithi mkataa. Na imeshasemwa mara kwa mara kwamba neno Yaddi halina maana ya kiungo mpaka mtu adhani kwamba kuthibiti kwake ni kuthibitisha vidole, bali ni unyamazishaji uliotajwa na Mweka sharia, hana namna wala hafananishwi. Na huenda utajo wa vidole ni kutokana na uchakachujaji wa kiyahudi. Hakika Mayahudi ni wafananishaji, na kati ya mambo ambayo hudai kuwa ni kutoka katika Taurat ni matamshi yanayoingia katika mlango wa ufananisho, wala hayaingii katika madhehebu za Waislamu. Na ama uchekaji wake ﷺ kutokana na kauli ya Mayahudi huenda ni kwa kuridhia au kutokuridhia. Na ama kauli ya mpokezi: ‘kwa kumsadikisha’ ni dhana kutoka

⁶⁷ Maneno haya na ya baada yake yamenukuliwa katika kitabu *Fat-hul-Baari*, Juz. 13 uk. 398.

kwake, na hakika imekuja hadithi hii kutoka katika njia mbalimbali na hakuna ndani yake ziada hii. Na hata kama tukikubali kusihhi kwake, hakika wekundu wa uso huwa ni dalili ya haya, na unjano wake huwa ni dalili juu ya hofu. Hivyo jambo linakuwa ni tofauti na hivyo, kwani wekundu unaweza kuwa ni dalili ya jambo lililotokea mwilini kama vile shinikizo la damu, na njano inaweza kuwa ni dalili ya kukorogeka na mchanganyiko wa nyongo na mengineyo. Na kama kuna ulazima wa kuhifadhiwa hilo basi maana yake ni tafsiri ya kauli yake (s.w.t):

وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ ۗ

“Na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume.....” (az-Zumar; 39:67), yaani uwezo wake juu ya ukunjaji wake, na wepesi wa jambo juu yake katika ukusanyaji wake kama ukusanyaji wa kitu kiganjani mwa mtu pasi na kukusanya viganja vyake bali huvikunja kwa baadhi ya vidole vyake.” Mwisho wa maneno ya Khatwabi

Na Khatwabi hakukanusha uwepo wa vidole katika hadithi, bali alichokanusha ni kudai kuwa hadithi ni mkataa. Na maneno yake ni sahihi kama alivyosema, na makusudio ya utajo wa vidole kuwa ni sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) si jambo lenye kuafikiwa na wote, na bado kuna uwezekano mwingine wa tafsiri. Na Harawi ni mtu asiyejali katika uthibitishaji wa sifa maadamu tu iwepo katika hadithi, pasi ya kuchunguza je hiyo inatokana na kitendo cha mpokezi au mfano wa hilo.

HADITHI YA ISHIRINI NA MOJA

Ibn Jariir amepokea katika *Tafsiir* yake kutoka kwa Abdullah bin Khalifa, amesema: Mwanamke mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume

ﷺ akasema: “Muombe Mwenyezi Mungu aningize peponi.” Mtume akamtukuza Mwenyezi Mungu, kisha akasema: Hakika Kursii imeenea mbingu na ardhi, kwani Yeye huketi juu yake na sehemu ya kipimo cha vidole vinne hubakia.” Akakusanya vidole vyake kisha kasema: “Na hakika Kursii hiyo ina sauti kama sauti ya kipando kipya ambacho hutoa sauti kutokana na uzito wa mpandaji wake.”⁶⁸ Amejipokea vile vile kutoka katika njia ya Abdullah bin Khalifa kutoka kwa Umar.

Na hadithi hii ni yenye kuchukiza iliyobuniwa, na sanad yake sio sahihi. Na lile alilolinasibisha kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), ambalo ni kuketi, halijakuja katika Qur’ani wala katika hadithi. Huu nao ni ufananisho wa wazi wazi. Mwenyezi Mungu ametukuka kutokana na ufananisho wa matukio:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.” (ash-Shura; 42:11). Na miongoni mwa yale ambayo yanajulisha juu ya uchukizaji wake, ukiacha yale yaliyotajwa, ni kwamba hakika Mtume ﷺ alipitisha muda wa uhai wake mtukufu akiwalingania watu kwenda peponi na akiwa-

⁶⁸ Hadithi ya Abdullah bin Khalifa nayo ni hadithi ya kubuniwa mbaya, amejipokea ibn Abi Aswim katika *As-Sunna* Juz. 1, uk. 254 na 574 na wengineo kutoka kwa Umar. Na Abdullah bin Khalifa hajulikani hali yake. Hafidh katika *Al-Lisaan* Juz. 7, uk. 266 amesema: Ibn Hasan haukaribii kujulikana ukweli wake” na akasema katika *Taqriib*: “Ni mwenye kukataliwa” yaani dhaifu, na hadithi ameiona ni dhaifu mpingaji wa zama zetu!! Katika *Mukhtaswarul-Uluwi* uk. 246, na katika *Takhrij Lisunna* cha ibn Abi Aswim nayo ni yenye kubuniwa bila shaka. Na nimekuta hadithi hii ya sauti ya kipando imepokewa kutoka kwa Kaab Akhbar, jambo ambalo linafaidisha kwamba Kaab Akhbar ndio asili yake nayo ni chimbuko lake. Na hakika amejipokea Abu Sheikh katika *Kitabul-Udhamat* Juz. 2, uk. 612 kutokana na chapa iliyohakikiwa iliyopatikana katika mjaladi mitano, na katika ukurasa wa 91 kutokana na chapa isiyohakikiwa iliyopatikana katika mjaladi mmoja.

hamasisha kwa hilo. Na ndani ya Qur’ani Tukufu zipo Aya mbali mbali zinawalingania watu pepo na neema za kudumu zilizomo humo. Hivyo basi itakubalika vipi kumhusu mwanamke ambaye alimuomba yeye amuombee kwa Mwenyezi Mungu amuingize peponi, amjibu yeye kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kwamba ni vigumu kwa mwanamke huyo kuingia peponi? Zaidi ya hapo ni kwamba hakika Mtume ﷺ aliwaombea wengi kuingia peponi.

HADITHI YA ISHIRINI NA MBILI

Abu Daud amepokea kutoka kwa Jubair bin Muhammad bin Jubair bin Mat’am kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, amesema: Alikuwa bedui mmoja kwa Mtume ﷺ akasema: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu nafsi zimepigana jihadi, familia zimepotea, mali zimeteketea, na mifugo imeangamia, basi tuombee sisi kwa Mwenyezi Mungu mvua. Hakika sisi tunaomba utuombee kwa Mwenyezi Mungu, na tunamuomba Mwenyezi Mungu kupitia kwako.” Mtume ﷺ akasema: “Ole wako! Je, unajua ulisemalo?” Mtume ﷺ akamsabihi Mwenyezi Mungu, na akaendelea kumsabihi mpaka likajulikana hilo katika nyuso za Masahaba wake, kisha akasema: “Na ole wako kwani Mwenyezi Mungu haombwi kupitia kiumbe wake yeyote. Shani ya Mwenyezi Mungu ni adhimu zaidi kuliko hilo. Ole wako je, Mwenyezi Mungu ni nini? Hakika Arshi yake iko hivi juu ya mbingu Zake.” Akasema kwa vidole vyake: “Ni kama kuba, na hutoa sauti kutokana na Yeye kama sauti ya kipando kipya ambacho hutoa sauti kutokana na uzito wa mpandaji wake.”⁶⁹

⁶⁹ Imebuniwa na kuwekwa. Ameipokea Abu Daud Juz. 4, uk. 232 na 4726 na Twabarani katika kitabu *Al-Kabiir* Juz. 2 uk. 129 na 1547 na Baghawi katika kitabu *Sharhul-Sunnat* Juz. 1, uk. 176 /92.

Hafidh Mundhiri amenukuu kutoka kwa Hafidh Abu Bakri al-Bazar⁷⁰ kwamba hakika yeye amesema: “Hadithi hii hatujui ni wapi imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ zaidi ya hapa, na Muhammad bin Is’haq hakusema ndani yake: Amenihadithia.” Imekwisha.

Mundhiri amesema: “Muhammad bin Is’haq ni mchakachuaji, na mchakachuaji anaposema: ‘Kutoka kwa fulani’, bila kusema ‘ametuhadithia sisi’, au ‘tulimsikia’ au ‘alitupa habari’, basi hadithi yake si hoja, na hili ndilo aliloliashiria al-Bazar. Pamoja na hivyo hakika Ibn Is’haq anaposema kinaga ubaga kuwa amesikia, mahafidhi hutofautiana katika kuifanya hadithi yake kuwa ni hoja. Basi vipi ikiwa hakusema kinaga ubaga? Na hakika ameipokea hiyo Yahya bin Main na wengineo, na hawakutaja tamko ‘kutokana na Yeye’.” Mwisho wa maneno ya Mundhiri.

Yaani hawakusema katika hadithi yao kuwa “Hutoa sauti kutokana na Yeye kama sauti ya kipando kipya ambacho hutoa sauti kutokana na uzito wa mpandaji wake.” Bali wao wamesema: “Hutoa sauti kama sauti ya kipando kipya ambacho hutoa sauti kutokana na uzito wa mpandaji wake.” Na hakika Ibn Qaym katika *Sharhu Tahdhibus-Sunan*⁷¹ amerefusha maneno katika kumtetea Muhammad bin Is’haq, akijaribu kuizingatia hadithi hii kuwa ni sahihi, mpaka hakika ameunga mkono hadithi ya ukaaji iliyobuniwa na kuwekwa tuliyoiona huko nyuma kutoka katika njia ya Ibn Jarir. Na hakika ameileta hiyo kutokana na hadithi ya Hafidh Mutwin, na hadithi pamoja na jaribio la Ibn Qaym bado ni dhaifu yenye kuchukiza.

Na Hafidh Ibn Asakir ana juzuu iitwayo *Bayanul-Takhlitwi Fii Hadith Atwitwi*, hivyo hakuna mazingatio katika yale ambayo amerefusha Ibn Qaym. Na wakiwa wanahadithi wameweka sharti katika hadithi, ya kifungu cha sharia kuwa ili ikubalike ni lazima mpokezi

⁷⁰ Angalia kitabu *Musnadul-Bazar* Juz. 8, uk. 356.

⁷¹ Kimepigwa chapa pamoja na kitabu *Aunul-Ma’abuud* Juz. 13 uk. 11.

wake awe ni mkweli mwaminifu, basi hadithi ya itikadi inafaa zaidi sharti hilo kama alivyosema Dhahabi. Na Ibn Is’haq hata kama tutakubali ukweli na uaminifu wake, lakini haiwezekani kuwa hoja katika hadithi hii na mfano wake katika yale ambayo yanafungamana na sifa za Mwenyezi Mungu (s.w.t).


HADITHI YA ISHIRINI NA TATU

Bayhaqiy amesema: “Hii ni riwaya inayokomea kwa Abdullah bin Amru, na ameipokea mtu asiyekuwa na jina, nayo ni yenye kukatika, na hakika imenifikia kwamba Ibn Uyayna ameipokea kutoka kwa Hisham ibn Ur’wat kutoka kwa baba yake kutoka kwa Abdullah bin Amru. Ikiwa litasihi hilo, basi Abdullah bin Amru alikuwa akiangalia katika vitabu vya mwanzo. Basi yale ambayo hayavushi mpaka kwa Mtume ﷺ hutarajiwa kuwa ni miongoni mwa yale aliyoyaona yeye katika vitabu hivyo vilivyoangukia mikononi mwake.”

Ibn Jawzi amesema katika kitabu *Daf’u Shabhi Tashbiih*: “Kadhi Abu Ya’ali amethibitisha kwa riwaya hiyo dhiraa mbili na kifua kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), na hili ni baya, kwani hadithi sio yenye kunyanyuliwa wala haisihi. Na je, inajuzu aumbe kiumbe kutokana na dhati ya kale?! Na hili ni baya zaidi kuliko yale wanayoyadai manaswara. Na athari hii ya Abdullah bin Amru imechukuliwa kutokana na hadithi za Kiyahudi.”

HADITHI YA ISHIRINI NA NNE

Bayhaqiy amepokea katika kitabu *Al-Asmau Waswifat* kutoka katika njia ya Muhammad bin Is’haq kutoka kwa Abdul-Rahman bin Harith bin Abdullah bin Ayyash bin Abi Rabia, kutoka kwa Abdullah bin Abi Salama, amesema: Hakika Abdullah bin Umar bin Khwatwab alimtuma kwa Abdullah bin Abbas amuulize: “Je, Muham-

mad  alimuona Mola Wake Mlezi?” Akamtumia ujumbe Abdullah bin Abbas: “Ndio.” Abdullah bin Umar akamrudisha mjumbe wake akamuulize: “Alimuonaje?” Akamtumia ujumbe: “Hakika yeye alimuona katika kiwanja cha kijani kibichi, chini yake kuna tandiko⁷² kutokana na dhahabu, akiwa juu ya kiti chake cha dhahabu, na wamekibeba malaika wanne, malaika mwenye sura ya mwanaume, malaika mwenye sura ya ng’ombe, malaika mwenye sura ya mwewe, na malaika mwenye sura ya simba.”⁷³ Akaongeza Yunus katika hadithi yake: “Katika sura ya kijana.”

Bayhaqiy amesema: “Hadithi hii ameipokea peke yake Muhammad bin Is’haq bin Yasar, naye ni dhaifu katika anayopokea ikiwa hakubainisha usikiaji wake. Na katika hadithi hii kuna kukatika baina ya Ibn Abbas na mpokezi, yaani hakika ambaye aliyemtuma Ibn Umar kwa Ibn Abbas hajulikani, na hakuna chochote miongoni mwa matamshi haya katika hadithi sahihi kutoka kwa Ibn Abbas.” Bayhaqiy amesema: “Na imepokewa kwa upande mwingine dhaifu. Wameipokea hiyo kutoka katika njia ya Ibrahim bin Hakam bin Aban kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Akrama, kutoka kwa Ibn Abbas, kwamba hakika yeye aliulizwa je, alimuona Mola Wake Mlezi? Akasema: Ndio, alimuona yeye kama kwamba nyayo zake ziko juu ya sehemu ya kijani kibichi bila sitara. Ibrahim na baba yake ni watu madhaifu.” Imekwisha.

Nasema: Hadithi hii ni iliyokomea kwa Sahaba, na si ya kawaida, na ni yenye kuchukiza. Na inayokomea kwa Sahaba haitendewi kazi katika hukmu kama vile ilivyo katika elimu ya Misingi ya Sha-

⁷² Na inafaa kusemwa kuwa mpokezi anakusudia godoro ambalo anakalia mtu juu yake.

⁷³ Ni hadithi ya kubuniwa ya uongo. Ameipokea Abdullah bin Ahmad katika *As-Sunnat* Juz. 1, uk. 176 nambari 217 na Ibn Jawzi katika *Ilalul-Mutanahiyat*, Juz. 1 uk. 24 na Bayhaqi katika *Al-Asmau wa Sifaat*, uk. 443. Na hakika nimebainisha kwamba Nawawi (r.a) ametoa hoja kwa sehemu ya hadithi hiyo na akakosea. Nimebainisha huko katika kitabu changu cha *Ruuyat*.

ria. Inakuwaje katika jambo hili adhimu, ambalo linamfanya Mwenyezi Mungu ana mwili?! Na vipi inafaa katika akili ya mwenye akili, kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) awe katika uwanja ya kijani? Na nyayo Zake mbili juu ya sehemu ya kijani kibichi, naye yuko juu ya kiti cha enzi, kinachotokana na dhahabu, ambacho wanakibeba malaika wanne?! Mambo haya yenye kuchukiza yanautia kinyaa moyo wa Mwislamu, kwani hizo zinasigana na utukufu wa Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kuyarudisha hayo katika kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t): “Hakuna chochote kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.” (42:11).

Na mfano wake katika kuchukiza na ubatili ni ile riwaya aliyoipokea Bayhaqiy kutoka katika njia ya Abu Hamza Sukri, kutoka kwa Aamash kutoka kwa Salim bin Abi Juud, kutoka kwa Abdullah, kuhusu kauli ya Allah: “Na naapa kwa Alfajiri” (89:1), akasema: “Ameapa: Hakika Mola wako Mlezi yuko kwenye kuotea. (89:14), nyuma ya njia kuna madaraja matatu: Daraja moja juu yake kuna amana, na daraja jingine juu yake kuna Rahma, na daraja la tatu juu yake yupo Mola Mlezi aliyetukuka.”⁷⁴

Hii imekomea kwa Sahaba, na si ya kawaida, na ni yenye kuchukiza, na sanad yake ni dhaifu. Sukri ni mwenye kuchanganyikiwa, na Aamash ni mchakachuaji na ni mwingi wa kurefusha sadani, na vivyo hivyo Salim, pamoja na kuwa yeye hakukutana na Abdullah, na athari ya ubatili wake inajulikana kwa dharura, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

⁷⁴ Ni hadithi iliyobuniwa na kuwekwa ya uongo!! Na la kushangaza ni kwamba Hakim ameipokea katika kitabu *Mustadrak* Juz. 2, uk. 523 na akasema: Sanad yake ni sahihi na hawakuitoa hiyo wawili na akakiri Dhahabi juu ya hili!! Akasema: “Ni sahihi” Nayo ni kati ya zile tofauti za uongo!! Na ametukuka Mwenyezi Mungu kutokana na hilo mbali mno!! Na amelitaja Ibn Rajab katika kitabu kiiwacho *Kitabu Tahriif Minan-Naari* uk. 174 na vitabu vya Ibn Rajab katika *Targhiib wa Tarhiib* vina maajabu ya kuchukiza!!

HADITHI YA ISHIRINI NA TANO

Khatwib katika *Tarikh Baghdad* ameeleza kutoka katika njia ya Ahmad bin Muhammad bin Hajjaj Abi Bakri al-Maruziy, amesema: Alituhadithia Hasan bin Shuaib Ajuuri: Alitupa habari Abu Hamza Aslami Bitursus: Alitusimulia Waqii: Alituhadithia Abu Ismail, kutoka kwa Abu Is'haq, kutoka kwa Abdullah bin Khalifa, alisema: Mtume ﷺ amesema: “Al-Kursiyyu ni kiti ambacho anaketi juu yake Mola Mlezi (s.w.t), na haibaki sehemu ila upana wa vidole vinne anapoketi, nacho hutoa sauti kutokana na Yeye kama sauti ya kipando kipya ambacho hutoa sauti kutokana na uzito wa mpandaji wake.”⁷⁵

Amesema Abu Bakri al-Maruziy: Abu Ali Husein ibn Shabib aliniambia: Abu Bakri bin Salim Abid aliniambia wakati tulipokwenda Baghdad: Hadithi hiyo tuliyoandika aliitoka kutoka kwa Abu Hamza, hivyo Abu Bakri bin Salam akaiandika kwa hati yake, na tukaisikia sote, na Abu Bakri bin Salam akasema: Hakika sehemu inayobaki ni ya Muhammad ﷺ, atamketisha hapo.⁷⁶ Hadithi hii ni ya kuvushwa, haina sanadi yote, (mursal), Abdullah bin Khalifa ni Tabiina, na Abu Is'haq ni mchakachuaji, na hakika amechomeka wapokezi wa uwongo. Na imepatikana kwa njia nyingine wenye kuungwa kutoka kwa Abdullah bin Khalifa kutoka kwa Umar kwa sanad iliyo dhaifu.

Nayo ni hadithi isiyo ya kawaida, yenye kuchukiza, isiyoingia akilini, na Hafidh Ibn Asakir ana juzuu iitwayo *Bayanul-Takhliitwi Fii Hadith Atwitwi*, na hadithi hii ipo wazi kabisa katika kumfanya

⁷⁵ Imebuniwa na kuwekwa nayo imejirudia kutoka katika hadithi iliyotangulia nambari 21. Imetajwa katika *Tariikh Baghdad* Juz. 8, uk. 52 na Ibn Jawzi katika *Ilalu-Mutanaahiyya* Juz. 1 uk. 20 na Ibn Abu Aswim katika *as-Sunnat* Juz. 1, uk. 252/574 na wengineo kutoka kwa Umar, na Abdullah bin Khalifa hajulikani hali yake.

⁷⁶ Hawa wawili ni maimamu wapotofu. Ametukuka Mwenyezi Mungu kutokana na uzushi wao hao wawili mbali mno, na ametukuka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kutokana na yale ambayo wanaenda nayo hao!!

Mwenyezi Mungu ana mwili pale iliponasibisha kwa Mwenyezi Mungu kuwa ameketi juu ya kiti, na kwamba inabakia sehemu katika kiti ambayo ataketi juu yake Mtume ﷺ. Na huenda Mayahudi waliingiza hadithi hii ndani ya vitabu vya baadhi ya Waislamu, na Waislamu hawakujua kuwa hilo ni fitina, kwani yaliyomo ndani yake ya kumfanya Mwenyezi Mungu ana mwili, hayo hakika ni itikadi ya Mayahudi. Na la kushangaza ni kutoka kwa Ibn Qayyim alipounga mkono ukaaji wa Mtume ﷺ juu ya kiti cha enzi au juu ya Arshi pembezoni mwa Mwenyezi Mungu (s.w.t). Amelitaja hilo katika kitabu *Badaiul-Fawaid* na akatoa ushahidi kwa beti kadhaa za mashairi zilizonasibishwa kwa Daar Qutni. Imekuja kama ifuatavyo:

“Wala msikanushe kwamba Yeye si mkaaji.
Wala msikanushe kwamba hatamkalisha yeye.”

Pamoja na kuwa sanad ya Daar Qutni sio sahihi. Na hakika nimet-anabahisha juu ya hilo katika juzuu *Raf’ul-Ishkaal*, au *Mas’alatul-Muhaal*. Na la kushangaza zaidi kutokana na hili, na lililo geni zaidi ni kwamba Ibn Qayyim ameandika kitabu alichokiita *Fawaidul-Mashuqah Ilaa Ulumil-Qur’ani Wailmil-Bayan*, ndani yake amezungumzia aina za majazi na istiara na yasiyokuwa hayo miongoni mwa yale ambayo yamethibiti katika elimu ya Bayan. Na ametaja mifano mingi kutoka katika Qur’ani tukufu, kisha alipoandika kitabu *Swawaiqul-Mursalat Alaa Juhmiyyat wal-Muatwalat* akamfuata Sheikh wake katika ukanushaji wake wa aina zote za majazi,⁷⁷ na akadai hakika majazi ni bidaa (uzushi) na wala halikuwa maarufu kwa watu wa kale.

⁷⁷ Pamoja na kuwa Ibn Taymiyya anasigana kuhusu suala la Majazi, lakini amethibitisha hilo katika mahala alipodharurika yeye na akaiieleza hiyo, na hii ni kauli yake katika kitabu *Majmuul-Fataawa* Juz. 7 uk. 577: [Na haya ni sehemu ya imani, na hakika inajulisha kwa kwenda sambamba ya kwanza kwa jina la majazi] na kauli yake katika kitabu *Majmuul-Fataawa* Juz. 12, uk. 553: [Na ama kauli ya msemaji je, maneno ya Mwenyezi Mungu yanakuwa majazi? Basi inasemwa: Alama ya Majazi ni kusihhi kwa kumuepusha Yeye....]!! Na nyinginezo nyingi mno!!

Na hakika wa kwanza kuzungumza hilo na kulidhihirisha hilo ni Abu Ubaida, na akakosea katika hilo kosa kubwa. Hakika majazi inajulikana katika lugha ya Kiarabu tangu Mwenyezi Mungu alipoumba Kiarabu, na Qur’ani imesheheni aina mbalimbali za majazi. Kuna uhusiano gani baina ya lugha na Bidaa, na je, limepatikana andiko kutoka kwa mtoasharia akibainisha kwamba hakika haifai kutumia maneno katika majazi na aina zake za mitindo ya kilugha hata tupokee sharia hiyo kutoka kwa watu wa kale? Na lengo la Ibn Qayyim na Sheikh wake katika madai haya ni kutaka kuhalalisha kutafsiri matamshi yenye kuhusiana na sifa za Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa uhakika wake wa kilugha, maneno mfano wa ‘kuenea’, ‘mkono’, ‘unyayo’, na mfano wa hayo, na huku ni kuzama katika kuthibitisha mpaka katika kiwango cha kumshabihisha na kumfananaisha Mungu na viumbe, na kumfanya ni mwili. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

HADITHI YA ISHIRINI NA SITA

Imethibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Anas bin Malik kwamba amesema: Mtume ﷺ alisema: “Hakutumwa Nabii ila aliuonya umma wake kuhusiana na chongo na muongo, kwani yeye (Ibilisi) ni chongo na Mola Wenu sio chongo, na baina ya macho yake mawili Ibilisi kumeandikwa neno kafiri.”⁷⁸ Na ameipokea Harawi katika kitabu chake *Arbaiina* na ameandika kwa anwani: “Mlango wa kuthibitisha macho mawili ya Yeye aliyetukuka na kutakasika.”

Na hadithi haihusiani na kuthibitisha macho mawili ya Mwenyezi Mungu. Ni kutoka wapi Harawi ameyaleta hayo macho mawili,

⁷⁸ Hadithi hii haijathibiti kwetu sisi. Na ameipokea *Bukhari* 7131 na 7408 na *Muslim* 2933 kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه, na wameipokea pia kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه, na hao ni miongoni mwa wale waliopokea kutoka kwa Kaab Akhbar. Na hii ni miongoni mwa zile za Kiyahudi, na hakika hadithi ya Muslim imebainisha kuwa hii inatokana na hadithi ya Ibn Swayad!!

ikiwa kauli yake: “Hakika Mola Wenu sio chongo” inalazimu awe na macho mawili, basi hili ni kosa la wazi. Hakika sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) haithibiti isipokuwa kwa tamshi la wazi kutoka katika hadithi sahihi. Na hakika imekuja ndani ya Qur’ani uthibitisho⁷⁹ wa jicho moja kwa Mwenyezi Mungu, kama vile kauli yake (s.w.t): “machoni Mwangu” (Sura Twaha: 39), na wa macho mengi, kwa kauli Yake (s.w.t): “Macho Yetu” (Sura Tuur: 48), na “Na macho Yetu” (Sura Huud: 37), na “Macho Yetu” (Sura Qamar: 14).

Na hili linathibitisha kwamba unasibishaji wa jicho kwa Mwenyezi Mungu maana yake ni sifa ya uoni au usikivu na uzungumzaji. Na amesema Ibn Hazm:⁸⁰ “Haifai kwa yeyote amsifu Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwa ana macho mawili kwani andiko halijakuja hivyo.” Na jambo hili ni kawaida ya Harawi katika kitabu *Arbaiina*. Anathibitisha sifa kwa Mwenyezi Mungu bila dalili.

HADITHI YA ISHIRINI NA SABA

Kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه, amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amefaradhisha Swala kupitia ulimi wa Nabii wenu ﷺ kwa msafiri rakaa mbili na kwa mkazi rakaa nne, na kwa mwenye khofu rakaa moja.” Ameipokea Muslim katika *Sahih* yake.⁸¹ **Tunasema:**

1. Hakika Mtume ﷺ hakuwali katika hofu rakaa moja katu, na lau ingelikuwa ni wajibu asingeliacha.
2. Hakika kuhusu Swala ya hofu zimesihi aina mbalimbali za riwaya, kati ya hizo ni kwamba Mtume ﷺ aliswalisha kundi rakaa mbili na akatoa salamu kabla yake, na likaja kundi

⁷⁹ Sayyid (Mwenyezi Mungu anyanyue daraja lake) anakusudia kwa kauli yake (uthibitisho): “utajo” na hili umetangulia usemaji wake. Na naye hasemi kwa uthibitisho kabisa na hili linajulikana kutokana na kauli yake!

⁸⁰ Kitabu *Al-Faswlu Fi Milal wa Nihal* Juz. 2, uk. 128.

⁸¹ *Sahih Muslim* 687.

lingine akaliswalisha rakaa mbili na akatoa salamu, basi zikawa ni rakaa nne kwa makundi mawili, rakaa mbili mbili.

Na hili linapinga kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه iliyosema kuwa Mwenyezi Mungu amefaradhisha Swala kwa msafiri rakaa mbili. Na nyingine ni kwamba aliswalisha kundi moja rakaa mbili na akatoa salamu na likaja kundi lingine basi akaliswalisha rakaa mbili na akatoa salamu. Na hili linajulisha juu ya kusihifuataji wenye kujaaliwa ruhusa ambapo ni tofauti na Maliki. Na nyingine ni kwamba aliswalisha kundi rakaa moja na akahitimisha kwa rakaa moja na akaswalisha lingine rakaa moja na akatoa salamu, na akahitimisha yeye mwenyewe rakaa moja, na lau ingekuwa inasihifu Swala ya khoufu kwa rakaa moja basi aina hizi zilizotajwa zisingesihifu.

3. Hakika wanazuoni wameafikiana juu ya kufaa aina hizi na zinginezo katika Swala ya hofu kwa kuwa ni sahihi. Na lau kama ingelikuwa ni rakaa moja zisingelisihifu nyinginezo.
4. Amepokea Nasai kwamba hakika Masahaba waliswali Swala ya hofu kwa rakaa moja katika baadhi ya hali. Na hili ni dalili ya wazi zaidi juu ya kwamba hiyo sio faradhi, na kama ingelikuwa ni faradhi wasingeliiacha abadani.

HADITHI YA ISHIRINI NA NANE

Amepokea Muslim kutoka katika njia ya Twaus, kwamba Abu Swahbau alisema kumwambia Ibn Abbas رضي الله عنه: “Lete habari zako za kushangaza, hivi katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na zama za Abu Bakr رضي الله عنه talaka tatu hazikuwa talaka moja?” Akasema: “Ndiyo ilikuwa hivyo lakini ilipofika zama za Umar رضي الله عنه ilijitokeza tabia ya watu kufuatanisha katika talaka ndipo akairidhia dhidi yao (yaani kwa kuwadhuru wao wenyewe).”⁸²

⁸² Si ya kawaida!! Ameipokea Muslim 1472 na Ibn Abi Shayba Juz. 4, uk. 69 na Bayhaqi

Ahmad bin Hanbali na wengineo miongoni mwa maimamu wamesema kuwa hadithi hii si ya kawaida na ni yenye kuachwa, kama alivyonukuu hilo Hafidh Ibn Rajab katika kitabu *Sharhu Ilal Tirmidhiy*. Na Ahmad akasema katika barua aliyompelekea Musadad katika *Al-Muutaqidu Wafi Sunnat wal-Jamaa*, hili ndio andiko lake: “Na *Mut’ah* ni haramu hadi Siku ya Kiyama. Na atakayetaliki talaka tatu katika tamko moja, hakika atakuwa amefanya ujinga, na mkewe atakuwa ni haramu juu yake, wala hawi halali kwake milele mpaka aolewe na mume mwingine.” Imekwisha.

Na kati ya yale yanayochukiza kuhusiana na hadithi hii ni kauli ya Abu Swahbau kwa Ibn Abbas رحمته الله: “Lete habari zako za kushangaza”, vipi Abu Swahbau amwambie Sheikh wake Ibn Abbas رحمته الله kwa ibara yenye kuchukiza kama hii na Ibn Abbas anyamaze? Na ibara hii inajulisha kwamba kuzingatia talaka tatu kuwa ni moja ni kati ya mambo yenye kuchukiza zaidi yaliyopokewa na Ibn Abbas رحمته الله.

Na Ibn Hazm katika kitabu *Muhalliy*⁸³ amesema: “Na ama hadithi ya Twaus kutoka kwa Ibn Abbas رحمته الله ambayo imetaja kwamba talaka tatu zilikuwa ni moja na huzingatiwa kuwa ni moja na hufanywa kuwa ni moja, haina kitu chochote kinachoonesha kuwa hakika yeye رحمته الله ndiye aliyefanya kuwa ni moja au aliyeirudisha hadi kuwa moja, wala haioneshi kuwa yeye رحمته الله alijua hilo na akalipitisha. Wala hakuna hoja ila katika yale yaliyosihhi kwamba yeye رحمته الله aliyasema au aliyatenda au aliyajua na hakuyakataza.” Imekwisha.

Na ametoa dalili Ibn Hazm kwa hadithi ya Awaymar Ajalani pamoja na mkewe ambaye alimlaani, kuthibitisha kuwa zinasihhi talaka tatu kwa mkupuo mmoja, ambapo mwishoni mwa hadithi hiyo kuna maelezo: Alisema: “Nitakuwa nimemuongopea ewe Mtume wa

katika *Sunanul-Kubra* Juz. 7, uk. 336.

⁸³ Kitabu *Muhalliy*, Juz. 10, uk. 168.

Mwenyezi Mungu, ikiwa nitaendelea kumshikilia.” Basi akamtaliki talaka tatu kabla Mtume ﷺ hajamwamrisha.

Na kwa hadithi ya Bukhari kutoka kwa Bibi Aisha ni kwamba Bibi Aisha alisema: “Hakika mtu mmoja alimtaliki mkewe talaka tatu basi akaolewa na mume mwingine na kisha naye akamtaliki. Basi Mtume ﷺ akaulizwa je, ni halali kwa yule wa kwanza? Akasema: “Hapana, mpaka aonje unyumba wake kama alivyoonya wa kwanza.”⁸⁴ Na yale yaliyothibiti kutoka kwa Umar na Ali na Uthman na Ibn Abbas na Ibn Mas’ud ni kwamba hakika wao walisema: Hakika talaka tatu iliyokusanywa katika neno moja inamlazimu mume kwamba mkewe huyo anakuwa haramu kwake milele mpaka aolewe na mume mwingine. Na ijapokuwa hadithi si ya kawaida, lakini bado mahakama za Misri na Moroko wanaitendea kazi mpaka leo wakimfuata Ibn Taymiya ambaye amekwenda kinyume na wanazuoni katika maswala mengi.

HADITHI YA ISHIRINI NA TISA

Abu Daud na Ibn Majah wamepokea kutoka kwa Ibn Maktum رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kwamba alimwambia Mtume ﷺ: “Hakika mimi ni mwanaume mlemavu wa macho na nyumba yangu iko mbali, na mimi ninaye kiongozi ambaye haendani na mimi, je, ninaruhusiwa kuswali nyumbani kwangu?” Akamuuliza: “Je, unasikia wito (adhana)?” Akajibu: “Ndio.” Akasema: “Sikuruhusu.”⁸⁵ Ameipokea Muslim na Nasai kutoka kwa Abu Huraira, kwamba amesema: “Mtume ﷺ alijiwa na mlemavu wa macho,” basi akataja hadithi hii.⁸⁶ Hadithi hii si ya kawaida, na amenukuu Hafidh Ibn Rajab katika kitabu *Sharhu Ilal Tirmidhiy* kutoka kwa baadhi yao kwamba hakika hajulikani yeyote aliyechukua madhumuni ya hadithi hii.

⁸⁴ Ameipokea *Bukhari* 5261 na *Muslim* 1433 kwa ufupi.

⁸⁵ Ameipokea *Abu Daud* 552 na *Ibn Majah* 792.

⁸⁶ Ameipokea *Muslim* 653 na *Nasaai* 850.

Nasema: Na miongoni mwa yale ambayo yanajulisha kuwa si hadithi ya kawaida ni ile hadithi ya Itban bin Malik. Hakika yeye alikuja kwa Mtume ﷺ akasema: “Ewe Mtume hakika mimi nimechukua uoni wangu na mimi ninawaswalisha kaumu yangu, na mvua inapofurika na kujaa bonde lililopo kati yangu na wao huwa siwezi kwenda msikitini kwao kuwaswalisha. Ewe Mtume, ninapenda uje uswalie katika mswala nitakaoufanya kuwa mswala wangu.” Mtume ﷺ akasema: “Inshaallah nitafanya hivyo.”⁸⁷ Ameipokea *Muslim* na wengineo.

Katika hadithi hii kuna ruhusa ya kutofautiana na jamaa kwa udhuru, nayo ni Ijmaai, na wamesema baadhi yao: Hakika kutomruhusu kwake Ibn Maktum رضى الله عنه ni kwa kuwa yeye alikuwa akiswalia katika msikiti wa Mtume ﷺ, na msikiti huu ni mahsusi ambao inazuiliwa kuacha jamaa humo, kwa kuwa hakika Mtume ﷺ alikuwa akihudhuria jamaa hiyo na yeye ndiye aliyekuwa akiwaswalisha jamaa hiyo.

HADITHI YA THELATHINI

Ameipokea Abu Daud⁸⁸ kutoka kwa Ammar bin Yasir رضى الله عنه, kwamba yeye alikuwa anahadithia kwamba wao wakiwa pamoja na Mtume ﷺ walitumia udongo kwa ajili ya Swala ya Alfajri, basi wakapiga kwa viganja vyao udongo, kisha wakapaka nyuso zao mara moja, kisha wakarudia wakapiga kwa viganja vyao udongo kwa mara nyingine basi wakapaka kwa mikono yao yote hadi kwenye makwapa, kwa kuanzia kwenye vitanga vyao.

Ibn Rajab ameihesabu hadithi hii kuwa ni miongoni mwa hadithi zisizokuwa za kawaida, nayo ni hadithi yenye kuchanganya. Shafi amesema: “Alisema Ammar: ‘Tulifanya tayammamu pamoja

⁸⁷ Ameipokea *Bukhari* 425 na lafudhi yake, na *Muslim* 33 kwa lafudhi inayokaribiana nayo.

⁸⁸ *Sunan Abi Daud*, hadithi ya 318.

na Mtume ﷺ mpaka katika vifundo.’ Na amepokea yeye kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alipaka uso na viganja viwili, basi ikawa kauli yake tulifanya tayamamu pamoja na Mtume ﷺ, haikuwa ni kutokana na amri ya Mtume ﷺ.”

Na akasema mwanahadithi Muhammad bin Is’haq Dahlawi: “Huu ni ulinganishaji wa masahaba katika mwanzo wa jambo, kabla ya kubainisha Mtume ﷺ, na pindi alipolibainisha hilo walijua namna ya kutayamamu.”

HADITHI YA THELATHINI NA MOJA

Bayhaqiy katika kitabu *Al-Asmau Waswifat* amepokea kutoka katika njia ya Nasai, kwamba amesema: Ametuhadithia Amru bin Yazid: Ametuhadithia Saif bin Ubaidullah na alikuwa mkweli, kutoka kwa Salama bin Ayaal, kutoka kwa Said bin Abdul-Aziz, kutoka kwa Zahari, kutoka kwa Said bin Masayyab, kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه, amesema: “Tulisema: Ewe Mtume! Je, tutamuona Mola Wetu Mlezi? Akasema: ‘Je, unaliona jua siku ambayo hakuna mawingu? Na unauona mwezi usiku ambao hakuna mawingu?’ Tukasema: Ndio, akasema: ‘Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu Mlezi, mpaka mmoja wenu atamkaribia zaidi, basi atasema kumwambia yeye: Mja Wangu je, unajua dhambi fulani na fulani? Atasema: Ewe Mola Wangu hujanisamehe mimi? Basi atasema: Kwa msamaha Wangu umefika hapa.”⁸⁹

⁸⁹ Ni batili yenye kurudishwa. Nayo ni moja ya hadithi ya sura iliyo ndefu mashuhuri!! Ameipokea hii kwa lafudhi ya Ibn Abi Aswim k kitabu *As-Sunna* Juz. 1, uk. 259 na Twabarani katika *Muujam Awsat* Juz. 2, uk. 194 na akaiona ni dhaifu mpinzani wa zama katika utoaji maelezo yake juu ya *Sunnan* ya Ibn Abi Aswim. Na hadithi ameipokea Ibn Haban katika *Sahih* yake Juz. 16, uk. 467 hadithi ya 7438 na ikapatikana yenye kudhibitiwa huko hivi: (Wala haibaki sehemu katika kikao hicho ila atakuwepo Mwenyezi Mungu). Na imepatikana kama ilivyotangulia kwa Twabarani na Ibn Abi Aswim kwa lafudhi (upande) na kwa *Tirmidhiy* hadithi ya 2549 kwa lafudhi (Mwenyezi Mungu kamsogelea upande wake) nayo inatokana na hadithi ya Abu Huraira na Abu Said, na hao wawili ni miongoni mwa wale wanaopokea kutoka kwa Kaab Akhbar na ni kutoka kwake umekuja msiba huu!!

Bayhaqiy⁹⁰ amesema: “Hadithi ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu hakika ameipokea mwingine kutoka kwa Zahari kutoka kwa Said bin Musayyab, na Atwau bin Yazid kutoka kwa Abu Huraira, hakuna ndani yake tamko: “mpaka mmoja wenu atamkaribia zaidi,” na Salama bin Ayaar na Saif bin Ubaidullah hawakuwa wanatajwa katika vitabu sahihi. Na mfano wa hii haithibitishi kuonekana kwa Mola Manani.”

Nasema: Tamko “mpaka mmoja wenu atamkaribia zaidi,” si la kawaida na ni lenye kuchukiza, halikuja ila katika njia hii, nayo ni yenye kurudishwa, kwani inapingana na utukufu wa Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Na wanazuoni wamesema kinaga ubaga kwamba yale yanayofungamana na sifa ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) hayakubaliki ila kwa hadithi sahihi mkataa. Na hakika Bayhaqiy ameitafsiri hadithi hii kwa maana ya kwamba atakuwa karibu zaidi na malaika au na neema ya Mwenyezi Mungu, nayo ni maana ya mbali, na ukweli ni kwamba neno hilo ni kutokana na hadithi isiyokubalika.

HADITHI YA THELATHINI NA MBILI

Amesema Ibn Abu Hatam katika *Tafsiiir* yake: Ametuhadithia Ali bin Husein: Ametuhadithia Shayban: Ametuhadithia Masrur bin Tamimi: Ametuhadithia Abdul-Rahman bin Amru Awzai, kutoka kwa Ur'wat bin Ruwaim, kutoka kwa Ali bin Abu Twalib عليه السلام, amesema: Mtume ﷺ amesema: “Itukuzeni mitende, hiyo ni shangazi zenu, kwani imeumbwa (mitende) kutokana na mabaki ya udongo alioumbiwa Adam عليه السلام, na katika miti hakuna chochote kinachopandishwa isipokuwa wenyewe.”⁹¹

⁹⁰ Katika kitabu *Asmaau wa Sifaat*, uk. 460.

⁹¹ Hadithi iliyobuniwa. Ameipokea Abu Ya'ali katika *Musnad* wake Juz. 1, Juz. 353/455 na Abu Nuaim katika *Hilyat* Juz. 6 uk. 123 na Ramihri Muzzi katika *Amthalul-Hadithi* uk. 73, na Daaylami katika *Musnadul-Firdaus* Juz. 1, uk. 68 katika sanad yake yuko Ur-wat bin Ruwaim anbay hakumdiriki bwana wetu Ali عليه السلام, na Masruur bin Said ni miongoni mwa watu madhaifu. Na ameitaja hiyo Haythami katika *Majmaul-Zawaid* Juz. 5, uk. 89 na akasema: “Ameipokea Abu Ya'ali na ndani yake yupo Masruri bin Said Tayamimi naye ni dhaifu.”

– Ibn Kathir amesema: Hadithi hii ni yenye kuchukiza mno.

Nasema: Katika sanad yake yupo Masrur bin Said. Ibn Haban amesema: “Hupokea kutoka kwa Awzai hadithi nyingi zenye kuchukiza.” Na Aqili⁹² amesema: “Hadithi yake sio yenye kuhifadhika, hajulikani ila kwayo.” Yaani hadithi hii tuliyoitaja.

Hadithi hii ni yenye kuchukiza mno kama alivyosema Ibn Kathir, na wala siwi mbali kusema ni ya kubuniwa na kuzushwa, kwa sababu Mtume ﷺ haiwezekani aufanye mtende kuwa ni shangazi yetu. Na ndani yake kuna mambo yasiyofaa pia, kuwa huo umeumbwa kutokana na udongo wa Adam, na maana yake ni kwamba hakika Mwenyezi Mungu pindi alipokadiria udongo ambao alimuambia Adam ﷺ, ukadirio wake haukulingana na Adam ﷺ, bali yalibakia mabaki yaliyotumika kuumba mtende. Na wala haifai kulinasibisha hili kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), kwani yeye anajua makadirio ya vitu kwa mipaka. Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi zaidi.

HADITHI YA THELATHINI NA TATU

Ahmad katika *Musnad* yake⁹³ amesema: Ametuhadithia Muhammad bin Abdullah bin Zubair, amesema: Ametusimulia Israili bin Sammak, kutoka kwa Alqamah bin Wail, kutoka kwa baba yake amesema: Alitoka mwanamke mmoja kwenda kuswali, basi akakutana na mwanaume. Mwanamume yule akamfunika huyo mwanamke kwa nguo zake na kisha akakidhi haja yake na kwenda zake. Mwanamume mwingine akamkuta bibi yule, na bibi akamwambia: hakika kuna mwanamume amenifanya hivi na vile. Mwanamume yule aka-

⁹² Kitabu *Dhuaaful-Aqiili* Juz. 4, uk. 256.

⁹³ Ni dhaifu. *Musnad Ahmad* Juz. 6, uk. 399 na *Tirmidhiy*, hadith ya 1454 na *Abu Daud*, hadith ya 4379 na katika sanad yake yupo Sammak bin Harb na Aqrama bin Wail bin Hajar, na ndani yao hao wawili upo udhaifu. Na anayo sanad nyingine anaipokea Hajjaj ibn Artwaat kutoka kwa Abdul-Jabbar bin Wail kutoka kwa baba yake, nayo ni yenye kukatika, ameipokea *Tirmidhiy* namba 1453 na *Ibn Majah* 2598.

toka mbio kwenda kumtafuta. Na mara watu miongoni mwa Answar wakamkuta bibi yule, akawaambia wao kwamba hakika mwanaume mmoja amenifanyia mimi hivi na vile.

Basi na wao wakaenda kumtafuta yule mtu. Na mara kundi lile la Answar likaja na yule mwanaume aliyekwenda kumtafuta yule aliyemfanyia tendo baya bibi yule, wakaenda naye hadi kwa Mtume عليه السلام, (mwanamke) alipoulizwa akasema: ‘Ni huyu.’ Na pindi Mtume عليه السلام alipoamrisha kupigwa mawe, akaibuka yule aliyemfanyia tendo baya bibi yule na kusema: ‘Ewe Mtume, mimi ndiye niliyetenda.’ Mtume عليه السلام akamwambia yule mwanamke: ‘Nenda zako, hakika Mwenyezi Mungu ameshakusamehe wewe.’ Na akasema kauli nzuri kumwambia yule mwanaume. Pakasemwa: ‘Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu je, humpigi mawe?!’ Akasema: ‘Hakika ametubia toba ya hakika lau wangelitubia watu wa Madina toba hiyo wangekubaliwa.’”

Hadithi hii ni miongoni mwa hadithi sizokuwa za kawaida kwani inakwenda kinyume na yale waliyoafikiana wanazuoni, kwamba adhabu ya sharia ikiwa itamfikia Imam basi ni lazima kuitekeleza, kama ilivyokuja katika hadithi nyingine. Na katika kitabu *Sunan Abi Daud* na *Nasaai* kutoka katika njia ya Amru bin Shuaib, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake; hakika Mtume عليه السلام amesema: “Ondoeni adhabu kati yenu, na yale yatakayonifikia mimi yaliyo na adhabu itakuwa ni wajibu.”⁹⁴ Nayo inafaidisha kwamba Imam haifai kwake kusamehe adhabu pindi itakapomfikia.

Na katika *Sahih Bukhari* imepokewa kutoka kwa Aisha, kwamba hakika Usama bin Zaid عليه السلام alimsemesha Mtume عليه السلام kuhusiana na mwanamke wa kabila la Bani Makhzum ambaye aliiba. Mtume عليه السلام akamwambia: “Je, unataka uombezi katika adhabu ya sharia ya Mwenyezi Mungu?”⁹⁵

⁹⁴ Ameipokea *Nasaai* 4886 na *Abu Daud* 4376 na wengineo wasiokuwa hao wawili nayo ni hadithi ambayo sanad yake ni nzuri.

⁹⁵ Ameipokea *Bukhari* 3475 na 6788 na *Muslim* 1688.

Lakini amepokea *Abu Daud*⁹⁶ kwa fuo la maneno linalodhihirisha kuwa hakika hadithi hii ni ya kawaida, akasema: Ametuhadithia Muhammad bin Yahya bin Faris: Ametusimulia Faryabi: Ametuhadithia Israili: Ametusimulia Sammak bin Harb, kutoka kwa Akrama bin Wail, kutoka kwa baba yake: Hakika mwanamke mmoja katika zama za Mtume ﷺ alitoka kwenda kuswali, basi akakutana na mwanaume akamfunika na kukidhi haja zake. Mwanamke akapiga ukelele na mwanamume akenda zake. Mara akapita mtu, mwanamke akasema: ‘Hakika yule amenifanyia mimi hivi na vile.’ Na mara likapita kundi la Muhajirina, mwanamke yule akawaambia: ‘Hakika yule amenifanyia mimi hivi na vile.’ Basi wakaenda zao wakamchukua mwanaume ambaye walidhani kwamba ndiye alimtendea vibaya yeye, na wakaja naye kwake, akasema: ‘Ndio, ndiye huyu’, wakamleta kwa Mtume ﷺ, na alipoamrisha yeye apigwe mawe, mara akasimama yule mhusika aliyemfanyia tendo baya, akasema:

‘Ewe Mtume mimi ni mhusika niliyemtendea ubaya mwanamke’, Mtume akasema kumwambia yeye: ‘Nenda zako hakika Mwenyezi Mungu amekusamehe wewe.’ Na akasema kauli nzuri kumwambia yule mwanaume. Akasema Abu Daud: Yaani mwanaume aliyechukuliwa, na akasema kumwambia yule mhusika ambaye alimfanyia tendo baya mwanamke: ‘Mpigeni mawe.’ Akasema: ‘Hakika ametubia toba ambayo lau watatubia watu wa Madina watakubaliwa.’ Abu Daud ameandika chini ya anwani: “Mlango unaohusu mtu anayestahiki adhabu ya sharia anayekuja na kukiri kosa.” Na hadithi yake iko wazi, imeondoa mishkili yote iliyokuwepo katika hadithi ya Ahmad.

⁹⁶ *Sunan Abi Daud* 4379.

HADITHI YA THELATHINI NA NNE

Amesema Abdul-Razzaq katika *Muswanaf*:⁹⁷ Amesema: Ametupa habari Muammar na Thawri kutoka kwa Abu Is’haq Sabiiy, kuhusu mwanamke wake, kwamba aliingia kwa Aisha akiwa na wanawake, basi yule mwanamke akamuuliza Aisha: “Ewe mama wa Waumini, nilikuwa na kijakazi nikamuuza kwa Atwai kwa thamani ya mia nane, kutoka katika milki ya Zayd bin Arqam, kisha nikamnunua kwa thamani ya mia sita kutoka katika milki ya Atwai, basi nikampatia mia sita na nikaandika juu yake mia nane.” Aisha akasema: “Ni kibaya alichonunua na alichonunua Zaid bin Arqam, kwani amebatilisha jihadi yale aliyoifanya pamoja na Mtume ﷺ isipokuwa kama atatubu.” Mwanamke yule akasema kumwambia Aisha: “Je, ikiwa nitachukua mtaji wangu na nikamrudishia yeye ziada, itakuwa ni bora?” Akasema: “Na aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola Wake, akakoma, basi yake ni yaliyokwisha” (2:275).

Na ameipokea Daar Qutni na Bayhaqiy⁹⁸ katika *Sunan* yake kutoka kwa Yunus bin Abi Is’haq kutoka kwa mama yake Aliyat, amesema: “Nilikuwa nimekaa kwa Aisha, basi akajiwa na Ummu Muhibbat akasema: Hakika mimi nilimuuzia Zaid bin Arqam kijakazi.” Akataja hadithi mfano wa hiyo.

Na akasema Ahmad: Ametuhadithia Muhammad bin Ja’far: Ametusimulia Shuubat kutoka kwa Abu Is’haq Sabiiy kuhusu mwanamke wake, kwamba aliingia kwa Aisha yeye na Ummu Walad Zaid bin Arqam, akasema Ummu Walad Zaid kumwambia Aisha: Hakika mimi niliuzia kutoka kwa Zaid kijana kwa thamani ya Dirham mia nane kwa malipo ya baadaye. Akataja hadithi mfano wa hiyo.

⁹⁷ *Muswanaf*, Juz. 8 uk. 185.

⁹⁸ *Sunan Daar Qutni* Juz. 3 uk. 52 na *Sunan Bayhaqi* Juz. 5 uk. 330.

Akasema Daar Qutni:⁹⁹ “Aliyat na Ummu Muhibba hawajulikani, kwa hivyo wao si hoja, na hadithi hii haijathibiti kutoka kwa Aisha, amesema hilo Imam Shafi.”

Na amesema Ibn Abdul-Barr katika kitabu *Istidhkar*: “Habari hii hawaithibitishi watu wa elimu kuwa ni hadithi, wala si kati ya zile wanazozitolea dalili na hoja. Basi mwanamke wa Abu Is’haq na mwanamke wa Abu Safar na Ummu Walad wa Zaid bin Arqam wote hawajulikani kwa sifa ya kubeba elimu.”

Na ni kwa mfano wa watu hawa amepokea Shuuba kutoka kwa Abu Hashim kwamba yeye amesema: Walikuwa wakichukua kuchukua hadithi kutoka kwa wanawake ila kutoka kwa wake wa Mtume ﷺ, amesema: “Na hadithi ni yenye kuchukiza, haina asili, kwa sababu matendo mema hayabatilishwi kwa ijtitihadi, bali yanaporomosha kwa kuritadi. Na ni muhali Aisha kumlazimisha Zaid kutubia kwa rai yake, na kumkufurisha yeye kwa ijtitihad yake, hili halifai kumdhania Aisha, wala halikubaliki juu yake.”

Na vivyo hivyo Ibn Hazm ameibatilisha kwa namna kama hii au iliyo nzuri zaidi. Angalia kitabu *Muhalliy*, Juz. 9, uk. 49-50. Basi habari ni batili hata kama Ibn Jawzi na baadhi ya Mahanafi wenye kughafilika na maana yake yenye kuchukiza wataizingatia kuwa ni sahihi. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

HADITHI YA THELATHINI NA TANO

Abu Daud na Nasai na Ibn Majah wamepokea kutoka katika njia ya Amru bin Shuaib kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, amesema: Hakika mtu mmoja alikwenda kwa Mtume 3 akasema: Ewe Mtume, ni ipi namna ya kujitoharisha? Basi Mtume akaomba aletewe maji katika chombo akaosha viganja vyake viwili mara tatu,

⁹⁹ *Sunan Daar Qutni*, Juz. 3, uk. 52.

kisha akaosha uso wake mara tatu, kisha akaosha dhira zake mara tatu, kisha akapaka sehemu ya kichwa chake mara tatu, na akaingiza vidole vyake viwili vya shahada masikioni mwake, kisha akaosha miguu yake mara tatu, kisha akasema: “Hivi ndiyo wudhuu ulivyo, basi yule anayezidisha juu ya hivi au kupunguza hakika amefanya ubaya na amefanya dhulma.”¹⁰⁰

Na hadithi hii si ya kawaida, na amenukuu Ibn Rajab kutoka kwa Muslim kwamba amesema: Ijimai ni juu ya kinyume chake.

Na akasema Hafidh katika kitabu *al-Fat’hu*.¹⁰¹ [Sanad yake ni nzuri, lakini Muslim ameihasabu ni katika jumla ya zile zilizokataliwa kutoka kwa Amru bin Shuaib, kwa sababu dhahiri yake ni kulaumu kupunguza chini ya tatu. Ninajibu kuwa ni jambo la mtu binafsi, na uovu hufungamana na mapungufu, na dhulma hufungamana na ziada. Na yanaunga mkono hilo yale aliyoyapokea Nuaim bin Hamad kutoka katika njia ya Mutwalib bin Hantwab: “Wudhuu ni mara moja, mara mbili na mara tatu, akipunguza chini ya moja au kuzidisha zaidi ya tatu atakuwa amekosea.” Nayo haina sanadi yote (*mursali*) na wapokezi wake ni wakweli. Vile vile ninajibu kuhusu hadithi hii kwamba hakika wapokezi hawakuafikiana juu ya utajo wa mapungufu ndani yake, bali wengi wao wametoshaka na kauli yake “kuzidisha zaidi ya tatu” tu, na ni vivyo hivyo amepokea Ibn Khuzaima katika *sahihi* yake na wengi-neo.] Yamekwisha maneno ya Hafidh.

Nasema: Neno lisilo la kawaida katika hadithi hii ni “hakika amefanya ubaya na amefanya dhulma.” Na hadithi *mursali* ya Mutwalib bin Hantwab ndani yake kuna neno: “Hakika amekosea.” Na tamko hili ni la kawaida, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

¹⁰⁰ Ameipokea hiyo Twahawi katika kitabu *Sharhu Maanil-Athar* Juz. 1 uk. 36 na *Abu Daud* 135 na Bayhaqi katika kitabu *Sunanul-Kubra* Juz. 1, uk. 79 na akasema Hafidh Ibn Hajar katika kitabu *Fat-hul-Baari* Juz. 1, uk. 233: [Sanad yake ni nzuri lakini Muslim ameihasabu katika jumla ya zile zilizomchukiza mno kutoka kwa Amru bin Shuaib].

¹⁰¹ *Fat-hul-Baari* Juz. 1, uk. 233.

HADITHI YA THELATHINI NA SITA

Amepokea Abu Ya'ali kutoka katika njia ya Ali bin Zaid bin Juduan, kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Mbingu ilinyesha mvua na kuwa madonge ya barafu. Akatuambia sisi Abu Twalha wakati tukiwa ni vijana: “Ewe Anas nipe donge la barafu,” nikampatia akaanza kula naye akiwa katika swaumu, nikasema: Je, wewe si uko katika swaumu? Akasema: “Ndiyo niko katika swaumu, hakika hiki sio chakula wala kinywaji, hakika hii ni baraka kutoka mbinguni tunaji-toharishia sisi.” Anas anasema: Basi nikaenda kwa Mtume ﷺ ni-kampa habari juu ya hilo, akasema: “Chukua kutoka kwa baba yako mdogo.”¹⁰²

Hafidh Haythami katika kitabu *Majmaul-Zawaid*¹⁰³ amesema: Ali bin Zaid kuhusu yeye kuna maneno. Wamemzingatia kuwa ni mkweli, na wapokezi wake waliobakia ni watu sahihi.” Amesema: Ameipokea Bazar ikikomea kwa Swahaba, na akaongeza: “Basi ni-kataja hilo kwa Said bin Musayyib akalichukia hilo, na akasema: Hakika hayo yanakata kiu.”

Nasema: Ametaja Hafidh Ibn Rajab hadithi hii katika jumla ya hadithi zisizokuwa za kawaida, nayo ndivyo ilivyo, kwani ni tofauti na yaliyokubalika katika Swaumu. Na hakika wamekosea baadhi ya wale wenye kudai kuwa na elimu na wakafutu kuwa inapasa mgonjwa katika mwezi wa Ramadhani ameze dawa bila ya maji na wala hawi mwenye kufungua Swaumu. Wamefanya hivyo kwa kulinganisha na hadithi hii, nao ni ulinganishaji muovu kabisa wa kuzifanya hadithi zisizokuwa za kawaida kuwa ndio kipimo, na Mwe-nyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

¹⁰² Ameipokea hiyo *Abu Ya'ali* Juz. 3, uk. 15 na akaitaja hiyo Ibn Jawzi katika *Ilalul-Mutanaahiya* Juz. 2, uk. 545 na Daar Qutni katika *Ilal* Juz. 6, uk. 11.

¹⁰³ *Majmaul-Zawaid* Juz. 3, uk. 172.

HADITHI YA THELATHINI NA SABA

Ahmad amesema: Ametuhadithia Hamad: Ametusimulia Ali bin Zaid, kutoka kwa Yusuf bin Mihran, kutoka kwa Ibn Abbas, amesema: Alikufa Ruqayya binti ya Mtume ﷺ, akasema ﷺ: “Muunganisheni na mwema aliyetutangulia, Uthman bin Madhuun.” Ibn Abbas anasema: “Wakalia wanawake, basi akawa Umar akiwapiga wao kwa mjeledi wake. Mtume ﷺ akasema: ‘Waache ewe Umar na jiepusheni na uliaji wa Shetani. Chochote kitokacho jichoni na moyoni hutoka kwa Mwenyezi Mungu na ni rehema, na chochote kitokacho mkononi na ulimini ni kutoka kwa Shetani.’ Na akakaa juu ya kaburi huku Fatima akiwa pembezoni mwake akilia, akawa anafuta jicho la Fatima kwa nguo yake.¹⁰⁴ Dhahabi¹⁰⁵ amesema: “Hadithi hii ni yenye kuchukiza, ndani yake kuna maelezo yanayoonesha kuwa Fatima alishuhudia maziko, na wala haisihi.” Mwisho.

Nasema: Ndani yake kuna mambo yenye kuchukiza. Pia suala la kuhudhuria Mtume ﷺ maziko yake, ilihali alikufa hali ya kuwa Mtume ﷺ akiwa katika vita vya Badr, na akazikwa siku aliyofika Zaid bin Haritha akitoa bishara njema kwa ushindi wa Mtume ﷺ wa Badr juu ya washirikina, na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

HADITHI YA THELATHINI NA NANE

Amepokea Tirmidhiy kutoka kwa Jabir bin Abdillahi al-Answar رضي الله عنه amesema: “Tulikuwa tukihiji pamoja na Mtume ﷺ na tulikuwa tukiwafanyia talbiya wanawake.”¹⁰⁶ Tirmidhiy amesema: “Hadithi hii ni

¹⁰⁴ Ni dhaifu. Ameipokea Twayalisi katika *Musnad* yake uk. 351 na Ahmad Juz. 1, uk. 237 na 335 na Ibn Saad katika kitabu *Twabaqaat* Juz. 3, uk. 399 na Bazar 1022 na Daylami katika *Musnadul-Furdasi* Juz. 1, uk. 381 na Bayhaqi katika *Sunanul-Kubra* Juz. 4, uk.70 na Ibn Abdul-Barr katika *Istiiab* Juz. 3, uk. 1056.

¹⁰⁵ Katika *al-Mizaan* katika wasifu wa Ali bin Ziyad Yamaami.

¹⁰⁶ Ameipokea *Tirmidhiy* 927 na akamuona dhaifu huyo kwa kauli yake: Ni ngeni, na

ngeni, hatuijui ila katika njia hii, na hakika wamekongamanika watu wa elimu juu ya mwanamke kutoa talbiya yeye mwenyewe, wala hatolewi talbiya na mtu mwingine.”

Nasema: Tirmidhiy amebainisha kwamba hadithi hii si ya kawaida, kwa kuwa inatofautiana na ijimai.

HADITHI YA THELATHINI NA TISA

Abu Daud na Tirmidhiy wamepokea kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema: “Mwenye kumuosha maiti basi aoge, na mwenye kumbeba basi atie Wudhuu.”¹⁰⁷ Tirmidhiy amesema: Hadithi ya Abu Huraira رَوَاهُ ni hadithi nzuri, na hakika imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kwa kukomea kwake tu. Na hakika wametofautiana watu wa elimu kuhusiana na muoshaji maiti, basi wakasema baadhi ya watu wa elimu miongoni mwa Masahaba wa Mtume ﷺ na wengineo: Akimuosha maiti ni juu yake kuoga. Na wakasema baadhi yao: Ni juu yake kutia wudhu. Na amesema Malik bin Anas: “Ni mustahabu kuoga kutokana na kumuosha maiti na wala sioni hilo kuwa ni wajibu.” Na ndivyo alivyosema Shafi. Ahmad amesema: “Mwenye kumuosha maiti ninatarajia isiwe ni wajibu juu yake kuoga, na ama wudhuu, ndio la chini lililosemwa kumhusu.” Na amesema Is’haq: “Hapana budi kutia wudhu, na hakika imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Mubarak kwamba hakika yeye amesema: Asioge wala asitie wudhu kutokana na kumuosha maiti.”

Nasema: Maneno ya Ibn Mubarak ni sahihi, na hadithi hii si ya kawaida, hata kama madhumuni yake ni rai ya wanazuoni. Na saba-bu ya kuwa kwake ni hadithi isiyo ya kawaida ni yale aliyoyapokea Bayhaqiy katika *Sunnan* yake kutoka kwa Ibn Abbas رَوَاهُ, amese-

akataja hakika ijamai iko tofauti nayo.

¹⁰⁷ Sanad yake ni nzuri, ameipokea *Abu Daud* 3161 na *Tirmidhiy* 993 na *Ibn Majah* 1463. Nayo ni yenye kuchukuliwa kwa maana ya sunna.

ma: Mtume ﷺ amesema: “Hakuna juu yenu joshu lolote wakati wa kumuosha maiti wenu, hakika maiti wenu anakufa akiwa twahara na sio najisi, basi yawatosheni nyinyi kuosha mikono yenu.”¹⁰⁸ Na sanad yake ni nzuri kama vile alivyosema Hafidh.¹⁰⁹

HADITHI YA ARUBAINI

Amesema Tirmidhiy: Ametuhadithia Qutayba: Ametusimulia Abdullah bin Ja’far kutoka kwa Zayd bin Aslam, kutoka kwa Muhammad bin Munkadar, kutoka kwa Muhammad bin Kaab, amesema: Nilikwenda kwa Anas bin Malik رضى الله عنه wakati wa Ramadhan naye akiwa anataka kusafiri, na alikuwa ameshaletewa kipando chake na ameshavaa nguo yake ya safari. Basi akaitisha chakula na akala, nikamuuliza yeye: Je, hii ni sunna?! Akasema: Ni sunna, kisha akapanda.¹¹⁰

Vile vile amesema: Ametuhadithia Muhammad bin Ismail: Ametusimulia Said bin Abi Maryam: Ametuhadithia Muhammad bin Jafar: Amenihadithia Zaid bin Aslam: Amenisimulia Muhammad bin Munkadar, kutoka kwa Muhammad bin Kaab amesema: Nilikwenda kwa Anas bin Malik رضى الله عنه katika mwezi wa Ramadhan. . . . basi akataja mfano wa maelezo yaliyotangulia. Tirmidhiy amesema: “Hadithi hii ni nzuri, na hakika wameifanyia kazi baadhi ya watu wa elimu hadithi hii, na wakasema: Msafiri anafuturu nyumbani kwake kabla hajatoka, na hapasi yeye kupunguza Swala mpaka atoke nje ya ukuta wa mji, au kijiji, nayo ni kauli ya Is’haq.”

¹⁰⁸ Mualal sio sahihi, ameipokea *Daar Qutni* Juz. 2, uk. 76 na ameitaja Dhahabi katika *Al-Mizaan* katika wasifu wa Khalid bin Mukhalid, na vivyo hivyo katika wasifu wa Amru bin Abi Amru.

¹⁰⁹ Katika *Talkhiiswu* Juz. 1, uk. 137 na kuifanya *hasan* hiyo ni kosa kutoka kwa Hafidh Ibn Hajar na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi.

¹¹⁰ Ameipokea *Tirmidhiy* 799, na akasema ni nzuri.

Nasema: Hadithi hii si ya kawaida, kwani hiyo inafaidisha ruhusa ya msafiri kufungua kabla ya kuanza safari, kwani kufungua kunakuwa ruhusa pindi mfungaji akiwa ameanza safari. Na haijakuja hadithi inayoafikiana nayo katika hili. Nayo pia inatofautiana na maana ya ruhusa, kwani mfungaji anaruhusiwa kufungua anapokuwa safarini, na ama kabla ya kuanza safari hafungui. Na ama yale ambayo ameyapokea Ahmad na Abu Daud kutoka kwa Ubaid bin Jabar akisema: “Nilipanda pamoja na Abu Baswra Ghafari katika jahazi kutoka mji wa Fistat katika mwezi wa Ramadhani, akatoa na akasogeza karibu chakula chake, kisha akasema: Karibia, nikasema: Je, sio baina ya nyumba nyingi? Abu Baswra akasema je, unaacha Sunna ya Mtume ﷺ?”¹¹¹

Katika hadithi hii kuna maelezo kuwa Abu Baswra alisogeza karibu chakula chake cha mchana baada ya kuanza safari, kwa dalili ya kauli yake “akatoa na akasogeza karibu chakula chake” kwa sababu maana yake kama ilivyo katika hadithi ya Ahmad ni: “Tulipotoa chakula chetu.” Na hili linaafikiana na yale yaliyopo katika *Sahihi Bukhari* kutoka kwa Abu Abbas, amesema: Alitoka Mtume ﷺ katika mwezi wa Ramadhani hadi katika vita vya Hunain huku watu wakitofautiana. Wapo wenye kufunga na wenye kufuturu, na pindi alipotulia juu ya kipando chake, akaitisha chombo cha maziwa au

¹¹¹ Amejipokea hiyo *Daar Qutni* 1713, na *Ahmad bin Hanbali* Juz. 6, uk. 398, na *Abu Daud* 2412, na Twabarani katika *Muujamul-Kabiir* Juz. 2, uk. 279, na Bayhaqi katika *Sunanul-Kubra* Juz. 4, uk. 246, nayo haisihi kutokana na upande wa sanad, kwa sababu ndani yake yupo Kaliib bin Dhuhul Khadhrami. Na anayo hadithi kwa *Ahmad* Juz. 6, uk. 7 kutoka katika njia ya Yazid bin Abi Habibi, kutoka kwa Abu Baswra, nayo ni yenye kukatika baina ya Yazid na Abu Baswra. Daar Qutni amesema katika kitabu *Ilal*: “Hakusikia kutoka kwa Ibn Amru wala kutoka kwa yeyote miongoni mwa masahaba.” Kama ilivyo katika mstari wa pambazoni mwa kitabu *Tahdhiibul-Kamaal* Juz. 32, uk. 106. Na hadithi ni yenye kupokewa kutoka njia nyingine kwa *Abu Daud* 2413 na *Ahmad* Juz. 6, uk. 398, nayo ni njia ya Yazid bin Habibi kutoka kwa Abu Khayr, kutoka kwa Mansur Kalabi, kutoka kwa Dahiyat bin Khalifa. Na Mansur bin Said Kalabi hajulikani, kama ilivyo katika *Tahdhiibul-Tahdhiib* Juz. 10, uk. 373 kutoka kwa Ibn Maniini na Ibn Khuzayma.

maji akayaweka juu ya kipando chake au juu ya kikalio chake, kisha akawaangalia watu akasema: “Waliofungua waambieni waliofungua: Fungueni.”

Na Anas bin Malik رضي الله عنه alifuturu kabla ya kuanza safari, hivyo basi hadithi yake inakuwa ni kati ya hadithi zisizokuwa za kawaida. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

HADITHI YA ARUBAINI NA MOJA

Abu Daud na Tirmidhiy wamepokea kutoka katika njia ya Hamad bin Salama kutoka kwa Abu Ashara, kutoka kwa baba yake, amesema: Nikasema ewe Mtume uchinjaji si hauwi ila katika koo na mfupa wake? Akasema ﷺ: “Hata kama utamchinja pajani kwake itatosheleza.”¹¹²

Hadithi hii si ya kawaida kwani imetofautiana na hadithi chungu tele ambazo zinafaidisha kwamba uchinjaji hufanyika kooni, na hakika wanazuoni wameitolea maana nyingine, na wamefanya hivyo ili kuiondoa katika hali ya kutokuwa ya kawaida.

Abu Daud amesema baada ya hadithi hii: “Halifai hili ila kwa mnyama pori mkali.” Na Tirmidhiy amesema: Ahmad bin Munii amesema: Yazid bin Haruna amesema: “Hili hufanyika wakati wa dharura.” Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

HADITHI YA ARUBAINI NA MBILI

Kutoka kwa Anas bin Malik ﷺ amesema: Mtume ﷺ amesema: “Alinjia Jibrail na kiganjani kwake kipo kitu kama vile kioo cheupe alichokibeba, na ndani yake kama vile nukta nyeusi, nikasema: Ewe Jibrail ni kitu gani kipo mkononi kwako? Akasema: Hii ni Ijumaa,

¹¹² Dhaifu. Wameipokea waandishi wengi wa vitabu vya hadithi na miongoni mwao ni: Tirmidhiy 1481 na Nasaai 4408 wote kutoka njia ya Hamad bin Salama kutoka kwa Abu Ashara na jina lake ni Usama bin Malik bin Qahtwam kutoka kwa baba yake, na Abu Ashara huyu hajulikani, akasema Bukhari katika kitabu chake Tariikhul-Kabiir Juz. 2 uk.21: “katika hadithi yake na jina lake na usikilizaji wake kutoka kwa baba yake yafaa uchunguzi.” Na akasema Ibn Saad: “Ni mtu hajulikani”, na hii ndiyo aliyotegemea Hafidh Ibn Hajar katika kitabu Taqriib na huo ndiyo ukweli, na ama Hamad ni lipi litakujulisha ni nani Hamad!! Na ameipokea Twabarani katika kitabu Awsat Juz. 5 uk. 131 kutoka katika njia nyingine ndani yake wapo wengi wasiojulikana yupo Bakr bin Sharuud, wasifu wake umo katika kitabu Lisaanul-Mizaan Juz. 2 uk. 52 na hakika Ibn Maiin amemtuhumu kwa uongo.

Mola Wako Mlezi anakuonesha wewe ili iwe Iddi kwako na kwa kaumu yako hapo baadaye, utakuwa wewe wa kwanza na watakuwa Mayahudi na Manaswara baada yako.” Akataja fadhila za Ijumaa mpaka aliposema:

“Hakika Mola Wako Mlezi amefanya makazi yake peponi kwenye bonde ambalo pananukia mahala hapo zaidi ya miski nyeupe. Na inapofika Siku ya Ijumaa huteremka (s.w.t) kutoka mahala pa juu, akiwa juu ya kiti Chake cha enzi mpaka kiti Chake kinapozungukwa na majukwaa ya nuru, hapo huja Mitume na kukaa juu ya majukwaa hayo. Kisha kiti Chake huzungukwa na majukwaa ya dhahabu, na hapo huja wakweli na mashahidi na kuketi juu ya majukwaa hayo. Kisha huja watu wa peponi na kuketi sehemu ya karibu, na mara Mola Wao hujidhihirisha kwao kiasi kwamba wao huutazama uso wake, naye husema: ‘Mimi ni yule ambaye nimekutimizieni ahadi Yangu na neema Yangu, hapa ni mahali pa karama Yangu.’ Basi wao humuomba Yeye ridhaa, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) husema: ‘Ridhaa Yangu ndio iliyokufikisheni katika nyumba Yangu na kukupeni karama Zangu, basi niombeni mimi.’ Hapo wao humuomba yeye mpaka yanaisha watakayo, na hapo wao hufunguliwa yale ambayo jicho halijawahi kuona, wala sikio kusikia, wala moyo wa mtu kuwaza, mpaka kiwango cha kuwatosha watu wa siku ya Ijumaa. Kisha Mola Manani (s.w.t) hupanda juu ya kiti Chake cha enzi na hapo mashahidi na wakweli hupanda pamoja Naye.”¹¹³

“Bazar na Twabarani katika kitabu *Awsat* wameipokea kwa mfanano huo, na moja ya sanad mbili za Twabarani, wapokezi wake ni watu sahihi isipokuwa Abdul-Rahman bin Thabit ibn Thuuban, na hakika zaidi ya mmoja wamemzingatia kuwa ni mkweli, na wengine wakamuona kuwa ni mtu dhaifu, na katika sanad ya Bazar kuna

¹¹³ Ni hadithi iliyobuniwa bila shaka. Hadithi ya kioo ni yenye kutungwa kwa pande zote, na hakika nimebainisha hilo katika utoaji maelezo wa kitabu *Al-Uluwu* uk. 159-169 cha Dhahabi hadithi nambari 40-43.

tofauti.” Hafidh Haythami amesema hayo katika kitabu *Majmauz-Zawaid*.¹¹⁴

Nasema: Hadithi hii si ya kawaida, kwani inamnasibisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) na uteremkaji, upandaji na ukaaji juu ya kiti, mambo ambayo kiakili na kisharia hayafai kumnasibisha nayo Mwenyezi Mungu (s.w.t), na inajulikana kwa dharura katika dini kwamba hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) haifai kabisa kumsifu kwa sifa za viumbe mfano wa uteremkaji, upandaji na utembeaji na kuwa na harakati zozote zile kama anavyosema: ‘Hafanani na chochote’ (Sura Shura:11). Hivyo hadithi ambayo inafaidisha kitu miongoni mwa sifa hizo inakuwa si ya kawaida na ni yenye kukataliwa hata ikithibiti kwa usahihi wa sanad zake.

Na hakika Suyutwi katika *Durrul-Manthur* ameitaja hadithi hii na akaitukuza kwa watoaji wengi, na akasema: “Kwa upande wa sanad zake ni *Jayidi*.” Na Suyutwi hategemewi katika hili kwa upuu-ziaji wake mkubwa. Na dalili juu ya hilo ni kwamba hakika yeye ametajwa miongoni mwa waliopokea hadithi za Imam Shafi,¹¹⁵ na Sheikh wake ni mwenye kuachwa. Na Ibn Abi Duniya aliyopo katika sanad yake ni mpokezi dhaifu, na iweje isihi kauli yake kuwa sanad hiyo ni nzuri?!

Na *Jayidi* kwa watu wa elimu ni bora zaidi kuliko *hasan*, hakika ametaja Hafidh Iraqi: Hakika Hafidh mkosoaji ikiwa atapata sanad ya hadithi iliyo juu ya *hasan*, na akawa na shaka kuwa haijafikia daraja la kusihi, basi huiita *Jayidi*. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwafikishaji.

¹¹⁴ *Majmaul-Zawaid* Juz. 10, uk. 422 na maneno ya Haythami sio sahihi kama nilivyo-libainisha hilo katika utoaji wa maelezo juu ya kitabu *Al-Uluwu* uk. 169-170.

¹¹⁵ Kitabu *Al-Ummu* Juz. 1, uk. 185 na hakika nimezungumza juu yake na nikabainisha kuwa hiyo ni yenye kubuniwa na kuzushwa, nimebainisha hilo katika utoaji wa maelezo juu ya *Al-Uluwu* uk. 166.

HADITHI YA ARUBAINI NA TATU

Muslim amepokea katika *Sahih* yake kutoka kwa Aisha Okwamba amesema: “Hakika ilikuwa katika yale yaliyoteremshwa ndani ya Qur’ani ni Aya ‘Unyonyeshaji mara kumi unaharamisha,’ kisha ikafutwa kwa Aya tano zilizojulikana. Basi akafariki Bwana Mtume ﷺ na hali Aya hiyo ikiwa ni kati ya zile zinazosomwa kutokana na Qur’ani Tukufu.”¹¹⁶

Hadithi hii si ya kawaida, kwani imefaidisha ufutwaji wa usomaji wa baadhi ya Aya za Qur’ani na ufutwaji wa Qur’ani ni muhali kiakili. Na kila hadithi inayofaidisha yale yasiyokubalika kiakili, basi hiyo ni katika zisizokuwa za kawaida, na hakika nimeandika juuzuu niliyoiita *Dhawqul-Halawat Bibayan Imtinai Naskhul-Tilawat*, nimebainisha ndani yake sababu tisa zilizopelekea kuwa muhali ufutwaji wa usomaji.

Na kati ya hizo ni: Ufutwaji wa usomaji unalazimu utokezo, nao ni kudhihiri kwa maslahi katika ufutaji wa Aya baada ya kufichika kwake, na utokezo katika haki ya Mwenyezi Mungu ni muhali.

Na kati ya hizo ni: Kubadilika tamko kwa kuwa lingine, au kulifuta kwa ujumla wake kunanasibiana na viumbe kutokana na upungufu wa elimu yao na kutozingira kwao maarifa, wala hayamhusu Mwenyezi Mungu ambaye anajua ya siri na yaliyojificha.

Na kati ya hizo ni: Hakika yale yaliyosemwa kuwa ilikuwa ni Qur’ani na ikafutwa lafudhi yake, hatukuti ndani yake mitindo ya Qur’ani, na wala usomaji wake, wala kengele ya lafudhi yake.

Na kati ya hizo ni: Yale yaliyokubaliwa katika elimu ya Misingi ya Sharia, kwamba: Hakika Qur’ani tukufu haithibiti ila kwa tawa-

¹¹⁶ Ni batili. Ameipokea hiyo *Muslim* 1452 na *Nasaai* 3307 na *Abu Daud* 2062 na wengineo. Akasema Hafidh ibn Hajar katika *Fat’hul-Baari* Juz. 9, uk. 147 kutokana na hadithi hii: [Haisimami juu kuwa hoja sahihi zaidi kuliko kauli za wanausuul, kwa sababu Qur’ani haithibitishwi ila kwa tawaturu].

turi, na ambalo sio katika tawaturi, haliwi Qur’ani, na sentensi ambazo zimesemwa kuwa zilikuwa ni Qur’ani, zimepatikana kwa njia ya mtu mmoja, nazo si za kawaida, haifai kuzisoma.

Na kati ya hizo ni: Hakika Qur’ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu nayo ni ya tangu na tangu, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۚ لَا مُبَدَّلَ لِكَلِمَاتِهِ ۗ وَهُوَ
السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

“Na limetimia neno la Mola Wako kwa ukweli na uadilifu; hakuna wa kubadilisha neno Lake. Na Yeye ni Msikizi, Mjuzi.” (Sura An’aam; 6:115), na kanuni iliyokubaliwa katika elimu ya itikadi ni kwamba: Hakika lililothibiti utangu wake, ni muhali kutokuwepo kwake, na vipi ifae pamoja na ufutaji huu wa Aya ya Qur’ani. Je, inafaa kusemwa kuwa: Yakiwa maneno ya Mwenyezi Mungu ni ya tangu na tangu, basi sasa sio maneno yake, hilo ni muhali, na kwa Mwenyezi Mungu tunaomba taufiki.

Hadithi hizi arubaini na tatu nilizozitaja ni mifano tu kati ya nyingi na zenye anuani mbalimbali, na zimebakia hadithi nyingi tu zisizokuwa za kawaida. Amezitaja baadhi yake Hafidh Ibn Rajab katika kitabu *Sharhu Ilalul-Tirmidhiy*, na baadhi yake zipo katika vitabu vya Sunna. Anaziona na kuziacha hizo mwenye kuzifuatilia.

Na hakika limethibiti katazo dhidi ya hadithi zisizokuwa za kawaida. Kati ya yale aliyoyapokea Ahmad bin Hanbali kutoka kati-ka njia ya Alaau bin Ziyad, kutoka kwa mtu anayemwamini, kutoka kwa Maadh (r.a), ni kwamba amesema: Mtume ﷺ amesema: “Hakika Shetani ni mbwa mwitu wa binadamu kama vile alivyo mbwa

mwitu wa mifugo, anachukua mbuzi wa nyuma na aliyejitenga. Basi msiachane na jamaa. Ni juu yenu kushikamana na jamaa, umma na msikiti.”¹¹⁷

Na akasema Ahmad: Ametuhadithia Is’haq bin Sulaiman Raazi, akasema: Nilimsikia Zakaria bin Salam akihadithia kutoka kwa baba yake, kutoka kwa mtu, akasema: Nilifika kwa Mtume ﷺ naye akiwa anasema: “Enyi watu! Ni juu yenu kushikamana na jamaa, na jiepusheni na mfarakano. Ni juu yenu kushikamana na jamaa, jiepusheni na mfarakano. Ni juu yenu kushikamana na jamaa, jiepusheni na mfarakano.”¹¹⁸

Na amepokea Tirmidhiy na Hakim kutoka kwa Ibn Umar kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu haukusanyi umma wangu juu ya upotovu, na mkono wa Mwenyezi upo pamoja na jamaa na mwenye kuiacha na kwenda peke yake basi huyo ni wa motoni.”¹¹⁹

Na kuna njia nyingi kwa Hakim, na lafudhi yake katika moja wapo ni: “Mwenyezi Mungu hawakusanyi maimamu hawa kwenye upotovu kamwe, na mkono wa Mwenyezi Mungu upo juu ya jamaa

¹¹⁷ Sanad yake ni dhaifu na matini yake ni yenye kuchukiza. Amejipokea Ahmad bin Hanbali Juz. 5, uk. 232 nayo ni yenye kukatika ambayo ni kati ya Alaau bin Ziyad na bwana wetu Maadh (r.a)! Basi hadithi ni dhaifu. Akasema Haythami katika *Al-Majmau* Juz. 2, uk. 23: “Amejipokea Ahmad, na Alaau bin Ziyad hakusikia kutoka kwa Maadh”

¹¹⁸ Sanad yake ni dhaifu. Amejipokea hiyo Ahmad bin Hanbali Juz. 5, uk. 370, na hii ni yenye kukatika pia.

¹¹⁹ Ni yenye kuchukiza aliyopokea *Tirmidhiy* 2167 na akamuona ni dhaifu kwa kauli yake: “Hadithi hii ni ngeni.” Na akaitaja Abu Twalib Qadhi katika *Ilalul-Tirmidhiy* uk. 323, na katika sanad yake yupo Suleiman Madani naye ni mtu dhaifu, na akasema Ibn Abi Hatam katika *Jarhu wa Ta’adil* Juz. 4, uk. 119: “Aliulizwa Abu Zar’at kuhusu Abu Sufiyan Suleiman bin Sufiyan akasema: Madani ni mwenye hadithi zenye kuchukiza. Zimepokewa kutoka kwa Abdullah bin Dinar hadithi tatu zote anataja wapokezi hewa kwenye sanadi, na ni zenye kuchukiza.” **Nasema:** Na hadithi hii inatokana na hizo, nayo ni kutoka kwa Abdullah bin Dinar. Na Hakim wakati amejipokea hiyo katika Juz. 1, uk. 115-116 hakuizingatia kuwa ni sahihi bali alitoa ishara kwa kutokusihhi kwake.

basi fuateni weusi adhimu zaidi, kwani mwenye kwenda peke yake huingia motoni.”¹²⁰

Na hadithi ina njia nyingi. Nimeitoa katika kitabu *Ibtihaaaju Bi Takhrij Ahadiithil-Minhaaj* nayo ni miongoni mwa dalili za watu wa Misingi ya Sharia katika kuthibitisha hoja ya Ijimai. Ama maana ya hadithi isiyo ya kawaida kiistilahi, hakika wametofautiana katika utambulisho wake. Amesema Imam Shafi na wengineo: “Ni ile ambayo ameipokea mkweli yenye kwenda kinyume na hadithi ya watu wengi.”

Na amesema Hafidh Abu Ya’ali Khalili, mwandishi wa kitabu *Irshad*: “Na ambalo juu yake mahafidhi wa hadithi wamekubaliana ni kwamba hadithi isiyo ya kawaida ni ile isiyo na sanad zaidi ya moja, ambayo kajitenga pamoja nayo mkweli au mwingine. Basi kile kinachotoka kwa asiye kuwa mkweli ni chenye kuachwa, na ambacho kinatoka kwa mkweli wao hukinyamazia na wala hawakitolei hoja.”¹²¹

Na akasema Hafidh Suyuti katika *Tadriibul-Raawi*,¹²² baada ya uelezaji wa wazi wa kauli na maneno na vipimo: “Na tija ni kwamba isiyokuwa ya kawaida ni yenye kurudishwa, nayo ni ile ya pekee inayokwenda kinyume, na ya pekee ambayo katika wapokezi wake hakuna wakweli na wadhibiti ambao wanalazimisha kuondoa up-eeke wake.”

¹²⁰ Ameipokea *Hakim* Juz. 1, uk. 115 na akaashiria kutosihi kwake. Hakuna shaka hakika ijimai ni hoja, na baadhi ya yale yaliyotajwa kutokana na hadithi kuhusiana na ijimai ni sahihi. Na yanatosha yale aliyoyapokea *Hakim* katika Juz. 1, uk. 116 kutokana na hadithi ya Ibn Abbas: “Mwenyezi Mungu haukusanyi umma wangu kwenye upotovu kamwe, na mkono wa Mwenyezi Mungu upo juu ya jamaa,” nayo ni sahihi.

¹²¹ Na rai hii ni yenye nguvu zaidi mno kwetu sisi, na hususan katika hadithi za sifa za Mwenyezi Mungu.

¹²² Kitabu *Tadriibul-Raawi* Juz. 1, uk. 236, na asili yake katika kitabu *Sharhu Muslim* cha Imam Nawawi Juz. 1, uk. 34, na *Minhalul-Ruwiya* Juz. 1, uk. 50.

Na zisizokuwa za kawaida ambazo nimezitaja katika juzuu hii, zipo ambazo zimetofautiana na Qur’ani tukufu, na zipo ambazo zimetofautiana na hadithi mutawatiri, na zipo zile zilizotofautiana na ijimai, na zipo zile ambazo zimetofautiana na kanuni miongoni mwa kanuni zilizokubalika.

Na wanazuoni wamekataza kupokea hadithi zisizokuwa za kawaida. Ibrahim bin Abi Ubla¹²³ amesema: “Mwenye kubeba hadithi zisizokuwa za kawaida huyo amebeba shari kubwa.”

Na Muawiya bin Qurrat amesema: “Jiepushe na hadithi zisizokuwa za kawaida miongoni mwa elimu.”

Shuuba amesema:¹²⁴ “Haikujii wewe hadithi isiyokuwa ya kawaida ila kutoka kwa mtu asiyekuwa wa kawaida.”

Na Abdul-Rahman bin Mahdi¹²⁵ amesema: “Hawi Imam katika elimu, yule anayehadithia hadithi zisizokuwa za kawaida.”

Na amepokea *Bayhaqiy* kutoka kwa Ibn Wahab¹²⁶ kwamba amesema: “Kama si Malik bin Anas na Layth bin Saad ningeliangamia. Nilikuwa ninadhani kwamba kila ambalo limekuja kutoka kwa Mtume 3 linatendewa kazi.” Yaani hakika hao wawili walimbainishia kuwa hadithi haitendewa kazi ikiwa ni kati ya zile zisizokuwa za kawaida au ngeni, na hii ndio maana ya kauli ya Ibrahim Nakhai: “Hakika mimi ninasikia hadithi basi ninaichukua ile ambayo huchukuliwa, na ninaziacha nyinginezo.”¹²⁷ Na hakika katika kitabu

¹²³ *Sayru Aalaam Nubalaai* Juz. 6, uk. 324 cha Dhahabi, na *Tahdhiibul-Kamaal* Juz. 2, uk. 144.

¹²⁴ Angalia kitabu *Kifayat* uk. 141 cha Khatiib Baghdadi na kitabu *Tadriibul-Raawi* Juz. 1, uk. 339.

¹²⁵ Kitabu *Hiylatul-Awliyaai* Juz. 9, uk. 4.

¹²⁶ Kitabu *Tahdhiibul-Kamaal* Juz. 24, uk. 270 cha Hafidh Mazzi.

¹²⁷ Ameipokea Ibn Ju’ud katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 129 kutoka katika njia ya Aamash, na Abu Naim katika *Al-Hilyat* Juz. 4, uk. 225, na Dhahabi katika *Sayr Aalaam Nubalaa* Juz. 6, uk. 234.

Ifraadu wal-Gharaaib yameandikwa mengi kutoka kwa Mahafidhi, na kadiri nijuavyo ni kwamba hakuna hata mmoja kati yao aliyeandika kuhusiana na hadithi zisizokuwa za kawaida. Na juzuu hii ni ya kwanza kuandikwa kuhusiana na hilo. Basi sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu juu ya fadhila zake, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwezeshaji.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Uboru wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-Ilaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqaalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kitiikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhaliifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebicho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

FAIDA ZENYE KUKUSUDIWA KATIKA KUBAINISHA
HADITHI ZENYE KUKATALIWA

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitua Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukosoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo (Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi